

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Nane – Tarehe 14 Aprili, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 64

Kampuni Zinazofanya Kazi Ndani ya Mgodi wa Geita

MHE. UPENDO F. PENEZA aliuliza:-

Kampuni ambazo zinafanya kazi ndani ya Mgodi wa *Geita Gold Mine*(contractors) zimekuwa zikilalamikiwa na wananchi wanaofanya kazi kwa kutopeleka fedha kwenye Mifuko ya Jamii na kutowapa mikataba:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kukomesha malalamiko hayo?

WAZIRI MKUU alijibu:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa *Geita Gold Mine (GGM)* ni moja ya waajiri walioandikishwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) na watumishi wanaofanya kazi katika mgodi huo wamegawanyika katika makundi mawili ambayo ni wale walioajiriwa moja kwa moja na *GGM* na wale walioajiriwa na wakandarasi wanaotoa huduma ndani ya mgodi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari 2020, jumla ya shilingi bilioni 5.01 zililipwa na Mgodi wa *GGM* kama mchango wa mwezi Januari, 2020 kwa watumishi 2,038 walioajiriwa moja kwa moja na *GGM* na kuandikishwa na *NSSF*. Katika mwezi huo huo, jumla ya wanachama 6,128 ambaao wameajiriwa na wakandarasi 39 wanaotoa huduma ndani ya mgodi huo walikuwa wameandikishwa na *NSSF* na kuchangiwa wastani wa shilingi bilioni 1.3

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia OWM-KVAU imekuwa ikifanya kaguzi katika maeneo mbalimbali ya kazi ikiwemo ya migodini kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa Sheria za Kazi. Kupitia Ofisi ya Kazi ya Mkoa wa Geita, ukaguzi katika Mgodi wa *Geita Gold Mine* ikiwemo kandarasi zinazofanya kazi chini ya Kampuni hiyo umekuwa ukifanyika ili kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi katika maeneo hayo. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, ukaguzi umefanyika katika Kampuni za *Geita Gold Mine, Africa Underground Mining Services, Capital Drilling, GHP Transportaton, Security Group Africa, Fabec Construction, GIPCO Construction, East Africa Radiators, Paulando Enterprises, AVLOW (T) Ltd na EPSON Ltd*. Aidha, baada ya ukaguzi huo hatua stahiki kwa mujibu wa sheria zimechukuliwa ikiwemo kuwapatia Amri Tekelezi waajiri waliobainika kukiuka sheria za kazi na baadhi ya wafanyakazi raia wa kigeni kufutiwa vibali vyao vya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi yangu itaendelea kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha maelekezo yanayotolewa yanazingatiwa ipasavyo na hivyo kuimarisha mahusiano mema baina ya waajiri na wafanyakazi katika maeneo hayo.

Na. 65

Kumalizia Vituo vya Afya vya Jimbo la Mufundi Kusini

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vituo vya Afya katika Kata za Mbalamaziwa, Mninga na Kata ya Mtwango?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufundi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/20, Kituo cha Afya Mbalamaziwa kimetengewa shilingi milioni 50 kwa ajili ya kujenga wodi na tayari jengo la huduma kwa wagonjwa wa nje (*OPD*) limekamilika na kuanza kutumika. Kituo cha afya Mtwango kilipokea shilingi milioni 10 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa *OPD* na ujenzi umekamilika. Kituo cha Afya Mninga kilipokea shilingi milioni 20 katika mwaka fedha 2018/2019 kwa ajili kukamilisha jengo la huduma kwa wagonjwa wa nje (*OPD*) na nyumba ya mtumishi ambapo ujenzi wa jengo la *OPD* umekamilika na ujenzi wa nyumba ya mtumishi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imeweka kipaumbele cha kuendelea na ujenzi wa vituo vya afya na zahanati katika Halmashauri zote 184 ili kuboresha huduma za afya.

Na. 66

Halmashauri Kuweza Kukopesha SACCOS za Vijana na Wanawake

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini Serikali itafanya marekebisho ya sheria ili kuruhusu Halmashauri kuweza kukopesha *SACCOS* za wanawake na vijana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAAalijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais-TAMISEMI inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Vikundi vya Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambavyo vinapatiwa mikopo isiyo na riba kwa makundi ya vijana (4%), wanawake (4%) na watu wenye ulemavu (2%).*SACCOS*ni vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa ambavyo vinaongozwa na Sheria ya Vyama vya Ushirika, Na.6 ya mwaka 2013 na zipo katika mfumo rasmi unaoziwezesha kupata mikopo katika taasisi mbalimbali za fedha.

Na. 67

Uvamizi wa Maeneo ya Wakulima - Bagamoyo

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWAaliuliza:-

Katika miaka ya karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la wafugaji kuingiza mifugo yao kwa wingi sana bila kufuata utaratibu katika Kata za Jimbo la Bagamoyo na kusababisha usumbu kwa wakulima na kuathiri shughuli za kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti hali hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAAalijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kudhibiti wimbi la uingizaji wa mifugo holela ni pamoja na kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji vitatu vya Fukayosi, Kidomole na Mkenge; kuzuia uingiza wa mifugo kwenye vijiji pasipo kibali kutoka Halmashauri; na kuondoa mifugo iliyoingia pasipo kufuata taratibu ambapo katika kipindi cha mwaka 2019 jumla ya maboma nane yenye ng'ombe 1,255 yaliondolewa kwenye Kijiji cha Mwavi.

Na.68

Kuwawezesha Wakulima wa Parachichi – Kagera

MHE. CHARLES J. MWIJAGE aliuliza:-

Wakulima wa Mkoa wa Kagera wamehamasika kulima zao la parachichi kwa ajili ya biashara lakini wanakwazwa na gharama za miche na elimu:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wakulima hawa kupata miche mingi ili kuzalisha matunda mengi na kuvutia soko la kimataifa?

(b) Kwa kuwa zao hili linamahitaji ya kitaalam katika kulima mpaka kuvuna; je, kwa nini Serikali isiwapatie mafunzo maalum wataalam angalau wawili katika kila Wilaya ya Mkoa wa Kagera ili waweze kuwaongoza wananchi ambao wamedhamiria kulima zao hili?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la maparachichi ni moja kati ya mazao ya asili ya matunda yanayozalishwa katika Mkoa wa Kagera na wakulima wengi wamehamasika

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kuzalisha zao hilo kutokana na kuwepo kwa soko la kimataifa la parachichi hususan aina za HASS na FUERTE. Katika kuhakikisha kuwa wakulima wa parachichi Mkoani Kagera wanapata miche bora, Wizara ya Kilimo kupitia Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha TARI - Maruku imeendelea kuzalisha na kusambaza miche bora ya parachichi katika Halmashauri za Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2018/2019, Kituo cha Utafiti Maruku kilizalisha na kusambaza miche 4,000 ya zao la parachichi kwa wakulima wa Halmashauri za Karagwe, Misenyi na Muleba. Aidha, katika msimu wa 2019/2020, Kituo cha TARI Maruku kitazalisha miche ya parachichi 10,000 itakayosambazwa na kuuzwa kwa wakulima wa Mkoa wa Kagera kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya za Mkoa wa Kagera imeendelea kutoa elimu kuhusu uzalishaji wa miche bora ya zao la parachichi kuititia Maonesho ya Nanenane msimu wa mwaka 2019/2020 na Maafisa Ugani wanne (4) kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi walipatiwa elimu ya uzalishaji wa miche bora ya parachichi. Vilevile, wakulima zaidi ya 300 walipatiwa elimu ya uzalishaji wa zao la parachichi kuititia Maonesho ya Wiki ya Uwekezaji Mkoani Kagera yaliyofanyika mwezi Agosti, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kuititia TARI - Maruku kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Kagera zimeandaa mpango wa mafunzo kwa wataalam wa kilimo katika Halmashauri za Mkoa wa Kagera kuhusu mbinu bora za uzalishaji wa zao la parachichi ili waweze kutoa elimu hiyo kwa wakulima wa zao la parachichi.

Na. 69

Hitaji la Wataalam wa Kilimo na Bodi ya Zao la Zabibu

MHE. JOEL M. MAKANYANGA aliuliza:-

Dodoma kwa kiasi kikubwa na muda mrefu imekuwa ikitegemea sana zabibu kama zao la biashara:-

(a)Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wataalam wa kilimo cha zabibu wanapatikana ili kuwasaidia wakulima wa zabibu?

(b)Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Bodi ya Zabibu ili kukuza kilimo cha zabibu?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyanga, Mbunge wa Jimbo la Chilonwa, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo TARI -Makutupora ina jukumu la kuzalisha na kusambaza teknolojia bora za kilimo cha zabibu ikiwemo kuhakikisha wataalam wa kilimo cha zabibu katika Mkoa wa Dodoma na maeneo mengine nchini wanajengewa uwezo ili kuwasaidia wakulima wa zabibu. Katika mwaka 2019 Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wadau wengine kama Kilimo Endelevu Tanzania (*Sustainable Agricultural Tanzania*) na Faida Mali imefanikiwa kusambaza teknolojia bora za zabibu kwa wakulima na wadau mbalimbali 3,065 katika Kata za Chihanga na Makutupora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza utaalam kwa watafiti wa TARI-Makutupora kuhusiana na taaluma ya mizabibu, Taasisi hiyo imeendelea kuwawezesha watalaam wake kupata mafunzo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kwenye nchi zilizobobe katika kilimo cha mizabibu kama vile Afrika Kusini na Ujerumani. Aidha, utaalam na uzoefu utakaopatikana utafikishwa kwa wagani na wakulima wa mfano ili kuzalisha zao hilo kwa tija na kulingana na vigezo vya masoko.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo inatambua umuhimu wa chombo au taasisi ambayo ingefaa

kusimamia kwa karibu uendelezaji wa zao la zabibu. Hata hivyo, kwa sasa Wizara haina mpango wa kuanzisha Bodi ya Zabibu, badala yake Wizara ipo kwenye hatua za awali za mapendekezo ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mazao ya Bustani. Aidha, zao la zabibu litakuwa ni mojawapo ya mazao yatakayoendelezwa chini ya usimamizi wa mamlaka hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo imeendelea kuweka mikakati ya kusimamia na kuendeleza zao la zabibu kufikia mwaka 2024/2025 ikiwemo kuongeza upatikanaji wa masoko kutoka 65% hadi 85%; kuongeza tija ya uzalishaji kutoka tani 6.25 kwa hekta hadi tani 20 kwa hekta; kuimarisha uwezo wa *TARI* - Makutupora kuzalisha miche bora kutoka miche 100,000 kwa msimu hadi miche 300,000 kwa msimu; kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika tasnia ya zabibu pamoja na kutenga na kulinda ardhi kwa ajili ya kilimo cha zabibu.

Na. 70

Mafunzo Kwa Askari Polisi

MHE. HAJI KHATIB KAI aliuliza:-

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ilivyo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekuwa ikiandaa kozi mbalimbali kwa Askari wa Jeshi la Polisi ili kuwajengea uwezo katika majukumu yao kiutendaji lakini pia kuwaongeza maslahi mara wanapomaliza kozi hizo:-

Je, kozi hizo zinatolewa kwa utaratibu gani na mara ngapi kwa kila Askari Polisi?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa taasisi yoyote ni uhai na msingi wa utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi na tija. Aidha, Majeshi yote duniani yamejengwa kwenye misingi ya mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jeshi la Polisi Tanzania, mtu (raia) anapojiunga ili awe Askari Polisi ni lazima aanze na mafunzo ya awali (*Basic Recruit Course*) na akihitimu ndipo anakuwa Askari (*Police Constable*). Baada ya hapo kunaweza kuwepo na kozi mbalimbali kulingana na mahitaji ya jeshi kwa nyakati mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Mafunzo ya upandishwaji vyeo hutolewa kulingana na mahitaji ya ikama na hufanyika baada ya mawasiliano na Idara Kuu ya Utumishi pamoja na upatikanaji wa bajeti ya kuwalipa mishahara na posho mpya baada ya kufuzu mafunzo. Kozi ya upandishwaji vyeo ya chini ni miezi mitatu (3) na kwa ngazi ya ukaguzi na uofisa ni miezi sita (6).

(ii) Mafunzo ya ujuzi maalumu kwa mfano Upelelezi wa Makosa ya Jinai (*CID*), *Cyber Crime Investigation, Traffic, FFU* na kadhalika, haya hutolewa na kwa askari wa vitengo mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji, changamoto na upatikaji wa fedha ili kuwezesha mafunzo husika kufanyika. Muda wa mafunzo haya vyuoni ni miezi miwili (2) hadi mitatu (3) na yanaweza kutolewa mara moja (1) hadi mara (3) kwa mwaka kwa Askari tofauti (sio kurudia waliosoma kozi hiyo hiyo).

(iii) Mafunzo ya utayari hutolewa kuwajengea uwezo Askari ili kuhimili majukumu na afya ya utendaji kazi bila ulegevu na woga. Haya huzingatia upungufu na uhitaji wa kukabili changamoto zinazojitokeza mara kwa mara. *Police General Orders(PGO)* Na.45, 86 na 90 zote zinasisitiza mafunzo katika maeneo ya kazi hata baada ya kumaliza kozi vyuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Inspekte Generali wa Jeshi la Polisi anaweza kuelekeza kufanyika mafunzo fulani kulingana na mahitaji ya Jeshi kiutendaji ili kuleta ufanisi wa kazi za Ulinzi na Usalama katika nchi.

Utaratibu Unaotumika Kupata Ubora wa Bidhaa

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA aliuliza:-

Je, ni utaratibu gani unaotumika inapotokea *TBS*haina uwezo wa kupima au kutambua ubora wa bidhaa inayozalishwa au inayotaka kuzalishwa hapa nchini?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Abdallah Ally Mtalea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) lina maabara zipatazo nane (8) kwa ajili ya upimaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo chakula, nguo, ngozi, kemikali, vifungashio, vifaa vya umeme, vifaa vya makenikali na vifaa vya ujenzi. Kati ya maabara hizo, maabara sita (6) zina Cheti cha Ithibati (*Accreditation*) ambacho kinazipa uhakika maabara hizo kutoa majibu yanayokubalika popote ulimwenguni. Uthibitishajji ubora wa bidhaa hufanywa kwa kupima bidhaa husika na kulinganisha majibu katika kiwango (*standard*) husika. Kwa kuzingatia utaratibu huo wa Ithibati (*Accreditation*), *TBS* inatambua majibu yanayotolewa na maabara zenye Cheti cha Ithibati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale inapotokea kuna bidhaa ambazo *TBS*haina uwezo wa kuzipima au kutambua ubora wa bidhaa hizo zinazozalishwa au zinazotaka kuzalishwa hapa nchini, utaratibu unaotumiwa ni kwamba *TBS* huwasiliana na maabara zenye Cheti cha Ithibati hapa nchini na kujua kama maabara hizo zina uwezo wa kupima bidhaa husika. Maabara hizo ni kama vile, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (*GCLA*) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (*TMDA*). Endapo ikibainika maabara hizo nazo hazina uwezo wa kupima bidhaa husika, *TBS*huchukua hatua zifuatazo:-

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

(i) *TBS* huwasiliana na Maabara nyingine za binafsi hapa nchini. Maabara hizo ni pamoja na ya *SGS* ambayo ina Hati ya Mashirkiano (*MoU*) na Shirika katika upimaji wa kigezo kimoja cha mafuta; na

(ii) Ikishindikana, huwasiliana na Maabara za Mashirika ya Viwango ya Kikanda kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kimataifa kwa ujumla. Msisitizo ni kwamba Maabara hizo ziwe na Cheti cha Umahiri/Ithibati (*Accreditation*).

Na. 72

Ranchi ya NARCO Mbarali Kutumika kwa Kilimo

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA aliuliza:-

(a) Ranchi ya NARCO Mbarali ilianzishwa kwa ajili ya mifugo; je, ni kwa nini eneo hilo sasa linatumika kwa kilimo?

(b) Migogoro ya wakulima na wafugaji Mbarali imekuwa ni mingi. Je, kwa nini Serikali isitoe eneo la Ranchi ya NARCO Mbarali ili litumike kwa ajili ya malisho ya mifugo?

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Ranchi ya Usangu iliyopo Wilayani Mbarali ni mionganoni mwa Ranchi ambazo Serikali ilielekeza zigawanywe katika vitalu na kukodishwa kwa wawekezaji ili kuendeleza ufugaji wa kisasa na kibiashara kwa mikataba maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huo, Ranchi hii iligawanywa katika vitalu 16 vyenye ukubwa wa kati ya hektaki 2,448.90 hadi 3,158.88 na kukodishwa kwa wawekezaji wazawa. Kwa sasa Ranchi hii ina jumla ya ng'ombe 9,885, mbuzi/kondoo 6,192, punda 56 na farasi wawili (2).

Mheshimiwa Naibu Spika, NARCO imekwishafanya tathmini na kubaini jumla ya wawekezaji katika vitalu vitano ambao wamekiuka masharti ya uwekezaji kwa kutumia

mashamba hayo kwa shughuli za kilimo. Hivyo, *NARCO* imechukua hatua za kisheria ikiwemo kutoa notisi za kuonesha nia ya kuvunja mikataba na kuwaondoa wawekezaji hao na maeneo yao yatakodishwa kwa wafugaji wengine wenye nia ya kuwekeza kwa mujibu wa sheria.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji, *NARCO* kwa sasa inaendelea na zoezi la kuweka mipaka inayoonekana katika Ranchi zake zote ikiwemo Ranchi ya Usangu na pia imeanzisha mpango wa kuwakodisha wafugaji maeneo kwa muda mfupi kwa utaratibu wa mikataba maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2019/2020 jumla ya vitalu 107 vimekodishwa kwa wafugaji katika Ranchi zake zote. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mbarali, *NARCO* imeanza zoezi la kuwabaini wafugaji ambao wapo tayari kuwekeza katika maeneo ambayo wataondolewa wawekezaji waliokiuka masharti ya mkataba. Zoezi hili linalenga kupunguza migogoro lakini pia kutoa maeneo ya malisho kwa wafugaji katika Wilaya hii.

Na. 73

Suma JKT Kutoendelea na Mradi wa Matrekta

MHE. MARTHA M. MLATA aliuliza:-

Je, ni sababu zipi zilisababisha SUMA-JKT kutoendelea na mradi wake wa matrekta?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, SUMA-JKT inaendelea na mradi wake wa matrekta kwa kununua matrekta, vipuli na zana zake na kuuza katika awamu tofauti tofauti. Katika mwaka

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

wa fedha 2018/2019 mradi uliagiza matrekta 100 na kufanikiwa kuuza matrekta 67 na unatarajia kuagiza matrekta mengine 100 na zana zake kabla ya Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na kasi ndogo ya ulipaji madeni ya matrekta, mradi sasa unaagiza na kuuza matrekta kwa fedha taslimu na kwa bei nafuu ili kumfanya mkulima aweze kumudu kununua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika linaendelea kufuatilia madeni ya matrekta na mradi unaendelea kufanya biashara ya kuagiza na kuuza matrekta.

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninayo hapa orodha ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ambao wameomba kuchangia hoja hii kwa utaratibu ule tulionao. Tutaanza na Mheshimiwa Charles Kitwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati ajiandae.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa TAMISEMI ambayo ni nzuri sana, imesheheni maeneo mengi ambayo yanahusika na TAMISEMI kwa ujumla; elimu, mapato na namna ambavyo tunaweza tukaboresha.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitajikita sana katika eneo hilo lakini kuna jambo moja ambalo ni la muhimu sana nimeliona, wenzetu wa TAMISEMI yawezekana wamelisahau na Wizara nyingine wanaweza kuwa wanalisahau lakini lina umuhimu mkubwa sana wa kuongeza mapato kwa Taifa letu, kwa nchi yetu kwa ujumla na vile vile kuimarisha ulinzi katika nchi yetu. Kitu hiki kinaitwa *NIDA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *NIDA* tunavyoiangalia, tusiiangalie kama *NIDA* ile ya kitambulisho. Naomba nizungumzie leo kwa upande wa TAMISEMI ili na Wizara nyingine ziweze kuona umuhimu wa kulihusisha hili jambo katika bajeti zao. *NIDA* ni utambulisho wa wananchi wote wanaoishi nchini. Kuna wananchi raia wana namba za *NIDA*, kuna wageni wana namba za *NIDA*, kuna wakimbizi wanaotakiwa wapewe namba za *NIDA*. Kwa kutumia namba hii, TAMISEMI wana-*play a very big role* kuweza kujua kwamba yupi ni Mtanzania na yuko wapi? Hili halijaonekana na ndiyo sababu hata katika uendeshaji wa *NIDA* kunakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutambue kwamba hospitali nyingi ziko chini ya TAMISEMI. Ukienda kijijini kuna *dispensary* wananchi wanazaliwa, kuna Vituo vya Afya wananchi wanazaliwa. Ukienda vijijini ndiko sehemu ambako TAMISEMI iko wananchi wanazikwa, wananchi wanatambuliwa kwamba huyu kweli amefariki. Sasa ukiiangalia *NIDA* kama *system* kwa ujumla, utajua nini umuhimu wa TAMISEMI kwenye *NIDA*. Tunapoandika au tunapojaza *particulars* zetu kwa ajili ya *NIDA*, tunasema mimi nakaa Kitongoji cha MaweMatatu, Kata ya Usagara, Kijiji cha...

MBUNGE FULANI: Kolomije.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni Kijiji cha Usagara. Kolomije yeye ndio anakokujua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukishakuwa umetambuliwa hivyo, hata kwenye kitambulisho chako cha

NIDA inaandikwa hivyo. Leo hii natoka Kitongoji cha Mawematatu Kijiji cha Usagara, nahamia Dodoma Chuo Kikuu, naishi huko. Kama sijalipa kodi nawe ukaenda ukabofya namba yangu ya *NIDA*, nitaonekana niko Usagara Kitongoji cha Mawematatu. Anayejua mimi nimehama Mawematatu kwenda *UDOM* ni Mwenyekiti wangu wa Kijiji aliye chini ya TAMISEMI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima sasa tutambue hili. *NIDA* ikae hapo tu kama kuhodhi *data base*, lakini *players* ni wananchi wote. Maana ukishaandikishwa leo, umeandikishwa, kinachofuatia ni mabadiliko ya jinsi unavyoishi na unavyohama na *record* za *NIDA* lazima zibadilike kulingana na wewe unavyohama au unavyoishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ni wangapi ambao wamefariki (Mungu awaweke mahali pema Peponi), lakini wanatambuliwa na *NIDA* bado wanaishi? Kwa hiyo, kadi ile inaweza ikatumika mahali popote kufanya uhalifu bila kujua, lakini kama tutashirikisha TAMISEMI kwenye maeneo ya maziko, mtu akishazikwa kuwe na utaratibu sasa; nije kwenye huo utaratibu (*system*), I am taking about a system. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri mimi ni mtaalam wa *IT*, nimejenga *system* na haya mambo nayafahamu mnavyoelewa. Tuache kuangalia kitambulisho. Kitambulisho is just anything, lakini records zinazohusu kitambulisho ndiyo tuitambue kama *NIDA data base*, ndiyo chenye thamani. Ikishakuwa records haziko sahihi, usahihi wa hicho kitambulisho changu umeisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunazungumzia watu wa *TRA* wana *TIN Number*, ukienda sijui Uhamiaji wana vitambulisho vyao mpaka sijui nini; lakini kama tutaamua kuitambua *National Identification* tutajua kuna wakimbizi wangapi wako Rusumo Kitongoji fulani hawastahili kulipa kodi? Tutajua mkimbizi gani amekwenda kufanya kazi mahali fulani na imelliingizia pato kiasi gani, kwa kutambua ile *NIDA card* yake kama atakuwa amepewa? Tutajua Kitwanga leo

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

hii ana kiasi gani cha fedha alizonazo benki kwa sababu tunamtambua kwa *NIDA* card yake.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu huwa naongea pole pole, ukiniongezea dakika mbili siyo mbaya ili nilieliezee hili vizuri na umuhimu wake.

Kwa hiyo, naomba *NIDA* na sehemu nyingine iangalie *NIDA* kama ile ya kitambulisho lakini *NIDA as a system* iwe *TRA*, iwe *TAMISEMI*, iwe mahali popote kwa sababu mtoto anapozaliwa leo, kuna hospitali. Hivi kuna sababu gani ya kusubiri mpaka baada ya miaka 18 mtoto huyo tena aanze kujaza fomu, aulizwe baba yako ni nani? Wakati leo amezaliwa, tumejata *records* zake baba yake ni nani, mama yake ni nani, ni Mtanzania, weka hizo *record* siku anafikisha miaka 18 kitambulisho chake cha *NIDA* kinatoka *automatic, pwa!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mtu amemaliza kuzikwa, ni *TAMISEMI* huko huko. Yule aliye Shehe, sijui nani...

MBUNGE FULANI: Mchungaji.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: ...Mchungaji aliyemaliza, akimaliza hapo, anasaini kile kitambulisho, huyu ni Marehemu, nimemzika, kinapelekwa. Tayari *NIDA* inakuwa *updated* kwamba tumejataza Mtanzania huyu na kitambulisho hiki hakifanyi kazi. Zote hizo zinaihusu *TAMISEMI* kwa sababu ndiko tunapokaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuipe uzito hii *NIDA* na hicho kitambulisho, tutaweza kuwatambua watu wetu, hakika ikiwezekana mtakuwa hata hamfanyi sensa. Ile fedha ya sensa iwekeni kwenye kuimarisha *NIDA*. Kwa sababu utakuwa unajua Watanzania wote walipo leo. Kwa sababu akiingia

Airpot anapewa kitambulisho cha *NIDA*, unajua amekuja kwa ajili gani na ana malengo gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, atakapazaliwa leo Mtanzania, unajua amezaliwa ni mwanamke, mwanaume, sehemu gani, ni Mtanzania au siyo Mtanzania, umeshamjua. Akifariki leo, unajua amefariki leo, ni Mtanzania au siyo Mtanzania, umeshamjua. Ukitaka kujua kwamba rafiki yangu Mheshimiwa Kamani mwezi huu amekatwa shilingi ngapi kulingana na *Pay As You Earn*, bonyeza namba yake ya *NIDA* unajua amekatwa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunahangaika *PPF*, sijui *NSSF* ya zamani mnaita watu wakajipange kuandikisha kupata *records* zao. *With all records in NIDA* huna haja ya kuwasumbua watu kwenda kujipanga, bali utajua huyu yupo, huyu hayupo, *status* yeke ni hii, mlipe, akaunti yake ni hii. Vyote vinakuwa *linked together*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *let us use NIDA; TAMISEMI take a leading role.* Acheni hao *NIDA* kama *NIDA* wahifadhi *data base* na watoe zile kadi, lakini *the system you own it. Watu wa afya, you own it. Everybody* kama Watanzania tuione hii. Huu ndiyo ukombozi wa kumjua ndugu yangu huyu hapa sijui anaitwa nani, Mnyalukolo...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mwamoto! Wewe utaitwaje Mwamoto halafu bado uendelee kuwepo hapa hapa? Kwa nini usiitwe Mwabaridi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kitwanga, dakika 15 hizo. Kwa hiyo, zimekutosha.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Aaaah!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri ameelewa kabisa hoja yako ya msingi kabisa, ameielewa vizuri.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, sijasema hata na yale mengine. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia kwenye hii bajeti ya TAMISEMI. Naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Manaibu wake na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya chini ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo machache ya *ku-comment* kwenye bajeti ya Wizara hii. La kwanza, naomba nianze na *TARURA*. Mvua zimenyesha nchi nzima, madaraja yamebomoka, barabara zimekatika kila kona, barabara za *TARURA* hazipitiki, hakuna Mbunge hata mmoja hapa atakayesema barabara za *TARURA* kwake ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuchukue hatua ili kunusuru barabara za vijijini. Tusipochukuwa hatua kwenye Bunge hili kunusuru barabara za vijijini ambazo zimekatika na siyo kwa sababu Serikali haijafanya, hapana, ni kwa sababu ya janga la mvua za mwaka huu. Mafuriko kila kona na madaraja yamesombwa, lakini bajeti ambayo *TARURA* imetengewa ni ile ile, tena pungufu kuliko ya mwaka 2019. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye ukurasa wa 63 wa Randama, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2019/2020 *TARURA* ilitengewa bajeti ya shilingi 283,788,400,000/=

kutoka kwenye Mfuko wa Barabara, lakini fedha iliyotoka ni shilingi 149,636,637,419/=. Ni fedha ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya barabara ni mbaya kweli kweli. Sasa lazima tuchukue hatua za kidharura, huko tunakoenda barabara zimekatika. Chukulia kwa mfano kwenye Jimbo langu, hali ni mbaya kweli kweli. Barabara ya kuanzia Mugumu, Kibeyo, Machochwe mpaka Nyansulula, barabara ambayo inatumiwa na watalii, imekatika haipitiki kabisa na mvua zinaendelea kunyesha. Sasa hiyo ni *sample* ya Jimbo langu. Ukienda kwenye Majimbo ya Wabunge wengine hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachoomba Wizara ya Fedha iangalie nini cha kuisaidia Wizara ya TAMISEMI kwamba *TARURA* wapate ongezeko la bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inarudishia miundombinu baada ya mvua kwisha. Tusipofanya hivyo, tunaenda kwenye uchaguzi, tutashughulikiwa na wananchi, siyo kwa sababu tumependa, ni kwa sababu ya janga ambalo hatukulitegemea. Sasa nasi tuangalie namna ya kuisaidia TAMISEMI ili ku-rescue barabara ambazo zimekatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna mgogoro wa *financing* kwenye *TARURA*, ile ya kusema asilimia 30; asilimia 70 *TANROADS*, 30 *TARURA*. Naomba kuwepo na *special fund* ambayo itaisaidia *TARURA*. Tukisema tunawanyang'anya *TANROADS* napo tutakuwa tunaharibu. Barabara ambazo zinazimamiwa na *TANROADS* ni barabara ambazo magari makubwa mazito yanapita. Kwa hiyo, tukiwapunguzia bajeti, tutaharibu, lakini tutafute *special source* ya kuisaidia *TARURA* ili iweze kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Jafo na Wizara yake. Mimi nimekuwa Mbunge Jimbo la Serengeti katika Mji Mugumu ambao ni mji wa kitalii uliokuwa hauna hata mita moja ya lami. Leo tunaongelea zaidi ya kilomita tano za lami na bado nyininge kilometra nne ambazo umetuhahidi zinaendelea kujengwa, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Waziri, kuipongeza llani ya Chama cha Mapinduzi, kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayofanya. Mimi ni Mbunge wa kwanza kupata lami Serengeti. Eeh! Haijawahи kutokea. Kwa hiyo, naomba niishukuru sana CCM, inafanya kazi kubwa hata kama hawaoni. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja nikwambie, TAMISEMI hawa wanafanya kazi sana. Huyu rafiki yangu Mheshimiwa Jafo anafanya kazi. Alikuja Serengeti, tulikuwa hatuna Hospitali ya Wilaya. Ninavyoongea, Hospitali ya Wilaya imekamilika, wametupa pesa ya kutosha na mwaka huu wametutengea shilingi bilioni moja kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya. Kwa nini nisiishukuru CCM murah? Aya! Imefanya kazi kubwa, imefanya kazi kubwa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja nikwambie. Mimi wakati naingia kuwa Mbunge, tumekuta Jimbo la Serengeti lina Shule za Sekondari 23, kipindi hiki tumeingia tumejenga Shule za Sekondari 14 na zimefunguliwa na Mheshimiwa Jafo ametusaidia, kwa nini nisiseme CCM ni nzuri? Halafu mtu aseme CCM mbaya, aya! Murah, aah! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefungua shule za msingi 30. Thelathini unadhani mchezo! Mheshimiwa Waziri tunachokuomba, kwenye ule mgao wa walimu mwaka huu, tunaomba walimu wa kutosha Serengeti, maana tumefungua shule mpya za msingi, shule mpya za Sekondari, lakini walimu hatujaongezewa. Kwa hiyo, tunaomba package.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliangalia kwenye ripoti ya *UNICEF* walikuwa wanafanya tathmini ya walimu nchi nzima. Serengeti ndio tulionekana tunavuta mkia kwa upungufu mkubwa wa walimu, *of course* nafahamu kwanini tuna upungufu mkubwa wa walimu, ni kwa sababu tumeongeza shule nydingi. Kwa hiyo imebidi tunyang'anye kutoka kwenye shule, tumepongiza punguza. Kwa hiyo, tuna upungufu, tuna *gap* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo imebidi tunyang'anye kutoka kwenye shule tumepunguza punguza, kwa hiyo, tuna upungufu tuna *gap* kubwa. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Waziri tunahitaji walimu wa kutosha wa sayansi, walimu wa kutosha wa masomo ya hati nakadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo nilitaka niseme na la mwisho, *issue ya corona virus*. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli, kuna sentesi aliongea, wapo watakaoiona watakaoikejeli, lakini aliongea kitu cha kimungu kizuri sana, kwamba *no one can stop coronavirus* isipokuwa kwa nguvu ya Mungu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwambie Taifa kama Marekani watu wanapotea 2000 kwa siku, watu mnaongea tu kwamba watu wasifanye kazi hivi hawa Watananzania wakifungiwa tu wiki moja ndani wasifanye kazi watakuwaje, tata! Si watakuufa. Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Rais Magufuli kwanza ame-*recognize* nafasi ya Mungu kwamba pasipo Mungu *no one can stop corona virus* mtu asikudanganye *hata Marekani ameshindwa sasa sisi kalagabao ni kitu gani ukisema heti unaweza uka i-control corona virus*. (Makof) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kuchukua hatua zile za kitabibu tuzichukue tunawe mikono, tuweke *mask* tuchukue hatua hizo, lakini lazima tujue ni wakati wa pekee pia wa sisi kumrudia Mungu wa sisi kumtafuta Mungu, kwa sisi kujuja ya kwamba Mungu peke yake ndiyo anaweza kutunusuru na hili janga, tena tumshukuru Mungu. Ile ngoma ingelikuwa imanzia huku mbona wote tungekufa mzee, lakini ni neema tu ya Mungu ni nehema ya Mungu niwaambie. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho naomba niongelee kitu kinaitwa *monitoring and evaluation*. Jambo hili lina tatizo kidogo kwenye nchi yetu *monitoring and*

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

evaluation kwenye fedha zinazotolewa kwenda kwenye miradi ni ndogo sana. Nikuambie Mheshimiwa Jafo Madiwani wamekuwa *paralyzed*, Madiwani hawafanyi kazi yao, Madiwani ndiyo wangekusaidia wewe fedha wanazosukuma kwenda kule wakasimamie vizuri, lakini leo Madiwani wapi wanasisika, wapi wanaseumea. Kuna kitu kinaitwa *force accountimekuwa* ni kichaka cha kutumia hela vibaya fedha zinachukuliwa kupitia manunuzi hewa yanafanyika, nani anafanya *follow up* , tuna *Internal Auditors* sasa *Internal Auditors* ambaye anategemea Mkurugenzi ndiyo ampe mafuta, Mkurugenzi ndiyo ampe posho *Internal Auditors* akiona kweli atasema? Hatasema tutegemee CAG ndiye aende abaini madudu, tutegemee mwenge ndiyo huende uone madudu, lazima tuangalie namna kuimarisha kitengo cha *Internal Auditors* katika kusimamia na kukagua miradi na fedha zinazoenda kule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Tabora, naomba nimshukukuru anaenda *site*, anaenda na *BOQ* anaenda na vitu vinavyotakiwa katika kugagua mradi, lakini wengine hawa unakuta anaenda anagaangalia hivi utagundua nini.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niku...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, muda umeisha.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana *CCM* oyee! (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Hoyeee!

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya muda ametoa mchango mzuri Mheshimiwa Chacha, lakini sasa kuna mahali amezungumza kwa namna ambayo pengine inaifanya nchi yetu iwe na jina tofauti. Kwa hiyo

maneno hayo ya sisi kalagabao yanaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete ajandae.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa hii nafasi ili na mimi niweze kuchangia kidogo. Leo nitachangai katika sura tatu, sura ya kwanza nitachangia kama Mchungaji mtarajiwa, sura ya pili nitachangia kama Mbunge na sura ya tatu nitachangia kama balozi wa watu wenye ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kusema kwamba moyo usiyo na shukrani ukausha mema yote.

WABUNGE FULANI: Amen!

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Na nasema hili kwa sababu, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo imefanyika kwenye Majimbo yetu, ndiyo maana nimeanza kumshukuru kwa hayo maneno mazito, mambo yamefanyika makubwa na hatukumpata tu kwa bahati kwa sababu tulipiga goti chini tukasema tunataka Rais wa namna gani na Rais tuliyemtaka tumempata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wale ambao watakwenda kinyume naye basi laana itakuwa juu yao.

WABUNGE FULANI: Amen!

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jafo unamtendea haki Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu yale ambayo ye ye aliкуwa anayataka umeyafanya, umepita kila Jimbo mambo yameonekana. Niseme Kilolo sisi kwa kuwa wewe ni Muislam tumeangalia kitu cha kukupa labda kama itaruhusu kwa sababu dini yenu yenu inaruhusu tukupe mke mwингine, kwa sababu ili uwe jirani na sisi mambo uliyotufanya ni makubwa tulikuwa hatuna hospitali ya wilaya, ulifika pale kwetu tumepata hospitali ya wilaya, tulikuwa hatuna kituo cha afya, leo Kidabaga kituo

kile kimeanza kufanya kazi tarehe 08 Novemba, 2019 mpaka leo wanawake waliofanyiwa operesheni na wako salama 200, operesheni za uzazi, Mungu akupe nini huo ni uinjilisti hiyo ndiyo kazi yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi wanakushukuru sana, tuna hospitali ambayo kwa kweli kila unaposema Serikali hii imejenga hospitali za nguvu inayooonekana ni ya Kilolo, na hata kwenye jarida lako umeionyesha pale kwamba ni hospitali ya mfano, kilichobaki kazi imeanza, shughuli zimeanza kufanyika na kilichobaki ni kumalizia zile milioni 500 kazi zote ziishe na ili Mheshimiwa Rais kama alivyoahidi aje afungue hospitali ile. Kwa hiyo, tunakushukuru sana wewe pamoja na wasaidizi wako, kwasababu bila wao na wewe usingweza kwenda kote Mungu akubariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikushukuru kituo cha afya Suhaa Mbuyuni ambacho Mheshimiwa Rais alianza kwenye msingi kwa kutoa shilingi milioni tano na wewe ukaongeza milioni 200 kazi inaendelea na ningombwa Mungu akujalia baada ya leo kumalizana na wewe basi upange siku uende Kilolo ukaone na walichofanya pale kwenye ile hospitali kwenye ile wodi ya wanaume wameandika wodi ya Jafo utaiona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, si mbaya nikishukuru hata miradi ya maji, kuna wenzetu kutoka America *USAID* walishindanisha baadhi ya Wilaya jinsi gani tupate miradi maji, nishukuru Mwenyezi Mungu Wilaya ya Kilolo iliongoza tukapata miradi mitano na tumeongezwa mingine mitatu. Kwa hiyo, kazi inaendelea. Pia maji pale llula, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika kazi inaendelea na tu na Inshallah Mwenyezi Mungu akibariki basi atakapokuja Mheshimiwa Rais kufungua hospitali atatusaidia kufungua pale llula.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* kazi inaendelea, Mwenyezi mungu ameleta nehema ya mvua maana yake nayo ni nehema, lakini barabara zimeharibika. Kwa hiyo, ningombwa japo siyo ni sehemu yako basi sisi Wabunge wote

tuungane kwa pamoja ili *TARURA* waweze kuongezewa fedha kwa sababu sisi wote tunatoka kwenye wilaya, barabara za *TANROAD* zimeshakuwa zimetosha zinapitika, sasa nguvu iende kwenye barabara za wilaya ambazo ziko chini ya *TARURA*. Niombe hilo liweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe nichangie kama Mbunge wa watu wenyе ulemavu. Ukiangalia sikupata bahati kwenye kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu *corona*, kwanza niseme tu hofu huu ugonjwa ukiwa na hofu unaugua haraka sana kwa sababu ukiwa na hofu unapunguza hata *immune* yako kwenye mwili wako. Kwa hiyo, uwezekano wa kuugumua ni mkubwa, kwa hiyo, tuondoe hofu tuchape kazi tufuate yale masharti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na masharti na elimu nzuri ambayo inatolewa watu wenyе ulemavu bado wamesahaulika, kwasababu kuna watu ambao hawasikii wanapataje elimu ya *corona*, wanaipataje, kuna wale watu ambao hawasikii wanaipataje elimu ya *corona*. Niombe tu kwamba kwa sababu wako wachache na wale wachache walio wengi wanapata bahati ya kwenda mashulen, sasa hivi shule zimefungwa na kwasababu zimefungwa siyo rahisi kuwakusanya kwenda kuwapa elimu ambayo unatumia alama za vidole...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwamoto balozi mwenzio nikusadie tu hawaitwi watu wasiosikia, wanaitwa viziwi...

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, viziwi.

NAIBU SPIKA: Kwa sababu hata hao wengine ambao siyo viziwi kuna watu hawasikii. (*Kicheko*)

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea.

NAIBU SPIKA: Watu hao wanaitwa viziwi, we sema tu viziwi.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea taarifa viziwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba ufanyike utaratibu, pia hata hawa ambao hawaoni ili aende kwenye kunawa yale maji inabidi ashikwe mkono sasa na wao wamekuwa wakinyanyapaliwa anayemshika mkono na anayetaka kushikwa naye anakuwa na wasiwasi. Kwa hiyo, nafikiri tungeweka utaratibu fulani, wapo wanaotambaa ni tatizo. Kwa hiyo, tuangalie jinsi tunaweza tukawasaidia wamekuwa wakilalamika wakiniandia *message* wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuangalie jinsi gani gani na hata elimu tu ukisikiliza jinsi wanavyozungumza habari ya kujikinga na *corona* hamna sehemu ambayo inagusa walemavu kwamba je walemavu wanafanya vipli. Kwa hiyo, niombe hili ni jema na kama nilivyosema ni Mchungaji mtarajiwa basi wote mtabarikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe kwamba *corona* imetuunganisha sisi wote dunia nzima, wapinzani kwa mfano mimi na Mheshimiwa Lema sasa hivi ni marafiki kwasababu kuna kitu tunataka kuleta kuna dawa tunaifanyia utafit Mheshimiwa Lema *God bless*, ikishakubali mtashangaa, lakini kilichotuunganisha ni *corona*. Kwa hiyo, na dunia nzima sasa hivi imeungana vita watu hawapigani kwa ajili ya *corona*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuendelee kuwa kitu kimoja kwa sababu *corona* haichague huyu ni CCM huyu ni Chadema huyu ni Marekani, huyu ni Mrusi anakufa. Baada ya kusema hayo nisitake kuchukua muda mrefu niwaombee Madiwani wangu wote pamoja na Wabunge wote warudi isipokuwa wale wakorofi, ahsante naunga hoja mkono. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatuiwa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mheshimiwa Wilfred

Lwakatale ajiandae. Waheshimiwa Wabunge kabla hajaanza kuchangia Mheshimiwa Matiko niwakumbushe kwenye mtandao mmesharuhusiwa kupiga kura kuna Wabunge wengi humu ndani lakini kura hazionekani zikija huku. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuendelee na zoezi la kupiga kura kwa sababu baada ya muda zoezi hilo huwa linafungwa na pia niwakumbushe kwamba siku kama ya leo mahudhurio ni kura iliyopigwa, wataalam wetu wapo humu ndani kama kuna mtu anapata changamoto yoyote, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipa furasa hii nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo ya Tanzania.

Kwanza niwashukuru wananchi watanzania wale ambao waliweza kutuchangai kututoa gerezani kwa faini ambayo huwa tumepewa na Mahakama au kutumia kifungo maana yake bila wao leo nisingekuwa kwenye Bunge hili Tukufu nikiwasemea watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia hotuba ya Waziri ukiangalia anasema kwa bajeti ambayo tuliidhinisha Bunge lako 2019/2020 ya trillioni 1.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo mpaka Februari zilikuwa zimepokelewa bilioni 494 tu kwenda kwenye maendeleo, ambao ni sawasawa na asilimia 42 mpaka Februari kwa maana *quartertatu* wamepokea bilioni 494 tu *out of* trillioni 1.16, sasa unaweza ukaona hata tukisimama hapa tunapongeza nadhani hatuitendei haki majukumu yetu, hatuwezi kuwa tunaidhinisha trillioni 1.16 inaenda bilioni 492. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhamira hii unaona kabisa kwamba hakuna dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo na nilikuwa napitia ilani ya Chama Cha Mapinduzi kuhalisia ukipitia yale ambayo mliwaadaa watanzania kwenye hii ilani na yale ambayo mnaandika kwenye hotuba ambazo mnazileta hapa Bungeni hakika hamwatendei haki watanzania. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, mlisema tutahakikisha upatikanaji kwenye huduma za afya kwa mujibu wa sera yetu na mka-*insist* kabisa kwamba kila Kata itakuwa na kituo cha afya, kila zahanati walau tutakuwa, kila kijiji au mitaa kutakuwa na zahanati, tuna vijiji zaidi ya 12000 na kitu, tuna mitaa 4000 *plus* ukiangalia kwenye hotuba ya Waziri kwa miaka hii anakiri kabisa miaka minne kwamba mmejenga zahanati 338, kipindi hiki ambacho chama cha hapa kazi tu *dedicate* tumepeata Rais ambaye ni Rais kweli, Rais wa wanyonge zahanati 338 mpaka mje mfikie hizo kila Kijiji, Vijiji 12,000 vipate na hapa hii zahanati wanajenga wananchi maboma je, mnashindwa kwenda kumalizia tu na kupeleka vifaa na Waziri ni *mate* wanguhaswa,tu lakini hapa leo kwa kweli nitasema. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia vituo vya afya mmejenga mmeandika kwenye hotuba kabisa 433 jumla 938, kwa miaka 59 ya uhuru ambao Chama Cha Mapinduzi wananchi wamewapa kukusanya kodi na kupeleka maendeleo 938 ina maana tukienda na kasi hii ya vituo 430 na kitu mtahitaji tuwape basi kama ni kasi hii ambayo mnaisifiya, miaka 50 ila kila Kata iweze kuwa na kituo cha afya, na ikizingatiwa Tanzania miundombinu ya barabara kutoka huko kwenye Kata kuja hata kwenye hiyo hospitali za Miji au za Wilaya ni mibovu sana yaani kwa Tanzania hatuthamini afya au utu wa mtanzania, tunathamini *material things*.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani ukiangalia fedha ambazo zinaenda kwenye *infrastructure* sijui ujenzi wa *Stiegler's Gorge* huko, ujenzi wa *Standard Gauge*, ujenzi yaani kwa vitu ambavyo mngeweza kufumba macho mkawekeza kwenye vitu vya muhimu ambavyo ni afya fedha ambazo zimejenga hivi vituo ambavo mmevitaja hapa siyo hata trilioni mngefumba tu mkachukua hata trilioni tatu tu, hebu tumalizane na adha ya miundombinu ya afya, tumalizane na adha ya miundombinu ya elimu ndiyo muende ku-*move* na kwingine.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko kuna...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu tu mu-observe ndiyo kwanza nimeanza vumilieni.

NAIBU SPIKA: Kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Charles Kitwanga.

TAARIFA

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Esther Matiko kwa kujua taarifa za Chama Cha Mapinduzi, nimtaarifu tu kwamba ili uwatendee haki watanzania awe anatoa taarifa anazosoma kwamba mwaka 92 tulikuwa na Kata ngapi na na tulikuwa na hospitali ngapi, tulikuwa na watanzania wa ngapi sasa hivi tunakwenda kwa wapi, sababu *we are not stationary, we are moving* na sisi tunabadilisha mpango wetu kulingana na jinsi tunavyozaliana na mabadiliko ya nchi. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Matiko unaipokea taarifa hiyo.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kuipokea taarifa ambayo haina hata tija, mwaka 92 *despite*, kama hata ulikuwa na Kata 200, tunavyozungumza leo kwenye hizo kata 200 kama mmezigawa zikafika Kata 300 au 500 *population* inaongezeka kwenye hizo Kata, *what factor have you taken to consideration.* Kwa hiyo, siwezi kupoteza muda nachozungumzia *as stand as of now*, tuna Kata 4500 *plus* mna mkakati gani kama Chama Cha Mapinduzi ambacho mmepewa ridhaa kuiongoza nchi kwa miaka 59 mmefanya nini 92 ilikuwa ni CCM hii...

WABUNGE FULANI: Weee!

MHE. ESTHER N. MATIKO: ...leo mnakuja mnaongea vitu ambavyo havina matriki, niendelee. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri anasema madawa na vifaa vya tiba maospitalini vimeongezeka kwa asilimia 92 uwongo mtupu yaani kwa sababu mnajua Bunge haliko *live wananchi wakipata fursa ya kusoma hizi na wale ambao wako kwenye, reality kule this a disaster...*

MBUNGE FULANI: Taarifa!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Muda wangu tu...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa mmesimama wawili kwenye taarifa moja Mheshimiwa Mary Nagu

TAARIFA

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante namuomba Mbunge asiseme maneno ambayo hayana *statistics* nataka niwaambie Wilaya ya Hanang' ilikuwa na Kituo cha Afya kimoja leo tayari ina Vituo vya Afya vinne atasema nini hapo? Atasema nini? kama sio Rais huyu kuwa na mkakati mzuri na kusaidiwa na Mheshimiwa Jafo na watu wote wa TAMISEMI. Asiseme kama kwake haipo kwa sababu hajakazana nataka niwaambie nchi nzima hapa wamepata mambo mengi sio tu Vituo vya Afya, pamoja na barabara pamoja na maji pamoja na madarasa, nyumba za walimu na Vyoo naomba sana tukubali mambo mazuri yanavyofanyika ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiku unapokea taarifa hiyo?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kupokea taarifa yake, *I will do respect* acha nichangie. Ninapozungumza hivyo nina *evidence* kwa mfano Tarime Vijijini kama mnafanya *qualification* ya ambavyo vimejengwa; ukichukua Tarime Vijijini vimejengwa Vituo vya Afya kwa kipindi hiki ambacho Halmashauri na CHADEMA na Mbunge wa CHADEMA vimejengwa Vituo vya Afya nane *out of each* Serikali imepeleka fedha Kituo cha Afya kimoja tu vingine ni mapato ambayo wamepeleka kwenye

Halmashauri zile ambazo walikuwa hawajafanya *before*. Wamejenga Hospitali ya Nyamwaga kwa fedha ambazo wamezi-*qualify* hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye elimu, naomba niongee atajibu wakati ana *wind up*.

T A A R I F A

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, Mheshimiwa Mwita Waitara.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Esther Matiko kwamba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi imepeleka shilingi millioni mia nne kwenya Kituo cha Afya Mtende kwenye Jimbo lake, imepeleka fedha shilingi milioni mia tano kwenye Kituo cha Afya Sirari. Shule yake ya msingi Bomani imepata milioni arobaini na sita, madarasa mawili yamejengwa. Tumepeleka fedha milioni mia sita na hamsini Jimbo la Tarime Vijijini na hakuna Vituo vya Afya kule tisa, kuna zahanati ambazo wananchi wamechangia na nimefungua Zahanati ya Kimusi, Nyamuhibigola na maeneo mengi. Mheshimiwa Mbunge ni muhimu akatoa taarifa za kweli, asilidanganye Bunge. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, sipoeki tatizo ame-*panic*. Nimeeleza vizuri sana kwamba wamepeleka Kituo cha Afya kimoja vijijini ambacho ni cha Sirari ambacho amekitaja hapo. Tarime wamesema wanajenga kila Kata, mimi nina Kata nane wameweka Kituo kimoja cha afya tena ambacho sisi tume- *supplement* kama wananchi kumalizia. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Uuuuuuuuuuu!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, sikiliza nimesema, mtajibu, msinipotezee muda. Uhalsia hotuba ina *reflect*. Kwa *style hii hatuwezi kufika popote and I am repeating this with bolded word* kama mnajali afya za Watanzania nataka Taifa lisonge mbele wekeza kwenye afya, wekeza kwenye elimu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko, subiri; Waheshimiwa Wabunge tusikilize mchango, halafu Mheshimiwa Matiko usijibizane na Wabunge zungumza na mimi itakurahisishia kumaliza mchango wako. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, Mheshimiwa Esther Matiko endelea.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, *the good thing, the bad thing is Wabunge they don't read social service most of the Wabunge hawasomi na ku-compare things wanakuwa moved on*. Tunapongeza tunapongeza *let me move on*, ukija kwenye miundombinu ya elimu, nimesema mwanzo kwamba TAMISEMI ndio kwanza Wizara ambayo ilitakiwa ipewe fedha nyingi sana kwa sababu ina *deal immediately* na maisha ya Watanzania. Leo tusipowekeza kwenye afya, tusipowekeza kwenye elimu, tusipowekeza kwenye barabara kwa TARURA ambazo hazipitiki, tumetoka kusema hapa, tumepitisha bilioni mia tatu arobaini na kitu zimeenda mia moja arobaini na sita. Sasa hivi wameleta hapa Bunge tuidhinishe bilioni mia tatu arobaini na nne za ndani mia mbili sabini na tano, lakini wanajua mvua zimenesha nyingi, barabara nyingi hazipitiki kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukisema bajeti zao hazina uhalsia na hawana nia ya kusaidia Watanzania, hatukosei. Sisi kama Taifa na kama Wabunge tunatakiwa tuishauri Serikali, iongeze fedha na tuseme *this time* angalau ziende kwa sababu tunaweza tukapitisha bilioni mia tano hapa na zisiende, wakapeleka mia mbili barabara hazipitiki, wakati kule sasa ndio kuna uzalishaji wa mazao yanayokuja huku mjini kwa walaji, lakini barabara mbovu; wakikaa wanasema Chama cha Mapinduzi kimefanya kazi kubwa, kazi kubwa wakati *ninety percent* ya Watanzania ambao

wanaishi huko hawapati chochote. Ukija kwenye elimu sasa
...

TAARIFA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hii itakuwa taarifa ya mwisho kwa Mheshimiwa Matiko. Mheshimiwa Venance.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Nataka nimkumbushe tu Mheshimiwa Mbunge wakati tunapopitisha bajeti hapa ni yeye huwa anaongoza wenzake kusema hapana na kutoka nje, iweje leo anahoji maendeleo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Matiko endelea na mchango wako.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye elimu, tunataka elimu bora kwa vijana wetu, hatutaki tu bora elimu. Leo wamesema sijui elimu bure, *Professor pale amesema ni free education*, sasa hivi wanasema ada *well and good*. Wanasema wameondoa ada wamempunguzia raia mzigo, lakini mwananchi huyu haya maboma ambayo wameyaeleza hapa, wananchi ndio wanatakiwa wapongezwe, ndio wanajenga maboma na wakati mwingine Serikali inashindwa kumalizia. Mfano hai ni kwangu, inabidi tena na sisi wananchi tuchangishane huku na huku kumalizia maboma, fedha haziji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kuna shule tumejenga kata nane tumejenga shule mpya saba kwa nguvu za wananchi. Leo Mheshimiwa Waitara anasimama hapa, kila siku anafanya ziara pale Tarime, alienda Igalaala Sekondari pale akaahidi kwamba angepeleka fedha toka Serikali, mpaka leo watoto wanakaa chini hapa wameandika madawati; Walimu wanarundikana kwenye darasa moja hata Mwalimu Mkuu amekaa hapo yaani ni aibu, halafu wanakaa wanasema elimu itakuwa sawa, Mwalimu Mkuu, *Academics*, Mwalimu wa Taaluma yaani wote

wamerundikana hata wanafunzi wakienda, Walimu wengine wote darasa hilo hilo moja na ameenda Igalala aka-*promise*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo lazima tuboreshe miundombinu ya kujifunzia na kufundishia. Madarasa yawepo ya kutosha wakiwekeza mara moja watamaliza hili tatizo, kuna Wabunge wapo humu bora hata kwangu, madarasa yao ni majengo yameezekwa na nyasi, halafu wakikaa hapa wanapongeza eti tunesonga mbele, watoto wanasoma kwenye miti, wanasoma kwenye nyasi. Vyoo vinasikitisha, watoto wanasoma 120 kwenye darasa moja, halafu wanasema *we are moving*, walimu hawatoshi wameshindwa kuajiri Walimu, halafu wanategemea Tanzania itaenda mbele, bila elimu tutakuwa mazuzu daima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kengele yangu ya kwanza hiyo. Vyoo wameandika hapa, lakini vyoo vyote wamejenga wananchi. Wameandika maabara hapa 227 kwa miaka mine, tunasema Tanzania ya Viwanda, wanajenga maabara ambazo wananchi wamejenga maboma, 227 kwa miaka minne pengine wanasema hapa wanaenda mbele kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana naweza nikaongea, tunasaidiana na wananchi wangu, mimi sio jukumu langu kujenga lakini nikiona Watanzania wa Tarime watakuwa nyuma, nimejenga madarasa pale. Nimechangia matofali, nimechangia simenti, nimechangia mabati, nimejenga madarasa kabisa kwa mfuko wangu mwenyewe *ku-support education* sasa kama Serikali inafanya nini, sio wajibu wangu mimi ule. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Hongera sana!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Kimkakati; wameandika bilioni sabini iende kwenye miradi ya kimkakati.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, Mheshimiwa Esther Matiko, Waheshimiwa Wabunge ili upewe fursa ya kuzungumza unafahamu Kanuni zinasemaje, usizungumze kabla hujapewa fursa ya kuzungumza. Mheshimiwa Esther Matiko endelea.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kuna miradi ya Kimkakati imekuwa *indicated* hapa na kwamba zilitoka bilioni sabini kwa Halmashauri 38. Halmashauri ya Mji wa Tarime tulipata huo mradi wa kimkakati ambapo ilikuwa tupewe bilioni 8.9. Tukaenda mpaka mbali wakasema fedha zinakuja, wakaenda wakabomoa soko kuu pale Tarime. Sasa hivi karibu unafika mwaka, wananchi wale wanayumba kiuchumi, ikaja ikatangazwa na Hazina mradi umefutwa. Nikamsikia na Mheshimiwa Rais anasema kuliko kuwekeza kwenye hiyo miradi ya kimkakati ni bora fedha ziende kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua toka kwa Mheshimiwa Waziri, pale Tarime tunapata fedha lini za soko la kimkakati ambalo lilikuwa limeshabomolewa vibanda ili waendeleee kujenga, maana yake hata mji wangu wa Tarime unaonekana umekuwa *shabbysasa* hivi. Kama Serikali haileti hela za mradi wa kimkakati basi wa- *compensate* wale raia ambao walivunjiwa soko lile ili wajenge vibanda vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ukisoma Ibara ya 25, 26, 27 with due respect Waziri anasema Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulifuata Katiba ya Nchi, Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na 88. Ibara ya 26 anasema CCM walishinda kwa kishindo asilimia 99.9, ameenda mbali amesema uchaguzi ulikuwa wa amani kabisa. Mheshimiwa Waziri, kwamba uchaguzi ulikuwa wa amani, kwamba raia wa Tanzania wako salama kabisa na happy na ule uchaguzi, kwamba anaenda mbali anasema unahitaji ushirikiano na Wenye viti wa Mitaa haramu. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kama hajafanya tafiti, wananchi *they are bitter than ever, ever, fanyeni tafiti muone response* ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unavyokuwa unaandika hivi vitu...

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jenister kanuni inayovunjwa.

MBUNGE FULANI: Dada yetu leo amenyanyukaa!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba nitumie Kanuni ya 64(1)(f) Mbunge anapochangia Bungeni haruhusiwi kutumia lugha ambazo ni za kuudhi, lugha mbaya zenyne mwelekeo wa matusi. Kwa kweli si sahihi leo Mbunge anaposimama hapa Bungeni halafu anawaita Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vitongoji waliochaguliwa kwamba ni haramu. (*Makofii/ kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane amepewa nafasi Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha na kwa heshima ya Bunge lako hili Tukufu sidhani kabisa kama lugha hii inakubalika ndani ya Bunge letu. Mheshimiwa Mbunge anayo nafasi ya kuchangia na *ku-express* kile anachojikisia, lakini si kuwapa majina Watanzania wenzake ambayo ni majina yenye kudhalilisha,

ni majina ambayo hayaheshimu hadhi ya watu ambao anawapa majina hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nakuomba sana ikiwezekana kwa kweli jina hili alilowapa Wenyeviti hao lifutwe ili tuweze kuendelea na mjadala wetu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kanuni zetu zinatuongoza vizuri, Mheshimiwa Jenista amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64 akitukumbusha kuhusu mambo ambayo hayaruhuswi Bungeni. Yeye ametumia Kanuni ya 64(1)(f) ambayo inakataza kutumia lugha ambayo haipendezi kwa Mbunge au kwa mtu mwingine yejote. Hayo maneno ya Wenyeviti kuitwa Wenyeviti haramu si maneno mazuri kwa sababu hawa ni viongozi ambao wapo na watakuwepo kwa miaka mitano ijayo na ndio wanaotuongoza. Sisi wote kama Wabunge na ndio watunga sheria tunafahamu kwamba wako Wabunge humu ndani na mifano tunayo ambao wamepita kwenye Majimbo yao bila kupingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo mtu kutokupigisha kura haimaanishi hajachaguliwa, lazima tuelewane vizuri haimaanishwi hajachaguliwa na ndio maana Wabunge wote humu ndani pamoja na waliopita bila kupingwa ni Wabunge halali kama Wabunge wengine wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hiyo maneno haya yaliyotumika yapo kinyume na kanuni zetu. Kwa hivyo kwa kuwa nimeombwa utaratibu uamuzi ni huo kwamba maneno hayo ya kuwaita Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji ni haramu na viongozi wote waliopatikana katika uchaguzi wa Novemba, 2019 haramu hayako sawa sawa.

*(Hapa Mhe.John Heche alizungumza bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche tafadhali. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge maneno hayo yanaondolewa

kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Mheshimiwa Esther Matiko, malizia mchango wako.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nije hapo hapo utawala bora kwenye TAMISEMI, tumeshuhudia wimbi la kuondoa Mameya wa CHADEMA kinyume na utaratibu na Sheria za nchi yetu. Tumeona ni jinsi gani Meya ya Jiji la Dar es Salaam ambaye aliondolewa kinyume na Kanuni ya 84(3), (4) na (5) ambayo inasema kama kuna tuhuma zozote zile atahitaji kujitetea, *then* kuna kura zipigwe 2/3 zikisema huyu mtu aondolewe ndio anatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Meya wa Dar es Salaam pamoja na kuwa walijaribu kufoji hata jina la mjumbe ambaye hakuwepo lakini hata kura zenyewe hazikupigwa. Leo wamepoka ofisi, wamepoka na gari na Meya ndio hivyo hajullikani Meya wa Dar es Salaam ni yupi, hivyo, ningependa Mheshimiwa Waziri ukija ku-*ind up* utuambie. Meya wa Jiji la Dar es Salaam ni nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Iringa tumeshuhudia *the same happened*, wapiga kura 14 CCM, 12 CHADEMA haijafika 2/3 wamemwondoa Meya wa Iringa. Haya mambo sio tu yanajenga chuki sio tu yanajenga chuki kwenye jamii, wanaweza wakaona leo *people just get away of this stuff*, lakini wanalipeleka Taifa kwenye hali ya hatari zaidi. *You have to mark my word*, tunaendelea ku-*accumulate a lot* kwenye moyo wetu, siku tukiamua sasa ku-*burst out* kama Taifa hamta-*resist* kitakachoenda kutokea. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Fred Atupele Mwakibete, atafuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli ajiandae.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa name niweze kuchangia kwenye hii Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kabla ya yote nipende kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye leo ametufanya tuwepo katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi napenda sana kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ya kipekee sana ambavyo ameweza kuitendea haki Wizara hii ya TAMISEMI akiwa ye ye ndio Waziri na akikasimu madaraka kwa Mheshimiwa Jafo. Napenda pia kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara hii akiwemo Manaibu Waziri wote, Katibu Mkuu *Engineer Joseph Nyamuhanga* pamoja na Manaibu Katibu Wakuu wote pamoja na *Executives* ama Wakurugenzi wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Wizara hii imefanya vizuri sana katika miaka yote hii ambayo tumekuwa hapa Bungeni. Imekuwa mfano wa Wizara pia zingine, simaanishi Wizara zingine hazijafanya vizuri lakini TAMISEMI imefanya kazi nzuri Mheshimiwa Jafo anastahiki pongezi nyingi sana pamoja na wasaidizi wake wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Wakati naingia madarakani mwaka 2015 kwenye Jimbo langu la Busokelo mfano rahisi tu, tulikuwa na Kituo kimoja cha afya, hivi ninavyozungumza tumejenga vituo nane vya afya kupitia Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na katи ya Vituo nane vya Afya vituo vitatu vimepata fedha. Tumepata fedha milioni mia tano Kituo cha Afya Isange, tumepata fedha milioni mia tano kwa Kituo kingine cha Afya Mpata na milioni mia nne Kituo cha Ntaba na vituo hivyo tayari vimeshaanza kutoa huduma na wananchi wanapata huduma pale. Kwa hiyo lazima niishukuru Serikali yangu ya Awamu ya Tano, lakini zaidi wametujengea Hospitali ya Wilaya kwa thamani ya zaidi ya bilioni moja na milioni mia tano lazima, niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi, hivi ninavyozungumza tulikuwa tuna zahanati nne, hivi sasa tunajenga zahanati 14. Hii nazungumzia Sekta ya Afya tu na ni Jimbo ambalo lipo pembeni kabisa kule. Mwanzo hatukuwa na nyumba za watumishi, lakini hivi ninavyozungumza, tuna nyumba za

watumishi 14 zenye thamani ya zaidi ya bilioni moja na milioni mia moja katika Serikali hii ya Awamu ya Tano. Pia tunajenga Jengo la Halmashauri ambalo litagharimu zaidi ya bilioni tano na tayari zaidi ya bilioni tatu zimeshatolewa na Serikali hii ya Awamu ya Tano, lazima tuipongeze Serikali kwa kazi kubwa tena iliyotukuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kwa Mheshimiwa Jafo na amekuwa ni Waziri na *role model* kwetu sisi Wabunge vijana na amekuwa akitembea huku na kule na kila mara nikimwona nafarijika kwamba unachapa kazi vizuri. Katika Vituo hivi nya Afya nina hakika kutakuwa kuna upungufu wa watumishi, kwa hiyo ni wakati muafaka sasa wa kuweka katika bajeti watumishi watakaotosheleza katika kuhudumia vituo hivyo nya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija katika Sekta ya Elimu; tumepata zaidi ya bilioni moja na milioni mia tano katika mfumo ule wa *EP4R* pamoja na kuboresha maboma. Hivi ninavyozungumza zaidi ya shule za msingi 62 pamoja na za sekondari 17 tumezikarabati kuititia Serikali hii ya Awamu ya Tano. Pongezi nydingi kwenu wote mliosimamia jambo hili na zaidi tumefanikiwa pia kujenga shule ya wasichana wenye vipawa maalum. Kwa mara ya kwanza katika Historia ya Jimbo la Busokelo ambayo Serikali imetupatia zaidi ya milioni 380 na tayari wanafunzi wameshaanza kusoma na ndio inaongoza kwa matokeo ya kidato cha pili kwa Halmashauri nzima ya Busokelo. Sasa padogo hapo lazima tuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamalizia vile vile ujenzi wa Shule ya Wavulana nayo ya wenye vipawa maalum ambapo zamani tulikuwa mtoto wa Busokelo akifaulu basi uwe na hakika atakwenda mikoa ya mbali, lakini sasa hivi watoto wakifaulu watasoma palepale Busokelo, nayo inaitwa *Busokelo Boys* na wametupatia zaidi ya milioni 198 pamoja na nguvu kazi za wananchi zaidi ya milioni 100 maana yake ni zaidi ya milioni 398 karibu milioni 400 tunaendelea kutekeleza na katika shule za msingi tunamalizia kujenga Shule ya Msingi inaitwa Kimpiyola. Zote hizi ni nguvu za Serikali ya

Awamu ya Tano kwa kusaidiana na wananchi wa Jimbo la Busokelo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule za msingi tunamalizia kujenga shule ya msingi inaitwa Kipyola. Zote hizi ni nguvu za Serikali ya Awamu ya Tano kwa kusaidiana na wananchi wa Jimbo la Busokelo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika suala zima la *TARURA*, hii ni mionganini mwa taasisi zinazofanya vizuri sana tangu zianzishwe lakini kuna changamoto kubwa sana za kibajeti. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumza hapa kwamba barabara nyingi za vijijini zimeharibika lakini lazima pia nitambue mchango wa Serikali kwa miaka hii minne. Kwanza kati ya kilomita tulizonazo kama Busokelo zaidi ya kilomita 505 ambazo zipo katika mfumo wa *DROMAS*, kilomita zisizopungua 126.85 tumepata fedha kwa miaka yote minne zaidi ya Sh.7,259,000,000 na zimetumika kujenga madaraja na makaravati yasiyopungua 13. Hili lazima tuipongeze na kuishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la msingi kwa *TARURA*, naomba kwa kuwa fedha zao wanapata asilimia 30 tu ya bajeti nzima basi ni wakati muafaka wa kuanza kuifikiria au ama kuiongezea kiwango ama *ku-balance* kidogo kutoka kwa watu wa *TANROADS* kwa sababu mazao yetu mengi yanatoka vijijini. Pia kwa kuwa Majimbo mengine ambayo yako pembeni mwa nchi hii ya Tanzania ikiwemo Jimbo la Busokelo na mengine mengi hasa maeneo yale ambayo yanapata mvua nyingi kwa mwaka mzima; kwa mfano, kuna daraja ambalo linaitwa Ngobwisya liliharibika tangu mwaka jana na Mheshimiwa Jafo ni shahidi nimshukuru kwa kuwa tarehe 28 Aprili, 2019 walikuja na Mheshimiwa Rais, daraja hili ni kiunganishi cha Kata zisizopungua tatu za Mtiba, Kisegese, Itete na kata zingine kwenda Wilaya ya Kyela ambapo ujenzi wake utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 1, tunaomba katika bajeti hii katika mpango wa miradi ya maendeleo basi muweze kutukumbuka kwa kuwa ni kiunganishi muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna barabara za Kata za Rwangwa – Kamukasi na Luteba – Makete. Barabara hii tumekuwa tukilizungumza mara nyingi hapa Bungeni kwa sababu ni barabara ambayo tayari wananchi wamejitolea wao wenyewe kwa nguvu zao, tumelima kati ya kilomita 4 mpaka 5 na ina kilomita 7, itaunganisha Jimbo la Busokelo na Jimbo la Makete. Tunaomba hizo kilomita 2 ambazo zimebaki Mheshimiwa Jafo atakapokuwa ana-*wind up* basi aone namna ya kutusaidia na pia wataalam waje kuangalia kwa sabau zinapita milimani ambako kuna miteremko mikali, *slope* ama *gradient* ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaomba kumalizia madaraja ambapo kabla sijaja huku Bungeni nilipitia kuwaona wananchi wangu na tuliona madaraja mengine yameshaanza kupata ufa na ni ya miaka mingi. Kwa mfano, kuna Daraja la Mto Rufilio na Mto Mwatisa ambalo hili litakuwa ni daraja jipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika kitengo cha TEHAMA, tumeona namna ambavyo hotuba ya Mheshimiwa Waziri imesheheni mifumo mbalimbali ya TEHAMA ndani ya nchi yetu, niwapongeze sana. Hata hivyo, kuna baadhi ya halmashauri ambazo hazijaunganishwa na Mkongo wa Taifa, bado wanatumia kitu kinaitwa *Viasatmaana* yake ni *aevery small aperture* maana yake unatumia mifumo ya *satellite*. Kwa halmashauri zilizo pembedi, kwa vyovyote vile haziwezi kukidhi matarajio ya kulipwa kwa wakati kwa sababu hii *small aperture* ama VISAT inakuwa iko *extremely slow*. Kwa hiyo, naomba tuweze kuanganishwa na Mkongo wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa kuwa TEHAMA imekuwa na matokeo mazuri sana, naomba pia Bodi

...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bodi ya Watu wa *ICT*ianzishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Wilfred Rwakatare atachangia kwa dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Ismaeli Hongoli, Mheshimiwa Sebastian Kapufi ajiandae.

MHE. WILFRED M. RWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru, ninazo dakika tano. Kwanza, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenisimamisha hapa kwa muda huu wa dakika tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Wizara hii ya TAMISEMI ambayo nimeitumikia kwa muda wa miaka 13 wakati huo ikiitia TUMITAA. Nimekuwa Afisa wa Utumishi na Utawala kwa muda wa miaka 13 lakini nikaingia kwenye siasa na nikailipa Serikali mishahara mitatu. Nikabahatika kuwa Mbunge mwaka 2000 na kuwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Pia nikatumikia katika Chama cha CUF kama Naibu Katibu Mkuu lakini nikawa ndani ya CHADEMA kama *Director* wa *Security and Intelligence*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikajaribu kugombea Serikali za Mitaa mwaka 1994 nikiwa mtumishi kuitia *CUF* nikawa Mwenyekiti wa Mtaa. Hiyo ndiyo ikanipa jeuri nikagombea Ubunge mwaka 2000, nikawa Mbunge. Niligombea na Bwana Kataraia akanishinda niliporudi mara ya pili nikamuondoa, akaja Mheshimiwa Kagasheki akaniondoa lakini na mwaka 2015 nikamwondoa. Kwa hiyo, sina deni na watu wote ambao nimewahi kugombea nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nashukuru Mungu kwamba nafuata nyayo kwamba tunatangulia katika *ku-pave the way*, nafuata nyayo za mama Mheshimiwa Tibajuka, Mheshimiwa Bulembo wanaotoka mkondo wa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kagera kwamba napumzika siasa ambazo nimezitumikia kwa miaka mingi na katika nafasi nyingi. Kwa hilo, namshukuru Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema sina deni, sina kitu chochote, waliowahi kunishinda nimewashinda na namaliza Bunge nikiwa nimewashinda. Naamini nimejenga Upinzani ulio-*credible* na watu *credible* ambao wanaweza kuendelea kuiongoza Halmashauri ya Mji wa Bukoba na tukaendelea kuonyesha mfano kwamba kuna mahali ambapo Upinzani unaweza ukafanya kazi bila migogoro na kwa kusikilizana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kabisa Madiwani wote wa Manispa ya Bukoba kutoka vyama vyote vya CCM, CHADEMA, CUF na NCCR kwani wote tumeendesha Halmashauri tukiwa tunaheshimiana chini ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Viongozi wote wa Serikali. Mimi kwa kweli namshukuru sana Mungu kuona nafikia hatua hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nalotaka kuchangia, niliwhai kumsikia mdogo wangu Dkt. Bashiru anasema kabisa kwamba nchi hii kitu kinachokosekana ni Upinzani *credible*. Mimi naamini Upinzani *credible* unategemea na mpanga mipango naye awe *credible*, kama hayuko *credible* Upinzani hauwezi kuwa *credible*. Mambo ambayo yamezungumzwa hapa na wachangiaji wengine akiwemo Mheshimiwa Matiko, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani alielezea na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wameelezea, Mheshimiwa Jafo anapaswa kupima uchaguzi unaosimamiwa na Wizara yako ni *credible*? Kama hauwezi kuwa *credible* hata Upinzani hauwezi kuwa *credible* kwa sababu mtengeneza mipango hayuko *credible*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawasikitikia Chama cha Mapinduzi kwamba mmepata fursa ya kuiongoza mabadiliko ya vyama vingi, mwanzoni nilifikiri kuwepo Mfumo wa Vyama Vingi kama alivyotarajia Mwalimu Nyerere ni kupambanisha fikra na akili ili nchi ipange mipango mizuri tuweze kufika mahali pazuri lakini imekwenda vice versa.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Tumeona nchi ambazo zimefaidika na Mfumo wa Vyama Vingi mfano Uingereza, Marekani na Ujerumanu wana Upinzani na mfumo amba ni *credible* na tunaona faida inayopatikana kwa sababu keki inatengenezwa inakuwa kubwa na wakigawana ile keki kwa kuwa ni kubwa inafika kila mahali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa mfumo ambao tumeuona kwenye Chaguzi za Serikali za Mitaa ambapo tulikuwa na utaratibu ambao siyo *credible* matokeo yake tunakuwa na viongozi ambao kimsingi hawakubaliki kwa wananchi na matokeo yake kila siku akiwaita wananchi ili wapange mipango ya maendeleo hawaendi kwa sababu wale viongozi waliochaguliwa hawakubaliki. Nashukuru kuna baadhi wameanza kuona mambo hayaendi wameanza kuijdhuru kwa kuandika barua za kuijuzuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nigosie sala la *Corona*. Naamini Wizara hii inahusika sana. Tumeona nchi za wenzetu Uganda na Kenya walipochukua hatua ya *lock downwamehakikisha* wanaweka mipango ya kuwagawia watu chakula. Mheshimiwa Dkt. Mpango alipokuwa anaelezea hapa sikusikia anazungumzia kitu kama hicho. Sasa kama tutafikia hatua hii, unajua njaa haina baunsa, Watanzania hawa mkiwafungia ndani na navyowaona walivyo Mheshimiwa Jafo watu watanunua silaha kama ambavyo Calfonia silaha zote zimenunuliwa zimekwisha kwa sababu kila mmoja anajichunga asiabiwe chakula chake na mtu mwingine. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Mheshimiwa Lwakatare, nasi tukutakie kila la kheri katika maisha yako mapya utakayoanza, tukiamini hutachukua fomu maana kuna watu wanaaga halafu wanashahau tena mambo yanakuwa magumu kidogo, tunakutakia kila la kheri.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli atafuatiwa na

Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Salome Waycliffe Makamba ajiandae.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kushukuru kwa kupewa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na nikaweza kusimama mahali hapa siku hii ya leo. Nasema ahsante sana kwa Mwenyezi Mungu aliye juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa namna alivyofanya kazi katika miaka yote hii mitano. Tumeona maendeleo makubwa yakinoteka nchini, Watanzania wanasema kwamba wanamwombea tu afya njema ili waweze kumpitisha katika awamu ya pili aweze kukamilisha mirdi yake mingi mikubwa ambayo inafanyika katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana ndugu yangu Mheshimiwa Jafo kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara hii. Ni kweli amekuwa mchapakazi mzuri na ameweza kuimudu vizuri Wizara hii ya TAMISEMI, nampongeza sana. Pia nawapongeza Naibu Mawaziri wote wawili; ndugu yangu Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Waitara kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya za kumsaidia Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Rais kwa ujumla. Nawaombea Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki muendelee kuwa na afya na njema muweze kuifikisha Tanzania pale Watanzania ambapo wanahitaji. Pia niwapongeze watendaji wote wa TAMISEMI kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Wakuu na watendaji wengine wote, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana, tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia upande wa afya. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri imeeleza vizuri sana hasa upande wa ujenzi wa hospitali hizi 67 kwenye halmshauri mbalimbali. Naipongeza sana Serikali kwa mpango huu wa

ujenzi wa hizi hospitali kwenye hizi halmashauri kwa sababu kulikuwa na changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi pia katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Njombe nayo imebahatika kupata Hospitali ya Wilaya. Naipongeza Serikali na Mheshimiwa Rais wametupatia shilingi bilioni 1.5, tumeweza kujenga majengo yote saba (7) na yamekamilika kwa kiwango kizuri sana, tunakwamishwa na vifaa tu vichache. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sijaelewa vizuri, nimeona katika hizi hospitali zote 67 zimepewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu na pia wamepata fedha kwa ajili ya vifaa. Mko wetu wa Njombe halmashauri tatu zimepata hospitali, Halmashauri ya Wanging'ombe, Halmashauri ya Makambako na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Hata hivyo, ukiangalia ule ukurasa wa 314, kiambatanisho namba 10 hazioneshi fedha zinazokuja kwa ajili ya kuongezea zile wodi tatu pia kwa ajili ya vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda pengine mnaweza kuwa mmekosea basi nitamwomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama niweze kupata ufanuzi kwa sabau Halmashauri yangu ya Njombe *DC* hakuna fedha kwa ajili ya wodi na vifaa lakini halmashauri nyingine zote zimepata. Kwa hiyo, naomba ufanuzi kimetokea nini au labda kuna jambo limechanganywa pale. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atakaposimama aweze kutoa ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye upande wa vituo vya afya, naishukuru sana Serikali sisi tuna vituo vya afya vitano (5). Bahati mbaya kwa muda mrefu hatukupata fedha kwa ajili ya kujenga wodi na mambo mengine, zile shilingi milioni, 300, 400, 500 hatukupata lakini awamu hii tumepata angalau shilingi milioni 200 na tayari zimeshafika tumeshaanza shughuli za ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri yetu ya Wilaya ya Njombe haikupata fedha hizi, niombe awamu hii angalau hivi vituo vya afya vinne vilivyobakia viweze

kupata fedha. Kuna Kituo cha Afya cha muda mrefu sana cha Lupembe pale kili jengwa mwaka 1985 na tumejenga kwa nguvu zetu sisi na kupitia fedha za ndani za halmashauri tumeweza kujenga *theater*, hivi ninavyoongea wananchi wanapata huduma ya *theater* pale lakini bado mindombinu mingine hajajengwa pamoja na kwamba sisi wenyewe tumejenga wodi moja ya kina mama kupitia mapato ya ndani na michango ya wananchi na mimi Mbunge. Kwa hiyo, niombe sasa Serikali itusaidie tuweze kupata majengo mingine ili huduma pale iweze kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye vituo vya afya vingine kama Kituo cha Afya cha Sovi hakijapata fedha. Naomba nacho kiweze kupewa fedha ili tuweze kuboresha huduma pale kwenye Kituo cha Afya cha Sovi na vingine viliviyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Kituo cha Afya cha lkuna sisi wenyewe tumejenga *OPD* kupitia mapato ya ndani. Tuombe Serikali itusaidie tuweze kupata wodi ili huduma kwa ajili ya wananchi wetu iweze kuboreshwa kwa maana ya huduma ya afya. Naendelea kuipongeza sana Serikali kwa namna mnavyofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye upande wa elimu, nipongeze sana Serikali imeendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kukamilisha maboma na sisi tumepata fedha nyingi. Upande wa maboma kuna shule zetu tatu za *A-level*: Shule ya Sekondari Lupembe ina kidato cha kwanza mpaka cha sita; Shule ya Sekondari Manyunyu; na Shule ya Sekondari Itipingo. Tunashukuru tumepata fedha kwa ajili ya kujenga bweni shilingi milioni 150 kwenye Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Manyunyu bado sasa kwenye Shule ile ya Lupembe nayo tuweze kupata fedha kwa ajili ya mabweni, watoto pale wa *A-level*/na *O-level*/wanapata shida kidogo. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri tupate fedha hizo kwenye Shule ya Lupembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Shule ya Itipingo ina wanafunzi wengi sana sasa hivi wa kidato cha tano

mabweni hayatoshi, nayo iweze kupelekewa fedha. Wananchi kwa tukishirikiana na wadau mbalimbali tumeweza kujenga bweni moja la wasichana. Sasa hivi tunaendelea kukamilisha, tunafanya *fittings* za milango na madirisha basi Serikali na yenyewe itoe fedha tuweze kuongeza bweni la wavulana, madarasa na mahitaji mengine kwa maana ya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwenye upande wa *TARURA*, inajitahidi sana kwani wanatoa fedha nydingi na wataalam wanafanya kazi nzuri sana. Tatizo kubwa kama walivyoeleza Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni fedha kwa maana kwamba fedha wanazopewa *TARURA* hazitoshi. Niombe Serikali ifanye kila linalowezekana iwaongezee fedha *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* inashughullikia barabara hizi za wananchi ambazo upande wa vijijini wanategemea kusafirisha mazao yao ili yaweze kufikia soko kwa kupitia hizi barabara. Barabara zinapokuwa mbaya, haziwezi kupitika wananchi wanapoteza thamani ya mazao yao, kwa hiyo ubora wa bidhaa wanazozalisha unafikia soko ukiwa umepungua.

Kwa hiyo, ili tuweze kuinua uchumi wa nchi na pia wananchi waweze kupata faida kutokana na mazao yao wanayozalisha vijijini ni lazima *TARURA* iweze kuongezewa fedha ili barabara zote hizi za vijijini ziweze kupitisha mazao na mazao yao yaweze kupanda thamani. Bila kutengeneza hizi barabara ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene ajiandae.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu Katavi na kwa maana ya wale wote ambao wengine ni watani zangu tuna kitu kinaitwa '*Nsinde*'. *Nsinde* ni shamba ambalo umelilima kwa mara ya kwanza. Sasa kwa wale ambao ni wakulima wanafahamu, ukililima shamba kwa mara ya kwanza linaweza likakupa mazao lakini ukirudia kulilima kwa mara ya pili linakupa mazao mengi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini nimeutoa mfano huu? Mheshimiwa Rais wetu, Waziri wangu hapo kama kwa mara ya kwanza tu kila mmoja anayesimama anaongelea mafanikio vipi wakirudia mara ya pili? Tafsiri yangu ni hiyo hiyo. Watu wamesha-*practice* hilo, shamba umelilima mara ya kwanza ukirudia mara ya pili linakupa mazao ya kutosha. Kwa hiyo, tusikosee turudia mara ya pili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakin katika hilo niendelee kusema jambo lingine; Mheshimiwa Jafo jamani Waziri huyu ni mtu rahimu. Nikilisema hilo ninaanisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kule Katavi katika kuhangaikia masuala mbalimbali; vituo vyatya afya, shule za sekondari baba wa watu huyu inafika usiku yeye ndiye anayekupigia simu, anakuuliza Mbunge wangu fedha za maeneo fulani umepata? Namna pekee ya kumlipa mzee huyu ni kusema hadharani kwamba huyu ni mtu rahimu, ndiyo namba pekee ya kumlipa huyu baba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema hayo kwa maana ya utekelezaji wa miradi mbalimbali. Kule kwangu kuna zaidi ya Sh.18,438,060,000, hizi zote zimekwenda kwenye miradi mbalimbali ukizingatia masuala ya EP4R, EQUIP-T, TEA na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nafahamu kuna baadhi ya wenzangu hapa Wabunge walioweza kufika Mpanda - Katavi. Ukienda ukaikuta stendi nzuri, wale waliokuja miaka mitano nyuma, leo wakifika Mpanda, wanajiuliza nimefika Mpanda kweli? Ni kwa ajili ya stendi nzuri. Hayo ni matokeo ya fedha hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ukweli utasimama daima. Nikilisema hilo namaanisha. Leo kwa mimi ambaye nikio Katavi ukizunguka mjini pale, kuna barabara nzuri za lami na tunakwenda kufunga taa. Ni matokeo ya fedha hizi. Watu wengine wanajiuliza, hivi kweli nimefika sehemu ambayo wengine walizoea kupaita pembezoni! Kwa ajili ya maendeleo haya, wala siyo pembezoni tena. Yanabaki kuwa ni maeneo ya mpakani na wala siyo pembezoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo sijagusia masuala ya sekondari mbalimbali kwa maana ya fedha taslimu tulizopewa; ujenzi wa Mabweni; na ukarabati wa miundombinu mbalimbali. Yote hayo ni kazi ya fedha hizi ambazo Serikali imetuletea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua palipo na mafanikio, changamoto ni jambo la kawaida. Kwa hiyo, kwa mafanikio haya, ni kweli yamezalisha uhaba wa watumishi. Nami kwenye eneo hilo la uhaba wa watumishi, Mheshimiwa Jafo kwa sababu wewe ni mtu rahimu, nimeshatangulia kusema hapo mwanzo, upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali takribani 135 wawe ni afya, wawe ni walimu tulikuwa tunaomba hilo nalo liendelee kufanyiwa kazi sambamba na upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijenga, umepunguza lakini unaweza usimalize. Kwa hiyo, najua pia tuna upungufu wa vyumba vyaya madarasa kama 676. Hii yote niendelee kusema; na ustaaarabu unanituma kwamba ukisema ahsante ni namna ya kuomba tena. Kwa hiyo, hapo Mheshimiwa Jafo na kwa kuititia hapo hapo niendelee kulisema hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi hii ambayo sasa hivi tumeendelea kuizungumzia na iko hapa, wanasema miradi ya *tactic*. Kuna barabara ya Misunkumilo – Kakese - Mwamkuru tumekusudiwa kutengewa shilingi bilioni 30. Kuna ujenzi wa soko la kisasa eneo la Kazima shilingi bilioni 6.6, ujenzi wa dampo la taka shilingi bilioni nane; kuna ukarabati wa maghala, shilingi bilioni nane. Nilichokuwa naomba fedha hizi zote zikifika huko na kwa sababu miradi hii ni miradi ya kimkakati, tutaendelea kuiona tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla muda haujaainishia, najua kuna suala moja na nilikuwa naomba hapa kwa maana ya zahanati, tunaonyeshwa kwamba kuna Zahanati moja na Mheshimiwa utanisaidia, inasomeka Mpanda *Town council*; siyo Mpanda *Town council*; ni Mpanda *Municipal Council*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili nalo mliangalie. Tunaonekana tumetengewa milioni 200. Hilo nilikuwa naomba uliangalie vizuri; je, tunakusudia? Hili niliwahi kuongea na wewe Mheshimiwa. Kwa hiyo, kama kulikuwa na sintofahamu, nilikuwa naomba sana hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitimisha kwa suala la *Corona*. Najua changamoto ya *Corona* ni kubwa na kama walivyotangulia kusema watu wengine, mara nyine kwa kujenga hofu, tatizo linazidi kuwa kubwa na wataalam wanasema ikiwezekana tupunguze zile taarifa zinazoendelea kuturudisha huko, tatizo linakuwa kubwa zaidi. Nilichokuwa naomba ni kumsaidia Rais wetu. Lazima kwanza turudi kwenye kuheshimu maelekezo yote tunayopewa na watu wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, yawezekana kabisa tusifanye kwa *style* ya Ulaya na kwingineko. Najua kwa maana ya Afrika na kwa maana ya uchumi wetu mzee ambaao unaitwa ni uchumi wa kijungujiko (*Hand to mouth sort of economy*) itabidi tutengeneze mazingira ya kuhakikisha tunafanya je katika hili bila kuathiri mambo mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene na Mheshimiwa Godbless Lema ajiandae.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye Wizara hii muhimu sana ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kuniamini na kunateua kuwa Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria, nami namwahidi kwamba sitamwangusha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nasoma taarifa mbalimbali ambazo Serikali imezileta Bungeni, nimeona kwamba Mkoa wa Shinyanga ni Mkoa wa tano katika kuchangia kwenye pato la Taifa. Taarifa hii imenifikirisha sana. Imenifikirisha nikaanza kufikiria wananchi wangu wa Mkoa wa Shinyanga na juhudini zote katika kuhakikisha tunaleta mapato kwenye Serikali wamenufaika vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya *interest* ya muda, nilijaribu kuptitia eneo moja tu la afya kwenye suala la afya katika Mkoa wa Shinyanga hususan Jimbo la Shinyanga Mjini. Sera ya Afya ya Tanzania inataka angalau kwenye kila Kata kuwe kuna kituo kimoja cha afya na angalau kwenye kila Kijiji au Mtaa kuwe na Zahanati. Sasa Jimbo la Shinyanga Mjini kuna Kituo kimoja tu cha afya ambacho kilijengwa enzi za JK. kimoja tu! Jimbo hili lenye Kata 17 lina Mitaa 55 na Vijiji kama 11 hivi. Hili Jimbo lina Zahanati 11 tu. Yaani kuna upungufu za zahanati zaidi ya asilimia 90 kwenye Jimbo la Shinyanga Mjini. Halafu leo anasimama Mbunge na kupongeza kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawasaidia Watanzania, inawajali Watanzania wanyonge kwa kuapelekeea Vituo vya Afya. Vipi Mheshimiwa Mwenyekiti? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo hili la Shinyanga, kutoka kwenye Kituo cha Afya ambacho kipo katika Kata ya Kambarage, mtu akipewa *referral* kutoka kwenye Zahanati tuseme iko Chamaguha, ni zaidi ya kilometra tano mpaka nane. Huyo ni mama mjamzito aliye kuwa anajifungua akashindwa kujifungua kwa kawaida, labda anatakiwa afanyiwe *operation*, itabidi asafiri kilometra karibu nane kutafuta Kituo cha Afya kimoja ambacho ndiyo kinategemewa na Kata zote 17 ili aweze kujifungua salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema ipo kazi kubwa inatakiwa ifanywe na Serikali, badala ya kupiga kelele na maneno mengi, hii ndiyo kazi, tunataka Serikali izibe *gap* la huduma ya afya katika jamii ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaongea habari ya *Corona*. Hili ni janga la Kitaifa. Nilikuwa naangalia kuna kibonzo kimoja cha Masoud Kipanya anauliza, "hivi hii *Corona* tunayo isema hapa ndiyo ile iliyoko kule nje?" Akaambiwa, "ndiyo". Akasema "mbona kama tunafanya mizaha?"

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa tuna zahanati 11 ndani ya Jimbo la Shinyanga Mjini ambalo lina Vijiji 17, lina Mita 55, tuna zahanati 11, unawezaje kumweleza mwanakijiji huyu ambaye leo yuko *exposed* kwenye *risk* ya *Corona* atawenza kupata huduma kwa wakati atakapofikwa na janga hili? Unawezaje kumweleza? Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijaliona hili bado. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa *data*, tunawaeleza kwamba wako wanawake vijijini wanapata taabu, ambapo ninyi Serikali ya Chama cha Mapinduzi mmewafanya mtaji, tena mnaona wale kwa sabbau hawajui na hivi ndiyo mmezima Bunge, hawaelewi kinachoendelea, mnapiga *propaganda* hawa akina mama wanateseka kijijini na watoto wetu wanateseka kijijini kwa sababu hawawezi kupata huduma ya afya iliyokamilika kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani Mheshimiwa Waziri ajifikirie kuhusu hili. hatuwezi kuendelea kuwahadaa Watanzania. Afya ni jambo la msingi, elimu ni jambo la msingi; ni lazima Serikali itoke kwa Watanzania ikawaeleze, ni kwa nini mnakwenda kinyume na Sera ya Afya? Mara nydingi tunaongea kuhusu ndege humu ndani. Utaniambia kwamba ndege mh! Yaani ndege ni za muhimu kuliko Kituo cha Afya? Yaani naomba kujua, *flying over* ya Dar es Salaam ni ya muhimu kuliko Kituo cha Afya? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili lina Wabunge makini sana na kila siku wanatoa ushauri kwa Serikali, kitu gani ni cha kipaumbele kwa wananchi? Maji safi na salama ni kipaumbele kwa wananchi; elimu ni kipaumbele kwa wananchi; afya ni kipaumbele kwa wananchi. Hivi hii Serikali inashauriwa na nani? Ni nani anayeishauri Serikali kupanga vipaumbele vyake kama siyo Bunge hili Tukufu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani wataalam watafiti, wataalam wa *monitoring and evaluation* waje wafanye utafiti kuona *effectiveness* ya Bunge lako katika yale mambo ambayo Wabunge tunaishauri Serikali, ni kwa kiwango gani wametekeleza?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo ya kuondoa vyanzo vya mapato katika Halmashauri zetu; Halmashauri ya Shinyanga Mjini wameleta kituko kimoja kikubwa sana. Katika Halmashauri ile chini ya Mkurugenzi wamewashauri wananchi waunde vikundi ambapo vikundi vile vitaenda kufanya kazi ya kuchenjua makinikia ya almasi ambayo yanatoka katika mgodi wa Mwadui. Ukitizama kwa haraka, unaweza kudhani wale watu wanasakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuunda kikundi kimoja kinatumia kuanzia shilingi 50,000/= mpaka shilingi 150,000/=. Vimeundwa vikundi zaidi ya 1,000 katika Manispaa ya Shinyanga. Vikundi vile vinakwenda katika kuchenjua mchanga wa dhahabu, wakifika kule, yaani tangu wameanza leo ni zaidi ya miezi sita hakuna mtu aliyepeata almasi hata yenye *size* ya sukari, hakuna mtu aliyepeata. Hao

wanashauriwa na wataalam wa Serikali, watu ambao wanalipwa mshahara kwa kodi ya Watanzania, lakini leo Serikali imejipatia mapato kuititia kuunda vikundi na zaidi kuvitumia vikundi hivi kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa wanayopata Watanzania wale, ili uweze kuchenjua makinikia ya almasi ni lazima ulipe watu, ni lazima ununue maji, ni lazima kikundi kikae pale kuanzia asubuhi mpaka jioni, wale watu wanachomwa na jua, wanakaa kuchenjua mchanga ambao mategemeo ya kupata mali hayapo. Nini uwajibikaji wa Halmashauri kwenye hili? Nini uwajibikaji wao? Tusiwatumiie Watanzania kwa kuwazungusha kama midoli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mwaka wa uchaguzi, nami nilisema; siku vikundi hivi vinaundwa nilisema mnakwenda kutumika kisiasa. Hakuna kitu cha namna hiyo, kwa sababu mwisho wa siku utaundaje vikundi 1,000 ili viende vikachenjue makinikia? Yaani kikundi kimoja kinaingia kwenye eneo la hiyo sehemu ya kuchenjua kwa siku moja; yaani mpaka sasa hivi hawajafika hata kikundi cha 50. Sasa mpaka vikundi 1,000...

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba kuna taarifa. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Salome Makamba, Mbunge wa Viti Maalum; ni kwamba wachimbaji wadogo wenyewe wengi waliomba wapewe makinikia kwa ajili ya kuchakata kuweza kupata almasi katika mgodi wa Mwadui. Pia katika eneo la Mwadui, makinikia hayo yalikuwa ndani ya mgodi wa Mwadui na kulikuwa kuna matukio mengi sana ya watu ambao wanajulikana kwa jina maarufu la Wahabeshi,

walikuwa wanakatiza kuingia katika mgodi wa Mwadui kwa njia ambazo siyo rasmi na matukio hayo yalikuwa yanashirikisha watu ambao walikuwa wanakwenda kuchukua makinikia hayo na kuyatoa nje kwa maana ya kuyaiba ili waje wachakate kupata almasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri tuliwaomba Uongozi wa Mgodi huo wayatoe makinikia hayo mle ndani kuwapa wananchi waweze kuchakata ili kama kuna chochote basi waweze kujipatia kwa nia njema kabisa ya kuwasaidia wachimbaji na kuondoa matukio ya watu kukatiza kuingia ndani ya mgodi kwenda kuiba; na wengine walikuwa wanaweza kupigwa risasi na wakapoteza maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa nia njema imeamua kuwaomba mgodi wa Mwadui na wao wakatoa ushirikiano kwa kutupa makinikia hayo tuweze kuwasaidia wananchi wa Shinyanga nao waweze kuyachakata wajipatie chochote. Wema huo leo naona Mheshimiwa Mbunge anaona kama vile tumefanya kisa ambacho ni cha kuweza kuwapaka matope wananchi, kisa ambacho siyo kizuri na kuwapotosha wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge aipokee hiyo taarifa kwamba tulifanya hivyo kwa nia njema kabisa kama Serikali. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshauri Mheshimiwa Nyongo anisikilize halafu achukue ushauri wangu akaufanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa msingi mmoja; timu iliyohusika kuwashauri wananchi wa Mkoa wa Shinyanga watengeneze vikundi ni timu ya Serikali. Timu inayohusika kuutoa huo mchanga wa makinikia kwenye mgodi Serikali imo.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ambalo la vikundi vyakina mama na vijana wanaofanya kazi ya uchenjuaji wa makinikia, Serikali inasimamia, yaani watu wanaamka kuanzia asubuhi, wanachukua pesa zao kwenda kununua maji, wanachukue pesa zao wanakwenda kuchenjua makinikia, wanatoka hawapati hata senti tano.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, kuna taarifa nyine. Mheshimiwa Dotto Biteko.

TAARIFA

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimpe taarifa kwamba katika zoezi la kutoa hayo anayoyaita makinikia kutoka kwenye mgodi wa *WDL*, wachimbaji wadogo wenyewe kupitia Chama chao wametafuta mkandarasi wenyewe, hakuna mahali Serikali inahusika, lakini hata anavyosema kwamba wanafanya kazi hawajapata hata kimoja; mimi nina *record* hapa nitamsaidia wangapi wamepata almasi ya kiasi gani. Kwa hiyo, tuzungumze kwa vitu ambavyo ni *fact*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kupata hiyo *record* anayoisema Mheshimiwa Waziri. Ningependa tuiione hiyo *record*, kwa sababu mimi ni Mwakilishi wa Mkoa wa Shinyanga na taarifa ya hivyo vikundi viko ndani ya eneo la Shinyanga na ninakuhalikishia ndani ya Bunge hili, kama kuna...

Mheshimiwa Naibu Spika, tena ngoja niseme hivi; almasi ambayo anasema Mheshimiwa Waziri watu wanaipata, yaani hiyo almasi anayoisema haijafika hata ukubwa wa sukari. Tena juzi kuna almasi ambayo wanasesma ilipatikana yenye ukubwa wa angalau wa karanga, almasi ile wananchi waliambiwa ile almasi ni chupa. Unanielewa! Waliambiwa almasi ile ni chupa na...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, tusaidie vizuri, kwa sababu hao wananchi kwa namna unavyotaja idadi ni kubwa sana, halafu kama wao bado wanaendelea kwenda kuchenjua wakati hakuna kinachopatikana, siyo kwamba hao wananchi yaani wanatakiwa kushauriwa labda na Mheshimiwa Mbunge ili wasifanye hilo zoezi, si maana yake halizalishi kitu chochote! Maana kama wanaendelea kwenda na hawapati kitu chochote, nadhani kuna shida hapo.

Mheshimiwa Salome Makamba, endelea na mchango wako.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, vikundi ambavyo vimesajiliwa na Serikali, narudia; kikundi kimoja kinalipa kwenye Serikali shilingi 11,000/= kusajiliwa; ghamama za Katiba na nini, kikundi kimoja kinagharamika kuanzia shilingi 50,000/= mpaka shilingi 100,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikundi vyote mpaka sasa hivi havipungui vikundi 1,000; na kikundi kimoja kinaingia siku moja. Kikundi kimoja siku moja. Mpaka tunaongea sasa hivi havijafika hata vikundi 200, wanaendelea kuingia kila siku na wanaendelea kwenda kutafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Serikali ambayo imeajiriwa ina wataalam, wanalipwa mshahara kwa kodi za Watanzania. Hilo unalolisema wewe hawalioni. Wanachojali, wamepata *own source*, mnaita *own source*, wamepata pesa kwa ajili ya Halmashauri kuititia usajili wa vikundi. Hapa hatuungeleo suala la Wizara ya Madini. Naongelea athari ya...

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba kuna taarifa nydingine. Mheshimiwa Bulembo.

TAARIFA

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie mdogo wangu kwamba uchimbaji wa madini na upataji wa madini una *style* nydingi. Siyo lazima ukichenjua upate, kwa sababu haya ni madini. Kuna watu wanafanya kazi kwenye madini miaka 10 hawajawahi kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa sababu Mheshimiwa Waziri alishamwambia atampa taarifa, ajenda hiyo angeiachia karibu ili wapeane taarifa aweze kujua; lakini ukienda kuingilia undani wa madini ya kuchenjua, wapo watu wanapata upara hawajawahi kupata, lakini kila siku yupo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Watanzania wanaona kwamba ndiyo ushauri wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwamba utafanya mpaka utapata upara na Serikali ipo na wataalamu wapo na hutakaa upate. Kwa hiyo, wanajua kwamba watu hawa wataenda kutafuta makinikia miaka karne na karne na Serikali ipo na wataalamu wapo na watapata upara na hawatakaa wapate. Haya ndiyo maelezo ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi na mimi nachukua ushauri huo ni vizuri maana na wao wamesikia watapata upara hawatakaa wapate Serikali imepata *own source* kuititia uundwaji wa vikundi imepata mapatao wahajali, hawana shida na maslai ya watanzania mimi nimepokea huo ushauri. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Dotto Biteko.

T A A R I F A

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, sababu suala la kusema wachimbaji hawapati limekuwa likijirudia na kwa sababu Mheshimiwa Salome alikuwa ameomba fursa ya kumpatia hizo taarifa na ili tutende haki kwa Watanzania wanaotutazama naomba nimpe taarifa ndogo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 6 mwezi 4 kwenye makiniikia ya *WDL* wachimbaji walipata...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa kuhusu utaratibu.

MBUNGE FULANI: Pokea taarifa kwanza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dotto Biteko, kanuni inayovunjwa Mheshimiwa Salome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anayo nafasi ya kuleta hoja...

NAIBU SPIKA: Kanuni inayovunjwa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, unanipa muda niifungue.

NAIBU SPIKA: Ukihasimama maana yake unayo tayari hiyo kanuni wewe taja kanuni inayovunjwa halafu upewe nafasi ya kueleza utaratibu unavunjwa vipi.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa nakusomea dakika moja.

NAIBU SPIKA: Wakati unaitafuta hiyo kanuni nakuruhusu ukae utasimama. Mheshimiwa Dotto Biteko.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tarehe 6 mwezi wa 4 wachimbaji hao walipata vipande 86 vya almasi, tarehe 25 mwezi wa 3 wachimbaji hao walipata vipande vya almasi mia tisa kumi na sita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo tunataka tuweke kwenye *records*sasa sahihi, Serikali kazi yake ni kusikiliza kilio cha wachimbaji wadogo na kuwasaidia. Eneo hili la almasi la mwadui, lilikuwa ni eneo ambalo makinikia yake yapo miaka mingi na walikuwa wanakwenda huko kwa wizi na wanavunjika miguu na tunayo matukio mengi ya watu kuwekwa ndani sisi Serikali tukaamua kuzungumza na mgodi wayatoe nje chini ya usimamizi wao wenyewe kupitia chama cha wachimbaji wadogo na Serikali ni *regulator*tu wa mfumo mkandarasi wametafuta wenyewe, mgawanyo wa hisa wametafuta wenyewe, vikundi wametafuta wenyewe na mfumo wote ulioko hapo unasimamiwa na SHIREMA na wala siyo Wizara ya Madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kazi yetu ni kufuatilia mrabaha na malipo ya Serikali hilo ndiyo jambo tunalolifanya sidhani kama jambo hili, linaweza sasa kugeuka kuwa dhambi nilitarajia Mbunge wa Jimbo hilo angalau wangesema hilo limefanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho uchimbaji wa madini kote nchini una sifa tatu ya kwanza ni *capital intensive* inaitaji fedha nyingi ili uifikie madini, ya pili ni *time intensive* unahitaji muda mrefu kupata ku-*develop* mgodi mmoja unahitaji kwa wastani wa kuanzia miaka sifuri mpaka kumi na tano mgodi mkubwa haiwezekani uchimbe leo kesho upate, wachimbaji wanajuwa siri hii ndiyo maana wapo wanaendelea na katika vikundi vilivyopo havifiki elfu moja kama anavyosema, tunavyo vikundi mia saba thelathini na tano na hakuna hata mmoja alieondoka kwenye uchimbaji wanaendelea kuchimba tuzungumze kwa haki tuwatendee haki watanzania hao tusiwavunje moyo wanatafuta fedha

kwa ajili ya kuendesha familia zao na sisi tufanye siasa kwa ajili ya mambo yetu nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba fursa ziko mbili moja ilikuwa umalizie mchango wako...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea.

NAIBU SPIKA: Unamalizia mchango wako.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea.

NAIBU SPIKA: Karibu!

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimsihi Waziri nimemuomba alete taarifa kwenye Bunge, alete taarifa rasmi kwenye Bunge kwa sababu hata haya anayoyasema ya vikundi mia saba, mia tatu mia mbili mimi nimefanya utafiti wangu ye ye alete taarifa yake *formal* kwenye Bunge hili, ili i-bind.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome ngoja kwanza kanuni ili Waziri alete taarifa lazima mimi ndiyo nimwambie siyo kwa kuambiwa na Mbunge na sijamwambia alete hizo taarifa kwa hivyo wewe unavyoileweka si mimi nilieagiza ni wewe kwenye mchango wako. Kwa hiyo, siyo nilieagiza ye ye kapewa nafasi ya kutoa taarifa na amekuba taarifa kama wewe unapingana unapingana na hiyo taarifa sema uipokei, kama unaipokea ipokee ama kama wewe unazo takwimu tofauti na alizozitoa pia unaruhusiwa kuzisoma.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe kiti chako kimuelekeze Mheshimiwa Waziri atuletee taarifa hiyo nikuombe iwe sehemu ya mchango wangu ili Bunge hili lijiridhishe na kile ambacho nakisema alete taarifa rasmi.

MBUNGE FULANI: Taarifa ngoja nimsumbue.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumuache Mheshimiwa Salome kabakiza dakika moja tu amalize muda wake.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, si nimesema kwamba kituo cha afya kipo kimoja kati ya kata kumi na saba na hiyo sinimewasifia jamani au mnataka nisemeje kwasababu sehemu nyingine sio mpaka tusifie. Yaani ni hivi kituo kipo kimoja kilijengwa enzi za JK na Magufuli amekuja kukiendeleza hakuna jipya aliyolifanya kwenye Mkoa wa Shinyanga si nimewasifia jamani au mnataka nisemeje. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusivutane sana mwisho wa siku ibara ya 100 ya katiba inasema Mbunge yupo huru kutoa mawazo yake na mimi mawazo yangu kwenye jimbo la Shinyanga suala la vikundi Serikali kupitia halmashauri wameona ndiyo dirisha dogo la kupata *own source* kupata mapato imesajili vikundi mimi nimesema elfu moja, Waziri ame-*confirm* amesema ni mia saba wamesajili vikundi mia saba kila kikundi Serikali inachukuwa shilingi elfu kumi na moja mara mia saba ni shilingi ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara mia saba ni shilingi ngapi hiyo hela, Serikali inasema yeye kazi yake ni moja tu kwenda kukusanya mrahaba na kusimamia mapato ya Serikali, kuhusu wale watu wanapata hawapati wanapata hasara kuna *value for money* siyo kazi ya Serikali wanaota vipara siyo kazi ya Serikali, na watanzania wamesikia nimewafikishia kilio chao ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, atafuatiwa Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mheshimiwa Dkt Lameck Mwingulu Nchemba ajiandae.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa fursa ya kuamka sana siku ya leo na

kukutana humu ndani. Naomba nichangie hoja chache katika bajeti hii ya TAMISEMI kwa kuanza kwa kumshukuru sana na kumpongeza sana Rais Dkt. Magufuli kwa hatua za ujasiri na uwadilifu wa hali ya juu alizozichukuwa katika Awamu hii ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, binafsi natokea kwenye jimbo la pembe zone jimbo ambalo kwa miaka mingi sana kwa kweli limekuwa nyuma kimaendeleo kwa maana ya miundombinu ya kila aina. Lakini ninavyozungumza sasa hivi kuna maendeleo makubwa sana Mheshimiwa Halima tuheshimiane. (*Makofi/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Amesha vuta huyo achana naye.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi jimbo langu kwa kweli limepiga hatua katika maendeleo ambayo yanazungumzwa katika bajeti hii lleje hajaachwa nyuma, tuna barabara ya lami inayojengwa kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi na barabara hiyo imeanza kutengewa fedha Awamu hii ya Tano, barabara hii itakwenda mpaka Kyela Kasumulu mpaka sasa hivi imetengewa fedha mpaka Isongole. Vilevile, vitu vyaa afya viwili tumejengewa vikubwa na hospitali ya Wilaya kubwa sana nzuri ya kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la elimu Maji, Maji Umeme wa REA, ni maeneo ambayo huko nyuma tulikuwa nyuma sana lakini sasa hivi kila unapokwenda kwenye vijiji vyetu umeme upo na unaendelea kuwekwa. Kwa hiyo, hizi ni juhudhi ambazo zimefanywa na Serikali Chama cha Mapinduzi Awamu ya Tano na nitakuwa mtovu wa shukrani nisiposema pongezi kwa Rais lakini pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Jafo, Manaibu Waziri wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii wanafanya kazi kubwa sana. TAMISEMI ni Wizara kubwa lakini inasimamia eneo kubwa sana la nchi yetu na lazima tuwape pongezi kwa kazi wanayoifanya. Hatuwezi kuja hapa tukatoa maneno ya shutuma na maneno ya kejeli kama vile siyo binadamu tunaelewa umuhimu wa watu kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ni hatua, maendeleo ni *process* ni mchakato, leo hii kuna corona Marekani wanalia na wao ndiyo mataifa yaliyoendelea kwa hiyo, lazima tutambue kuwa maendeleo ni hatu na vitu kama vinajengwa kidogo kidogo *incrementally* lazima tutambue kwa huo ni mchango mzuri kwa maendeleo ingekuwa hakuna kinachofanyika kabisa tungeweza kusema kwanini hakuna kinachofanyika, lakini kwa kuanzia nilitaka kusema hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la miundombinu ambalo wilaya nyingi za pembe *zone* tumekuwa tukipata shida kubwa lleje moja wapo sasa hivi tunazungumzia mvua njia nyingi zilizonyesha na kuharibu Barabara lakini kwangu mvua ni kawaida kila mwaka mvua ni nyingi sana na kwa hali hiyo barabara zangu zitakuwa zimeongezeka tu kuharibika lakini nilikuwa namiundombinu milbovu sana ya barabara hasa zinazounganisha wilaya yangu na wilaya za jirani kama Wilaya ya Mbeya vijiji, Wilaya ya Rungwe, Wilaya ya Mbozi tunahitaji sana barabara hizi tusaidiwe fedha ya kutosha *TARURA* kwa ajili ya kuzijenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, barabara zinazounganisha kata kwa kata kuna tatizo kubwa sana la mizunguko mirefu ya wasafiri na usafirishaji kwasababu wa umbali kati ya kata na kata ili hali kuna nafasi ya kujenga barabara ambazo zinaunganisha kata kwa kata fupi zaidi ambazo zinabidi zipite kwenye milima ziwekewe madaraja ya kutosha kuweza kupitika na kutumika kwa kuboresha uchumi wa lleje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lleje ni Jimbo ambalo linarutuba, lina ardhi nzuri lina mvua nyingi na linaweza kuzalisha mazao yoyote yale unayoweza kuyafikiria lakini tunahitaji miundombinu bora ya kuunganisha kata zetu vijiji vyetu na masoko. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana barabara ya Shingamba kata Ibaba kilomita 26 lakini hii barabara ilishatengewa bajeti hajengeki kwa sababu ya miundombinu ya mvua mikubwa sana. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana *TARURA* waweze kuisimamia hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara zinazotoka Rubanda kwenda Mtula, nina kata ambazo uwezi kwenda wakati wa mvua hazifiki na hii ni miaka yote kwa hiyo tunapozungumzia mvua wakati huu ni nyongeza tu, ninahitaji sana jicho la pekee kwa ajili ya hii na nimeshamuomba Mheshimiwa Jafo kuwa nitaenda kumuona juu ya jambo hili kwa sababu bila hivyo lleje haitaendelea kwa haraka kama ambavyo naitegemea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia vilevile, suala la daraja, kuna daraja moja liliharibika tangu mwaka 2017 linalounganisha Mbozi na lleje. Hili ni daraja muhimu sana kwa ajili ya masoko ya wakulima wetu lakini vilevile, linaunganisha barabara inayokwenda Vwawa. Nilikuwa naomba sana daraja hili sasa litizamwe tumeshapeleka maombi ya bajeti hatujapatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja lingine la muhimu sana kwetu ni lile linalounganisha lleje na Mgodi wa Kiwira liko kwenye Mto Mrisi ambalo fedha tayari ilishatengwa, nafikiri sasa ilikuwa ni suala tu la kuachia hiyo fedha TARURA watujengee hili daraja. Ni la kilomita saba tu lakini limekaa muda mrefu na inasababisha ule mgodi hata utakapokuwa ukianza kufanya kazi haitawezekana sisi kuitisha mawe yale lleje, itabidi yazungukie Kyela. Kwa hili nalo ni eneo ambalo nilikuwa naliomba sana wizara hii itusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala kubwa sana la shule, lleje nafikiri katika wilaya chache sana au kama viro haina shule yoyote ya wasichana ya bweni na yenye masomo ya sayansi. Naamini kila wilaya inapaswa kuwa japo na shule moja ya wasichana ya sekondari. Kulikuwa kuna juhudhi tulikuwa tunazifanya za kutafuta wafadhili lakini imeshindikana.

Nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Jafo hili nalo uliingize katika bajeti yako ili nipate shule moja ya wasichana kwa sababu mimba za utotonu ndiyo zinapoanzia watoto wa kike inapowabidi waende wakapange kwenye sehemu za watu kwa ajili ya kwenda madarasani. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana Mheshimiwa Jafo shule ya wasichana ya bweni kwa ajili ya Wilaya ya lleje lakini madaja yangu makubwa ambayo nimeyataja na barabara za kata kwa kata, barabara za wilaya kwa wilaya. Nakuomba sana, kilio changu kikubwa ni miundombinu mambo mengine yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi ajiandae.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nataka mchango wangu....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema una dakika tano.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, basin *a-shift position* naenda moja kwa moja kwenye Corona. Nafikiri kama kuna Mbunge ana-treat sana na kumsumbuwa sana Mheshimiwa Waziri Ummey kuhusu ugonjwa mimi naongoza. Kwenye kundi la Waheshimiwa Wabunge tunatofautiana mawazo na Waheshimiwa Wabunge sana lakini kwa nia njema kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona Taifa kama Marekani wanazika watu 2,000 kwa siku na nguvu ya uchumi waliyonayo na ya kitabibu, ukaangalia mzaha unaofanyika katika Mataifa ya Afrika likiwemo Taifa letu ni bado kipenga hakijapiga. Nakuhakikishia hii mnayosema kwamba hili Taifa lina Mungu, ni muumini wa Imani ya Kikristu, naamini maandiko lakini maandiko yanasesma, hata Yesu hakutenda miujiza mingi kwao kwasababu ya kuto kuamini kwao. Unapokuwa ni kiongozi wa nchi una-deal na watu wenye imani tofauti katika nchi, unapokuwa Waziri ama Mbunge una-deal na watu tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na viongozi wanaoamini katika maandiko ni baraka kwa nchi lakini tukiwa na viongozi ambao hawawezi kutafsiri maandiko ni hatari kubwa sana. Nina taarifa ya mambo yanayoendelea ndani ya nchi hii, hili ni Bunge tuko hapa. Mwenyekiti Mheshimiwa Mbewe familia yake mtoto wake aliathirika na yuko hospitali, *thinking* ya kwanza tu ingekuwa ni hivi, kama huyu Mwenyekiti Mheshimiwa Mbewe ni Kiongozi ya Upinzani, anakaa kwenye Kamati ya Uongozi ya Bunge ambao Mheshimiwa Naibu Spika wewe umo, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wenyevit wa Kamati ambao wanakuja kwenye Kamati za Bunge. Amesema tu kwamba sehemu ya familia yangu imeathirika na ni Kiongozi wa Upinzani Bungeni anakutana na Wabunge wa *Opposition* ambao hao wote sisi ni marafiki. *Concern* ya kwanza ya kuonesha kwamba hili jambo ni *serious* ningetarajia kuona bunge zima vinakuja vipimo, tunachukuliwa vipimo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya utafiti unasema Waafrika, na ndiyo mgogoro ulioko China kwamba Waafrika wanaweza waka-*carry* hii Virus kwa muda mrefu kuliko wazungu na wachina na ndiyo sababu wanawapiga *burn* kule kwao. Sasa nina wasiwasi, ikiwa nimeambukizwa na ninaweza nika-*carry* vile virusi kwa siku 30, siku 21 mpaka 30, halafu nikaambukiza wengine maana yake ni nini. Kwenye bunge hili yuko Mheshimiwa Waziri Mkuu, upo wewe ambao nyie wenywewi ni *corridor of power*, Mheshimiwa Waziri Mkuu akipata ni rahisi Mheshimiwa Rais kupata, ni rahisi Mkuu wa Jeshi kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mko kwenye vita kubwa kama hii unahitaji kuona Mheshimiwa Rais anakuwa na afya, Mheshimiwa Waziri Mkuu anakuwa afya, Mheshimiwa Spika anakuwa. Sasa najiuliza, kama ni mbunge niko ndani ya bunge na hapa yuko Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri yaani nyie ndiyo *corridor of power* hatujapimwa na hapa nawatemea mate wakati naongea hatujapimwa, najiuliza itakuwaje ugonjwa huu utakapolipuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala ni *very serious* na kwa bahati mbaya utamaduni ama style ya viongozi wanavyoishi, kuonekana kwenye kahawa, kuonekana mitaani akina Makonda, akina Gambo inafanya wananchi waone hili jambo siyo kubwa. *Seriousness* ya *leadership* kwenye hili jambo lazima *life style* yetu ibadilike, isipobadilika wananchi wanaona kama ni kawaida. Juzi nimezunguka Arusha na gari tinted...

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

TAARIFA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nina taarifa ya mambo mawili; la kwanza Mheshimiwa Mbowe ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Chama cha CHADEMA ambaye mtoto wake aliugua, kwa taarifa zilizoko halali ni kwamba ana nyumba mbili kwa hiyo siku hiyo hakuwa kwenye nyumba ambayo matoto aliugua. Kwa hiyo, hakupata *contamination* yoyote isipokuwa aliogopa tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa taarifa ni moja tu.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Aaa! Sawa.

NAIBU SPIKA: Taarifa ni moja tu japo sijaelewa vizuri uhusiano, lakini Mheshimiwa Lema unaipokea taarifa hiyo?

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza kuongea nyumba za watu humu ndani, naweza nikabaki mwenyewe hapa, yaani tukianza hizo *story*, naweza nikabaki mwenyewe hapa. Kwa hiyo niseme tu haya mambo ni binafsi sana na huyu namfahamu na wewe unamfahamu

ndio maana wewe umeichukulia poa nilindie tu muda wangu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema huu ugonjwa utaua watu wengi Afrika, kwanza *life style* ya watu. Marekani wana zile *ventilator machine* zaidi ya 1,050,000. Sasa huku mitaani ukienda watu wanapeana moyo unajua hii *corona* mpaka uende hospitali, leo wakiumwa wagonjwa 50 hapa wakapelekwa hapo *General/hakuna mashine za kuwapa life support*. Sasa najiuliza wakianza kuumwa wagonjwa 200 kila siku, mikoani Singida ambako kuna mashine mbili, Shinyanga kuna mashine tatu, Tarime, Mbeya wakianza kuumwa wagonjwa wengi hali itakuwaje. Ndio nikasema hili suala sio llani ya Chama cha Mapinduzi, hii ni bahati mbaya ya ulimwengu, wasijisikie aibu kuleta hilo jambo hapa Bungeni tujadili bajeti na mikakati ya kuliondoa hata kama *lockdown* sio *solution*. Tukisema maneno haya mnasema hawa CHADEMA wanataka *lockdown* ili uchaguzi uahirishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, uweke kumbukumbu siku ya leo hakuna wiki tatu, utatafuta Wabunge hutawaona hapa, ngoja ianze kukamua sasa hivi watu wanaishi poa tu, huko mitaani poa tu, ngoja ianze kukamua, hata Mbeya hutaenda kutafuta kura nakuhakikishia. (*Makof/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Lema.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu

NAIBU SPIKA: Umesemaje Mheshimiwa Salome?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Ameshamaliza mchangiaji na kuhusu utaratibu soma vizuri hiyo kanuni yako ya 68.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome naomba ukae.

Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mheshimiwa Dkt. Jumanne Shukuru Kawambwa ajiandae.

MHE. DKT. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia mada hii muhimu kabisa. Kwanza nianze kwa kuweka kumbukumbu sawa, nimefuatilia wachangiaji wengi wakiwa wanalipotosha sana suala hili la vituo vya afya. Mchangiaji mmoja amesema kwamba tumejenga vituo vya 433 na anaweka neno tu na anasema tulisema kila kata na akaweka orodha ya kata zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mchangiaji wa aina hii ni mchangiaji ambaye hajaelewa kile Rais Magufuli anachokifanya. Rais Magufuli anachokifanya ukiangalia vitu vingi sana anavyofanya na Wabunge muitikie ni *next level*, hivyo vitu ni vya *generation* inayofuata sio vitu vya leo wala sio vya kesho tu. Tulipoweka kwenye ilani kwamba tutakuwa na kituo cha afya kila kata na ramani zake Waheshimiwa Wabunge ninyi mko majimboni mnatambua vituo vile ambavyo tayari tulishajenga kwenye kata vikoje ni jengo moja tu lina *u-shape*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini anavyojenga Rais Magufuli vina majengo ziadi ya nane na hesabu anayoipiga Rais Magufuli ukienda kwenye nchi yetu tuna tarafa karibu 527 na vituo hivi vinavyojengwa ambavyo kwa kweli vina hadhi ya Hospitali ya Wilaya vimekaa kwenye makao makuu ya tarafa, ukichukua 433 ukajumlisha na 98 vile ambavyo ni vya halmashauri maana yake unapata 531. Anachotuambia Rais Magufuli ni nini, amejenga Hospitali ya Wilaya kila tarafa na kwenye vituo hivyo vilivyojengwa kuna wodi ya wazazi, kuna wodi ya watoto, kuna OPD, kuna jengo la *operation*, kuna jengo la kuhifadhi miili ya wale amba Mungu atakuwa amewapenda; ukijumlisha hivyo vitu vilivyojengwa halafu wewe ukawa unalilia ile *u-shape* maana yake wewe uko

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

nyuma sana, uko *outdated*, uko mbali sana na mawazo anayowaza Rais Magufuli. (*Makofi*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nchemba kuna taarifa, Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba pale, sera ya afya inasema kila kata kituo cha afya, hata ukija ukajenga hospitali yenye vyumba 32 viko kwenye kata moja. Ilani yao ya Chama cha Mapinduzi walisema 2015/2020 kila kata kituo cha afya, ndio nikasema taarifa nampa nivumilie kidogo tu. Waziri amesema wamejenga vituo vya afya 433, zahanati 338, kwa hii kasi ya Magufuli ambayo mnaisifia, nikasema kufika huku tunabakiza vituo zaidi ya 3,000; mnahitaji miaka 50, miaka 59 ya uhuru mkasema mmejenga vituo 938 sasa...

NAIBU SPIKA: Haya Mheshimiwa Matiko...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hamja-*justify* ukubwa wa kituo kipo kwenye kata

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba unaipokea taarifa hiyo?

MHE. DKT. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, unajua Mheshimiwa Esther na Wabunge wenzake muda mwingi walikuwa mahakamani kwa hiyo hawakufanya shughuli za kuhamasisha wananchi wao ili waende sambamba na haya mambo ambayo Rais Magufuli anafanya. Hivi tunavyoongea pamoja na kujengwa hivi vikubwa ninavyosema ni hospitali za kila tarafa jambo hili halijasimamisha ujenzi wa vituo vingine vya kila kata na hivyo vinaendelea. Hii tunayoripoti ni vile ambavyo vimeshakamilika na huduma zinaendelea na wananchi wanalielewa vizuri sana jambo hili, kwa maana hiyo hiki kitu anachokisemea

anataka kuhamisha magoli baada ya kuwa tumeshaanza mchezo huu. Wananchi wanamuelewa sana Rais Magufuli na niseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasidhanie kwamba kujenga vituo vyenye hadhi ya hospitali kila tarafa ndani ya miaka minne kwamba ni jambo jepesi hili ni jambo kubwa mno na wananchi wanayaelewa majengo haya na yanawasaidia. Nashangazwa sana ukiona akinamama hata wao hawapongezi kwamba vituo hivi vitaokoa maisha ya akinamama, watoto, yaani ukiangalia mtu ambaye alitakiwa atoke Ndulungu kule aikimbilie Kiomboi, lakini sasa hivi anaenda Ndago halafu mwenzetu asione kabisa jambo liliofanyika hii ni kutokuwa *fair* kwenye ukweli na kutokuwa *fair* kwa yeye mwenyewe. Kwa kazi hiyo nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa jambo hili kubwa ambalo ametengeneza historia katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge jambo lingine ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya kwenye Wizara hii, Wizara hii miaka iliyopita kwa Wabunge mliokuwepo mtakumbuka ikiwa chini ya Waziri Mkuu, tunapokuja kujadiliana tulishaipa kila jina, mara ni mchwa na kila majina tulikuwa tunaipa wizara hii. Upotevu ulikuwa mkubwa usioweza kukadirika, lakini leo hii tunajadiliana mafanikio kwenye wizara hii. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais na msaidizi wake Mheshimiwa Jafo ambaye kwa kweli wamefanya kazi nzuri. Waheshimiwa Wabunge angalieni sasa hivi hatuongelei haya maneno ya mchwa, sijui wizi, bali tunaongelea vituo vyta afya vyta kisasa kabisa ambavyo vinapatikana hata kwenye nchi zilizoendelea. Kwa hiyo tuna kila sababu ya kupongeza jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nimeshasikia kengele ya kwanza nihamie kwenye jambo hili ambalo limeongeleta kwa sura tofauti tofauti hili jambo la *corona*. Hili jambo viongozi ni vyema tukawa na kauli moja, tusifanyie siasa kabisa kwenye jambo hili, twendeni tufanye siasa kwenye mambo yaliyoko kwenye ilani, hili jambo tuongee lugha moja. Niwapongeze sana viongozi wa kidini,

wametuzidi wanasiwa, wanaongelea jambo hili kwa umakini mkubwa. Jambo la kwanza na lugha ya kwanza ambayo inatakiwa itoke kwa viongozi ni kuwahamasisha Watanzania kila mmoja yeye mwenyewe awe mtu wa kwanza kubadili tabia, lakini tunavyoongea kila wakati tunataka kuonesha kama kuna jambo Serikali haijafanya, tunawapoteza watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikiliza lugha zingine unakuta mtu anaongea eti mabasi yanajaa, eti bado tunapitia madirishani unamwambia nani? Wewe unatoka tu ulikokuwa unaelekea nyumbani kwenu kwa nini uingilie dirishani, hivi kweli Serikali ikutafutie gari la kuondokea au Serikali itafute polisi wa kila mtu mmoja wa kumzuia asipite dirishani? Serikali itatafuta polisi kukabiliana na majambazi si kutafuta polisi kwenda kuzuia eti watu wasipitie madirishani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili jambo viongozi tuwe na lugha moja Watanzania kila mmoja achukue hatua kali kweli kwenye jambo hili. Na nilivyokuwa nawaza nilikuwa naona hata taarifa tunazotoa labda zibaki za aina tatu tu, tutoe taarifa ya kwamba hili gonjwa bado lipo, tutoe taarifa ya watu waliopona na tutoe taarifa labda ya wale ambao imekuwa bahati mbaya sana. Lakini hivi tunavyoweka kama tofali kama nchi zinashindana kwamba zime-*develop* wagonjwa wengi, naona hiki kitu na chenyewe kama hakijakaa sawa na sijui kwa nini wengine wanatamani sana takwimu ziwe nyngi na wanatamani kuwe na wagonjwa wengi, sijui ni kwa ajili gani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema jambo la kipumbavu likisemwa kizungu huwa linaonekana la maana, labda kwa sababu ilianza kule majuu mnaona kama sifa, bado mnaona tu kwamba eti watakuja wengi wataugua wengi, ninyi mna kikao na Mungu, kama Mungu ameamua kutunusuru na jambo hili ninyi kwa nini mnatamani kwamba itakuwa kubwa zaidi. Watanzania tubadili tabia kwenye jambo hili na naamini Mungu yuko sambamba nasi na ndio maana mpaka sasa ameendelea kutunusuru.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nchemba kuna taarifa, Mheshimiwa Esther Bulaya.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anayeongea amesema jambo hili tusilifanyie siasa. Sasa ye ye ndio anayefanya siasa, kuchukua tahadhari sio kuombea mabaya na tumekuwa tukipeana tahadhari kama Taifa, tunaleta mzaha hivi hivi halafu baadaye yanatupata, tutakuja kulaumiana. Hakuna anayeombea janga hili litupate wote tunakubaliana ni baya, tunasema tuchukue tahadhari kabla madhara makubwa hayajatokea na sio dhambi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Esther Bulaya., Mheshimiwa Mwigulu Nchemba malizia mchango wako.

MHE. DKT. MWIGULU L. NCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, Esther sijaona hata anachotolea taarifa ni kipi maana yake anachokisema ndicho Serikali inafanya na kiongozi mkuu wa tahadhari amekuwa Mheshimiwa Rais ye ye mwenyewe, kwa hiyo hiki naona anapigia mstari Serikali inachokifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kinachotushangaza ni kile ambacho kila wakati wanaona kama halijafanyika hilo, halafu namsikia anaongelea kwamba kule Iramba, mimi ninao uwezo wa kushinda jimbo lolote la upinzani kule, sasa ukiongelea Iramba huko ni kumfuata mamba kwenye kina kirefu cha maji, kwa hiyo hata sina hofu na wengi wanani pa taarifa, kwa sababu mwaka kesho watakuwa *gallery* kule wakinangalia mimi nikichangia hapa. Kwa hiyo nakushukuru sana acha watoe taarifa. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Maombi humu ndani yamepigwa sana katika Bunge hili kwamba kila mtu humu ndani aliyeko arudi, sasa wale walioko nje sijui watapita wapi ndio sijaelewa. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge tuendelee, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Jumanne Shukuru Kawambwa na Mheshimiwa Joel Makanya ajiandae.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwapa nguvu na afya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri wa TAMISEMI, nawaombea Mwenyezi Mungu aendelee kuwasimamia katika shughuli zao wanazozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana kwa Watanzania ndani ya miaka yake hili minne katika uongozi wake na hali kadhalika chaguo walilochagua katika kuipa Wizara ya TAMSEMI, akampatia kijana Jafo kwa kweli kura yake na chaguo lake lilikuwa ni mahali pake. Kiti kimepata mtu, mtu hakupata kiti, kwa hiyo tunamtakia kila la heri katika shughuli zake hiso. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia mambo matatu kama sio manne. La kwanza kabisa ni kuhusu suala la *TARURA*. *TARURA* wamefanya kazi kubwa sana, lakini bahati mbaya ama bahati nzuri mvua imekuja na kuharibu kazi nzuri waliyofanya. Sasa basi wengi wetu tumezungumza kwamba *TARURA* waangaliwe, mimi nasema kwamba tulichonacho mkononi ndicho tuzungumze nacho, tulichonacho mkononi ni asilimia 70 kwa 30. Tunaomba hiyo asilimia 30 iongezwe ifike asilimia 60, wapi itatoka Waziri wa Fedha ataelewa, tuweze kuiongeza kwa hivi sasa watoke na asilimia 60 ya pato la bajeti katika shughuli zao. Kwa kuwa hawa ndugu zetu bado wanahitajika kuunganisha vitongoji, vijiji na kata; *TANROADS* wameshatuunganisha na nchi za jirani, kimkoa na kiwilaya lakini *TARURA* bado wana kazi ngumu, tunaomba tutafute fedha kwenye bajeti hii tuwapatie angalau asilimia 60 ya bajeti yao ili waweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana ya vijiji kwa mfano kule Mkoa wetu wa Rukwa, Kinamwanga walipata mafuriko barabara haitumiki, bado Senga na Wipanga, bado Katumba, Pito Malagano, Majengo, Kingombe, Ulingi, Malonje, Milundikwa, Kanasi, Nakitosi, Wampembe hali kadhalika Namasi mpaka kufikia Ninde barabara hizi sasa hivi hazipitiki kabisa. Kwa hiyo bado tunahitaji ifahamike wazi kwamba hawa ndugu wa *TARURA* wanahitajika kupewa asilimia 60 ya bajeti yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu barabara ya Kibaoni, Kiliyamatundu, Miangarua kuunganika na barabara ya Tunduma- Sumbawanga, barabara hii madaraja yote yamekwisha, barabara imekanyagika kabisa haiwezi kupitika. Tunaomba barabara hii na naendelea kuiombea tena, tunaomba iwe katika barabara za mkakati kwa maana ya Mkoa wa Rukwa. Hii barabara ikikamilika nina imani kabisa kwamba itatuokoa katika mkoa wetu wa Rukwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati katika jibu langu la tarehe Mosi Aprili la kuhusu barabara ya kutoka Kawala kwenda Kalambo Falls kwamba sasa ndugu zangu wa *TARURA* wamepewa wafanye usanifu wa kina ili barabara ile iweze kujengwa kwa lami. Kwa hilo napenda kutoa shukrani sana kwa Serikali kuweza kulitambua kwamba nasi watalii tunawahitaji wafike Kalambo Falls.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia 2 % ya 10% ya wenye walemovu ambao si nadra kupatikana katika ujasiriamali kwa maana ya kikundi cha watu watano hata kikundi cha watu 10. Ushauri wangu kwa Serikali naomba hawa wenye ulemavu wapewe hata mtu mmoja mmoja ama watu wawili ili wawe na kitambulisho maalum cha kijiji ama cha mtaa kwamba huyu mwenye ulemavu anakaa mtaa huu, huyu mwenye ulemavu anakaa kijiji hiki. Kwa hiyo kijiji na mtaa kunakuwa ndio watakaofuatisila katika marejesho ya yule mwenye ulemavu lakini tukisema wenye ulemavu watano, au 10 hawawezi kupatikana. Kwa hiyo tunaomba

Serikali waifanye hivyo katika vikundi ama katika kuwapatia mkopo ule wa asilimia mbili kutoka kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Maafisa Watendaji wa Mitaa na Vijiji, tunao wachache. Tunaomba tupate ajira ya vijana hawa katika vijiji na katika mitaa yetu. Utakuta afisa mmoja anashika mitaa mitatu au minne ambapo kunakuwa hakuna ufanisi wa kazi. Tunaomba tupatiwe ajira za hawa watumishi kwa sababu tunao wasomi wako mitaani, Walimu na wataalam mbalimbali katika mitaa yetu na vijiji vyetu. Kwa hiyo ndio kusema wamba wa kuajiriwa wapo, wanahitaji vibali na hata halmashauri wameshatoa maombi ya vibali ila bado havijapatikana. Tunaomba vibali vitolewe ili Maafisa Watendaji wa Kata, Vijiji na Mitaa waweze kuajiriwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu watumishi wa zahanati na wa vituo vya afya walistaafu; walikuwa wanachangia katika Mfuko wa PSSF, tangu mwaka juzi 2018 mwezi Agosti wamestaafu, lakini mpaka leo hii bado hawajapata haki zao. Naomba suala hili liweze kufatiliwa ili kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine katika ukurasa wa 41 ni kwamba, kuna magari yamenunuliwa; magari hayo yamegawanywa tayari kwa maafisa mbalimbali wa ngazi ya mkoa na wilaya, lakini sikuona mgao wa Maafisa Maendeleo ya Jamii. Hawa hawakupata mgao wa magari. Hali kadhalika ukurasa wa 42 kuna pikipiki zimenunuliwa, lakini waliopewa ni Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Maendeleo ya Jamii bado hawajapata usafiri, lakini hao Maafisa Maendeleo ya Jamii tunawahitaji kwenye mitaa yetu, vijiji vyetu na kata zetu na ndio wanaosimamia na kufuatilia hizi asilimia 10 zinazotoka kwenye halmashauri; kutoa elimu kwenye vikundi, kutoa maelekezo kwenye vikundi, lakini wao hawana usafiri.

Kwa hiyo, tunahitaji Maafisa Maendeleo ya Jamii wapatiwe usafiri; ngazi ya wilaya na ngazi ya mkoa wapatiwe magari na ngazi ya kata na vijiji wapatiwe pikipiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia ...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa Silafu, ahsante sana.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Jumanne Shukuru Kawambwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mheshimiwa George Malima Lubeleje ajiandae.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia uhai na uzima na kutuwezesha kuhudhuria katika Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Jemedari, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa maono ya mbali na kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika kuboresha huduma ya afya nchini kwetu, huduma ambayo imeweza ujenzi wa jumla ya zahanati 368 katika kipindi cha miaka mine, vituo vya afya 433, hospitali za halmashauri 98 na mgao mkubwa wa madawa katika hospitali na zahanati zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kazi kubwa sana na ambayo haijawahi kufanywa wakati mwingine na inachangia maboresho ya huduma ya afya na ustawi wa wananchi wetu. Rasilimali kubwa ya nchi ni wananchi na wananchi wenye afya ndio watakaoweza kulisukuma taifa hili mbele.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Naibu Spika, ujio wa *Corona* katika dunia kwa upande mwingine umeonesha namna mtazamo au maono ya Rais na Serikali ya Awamu ya Tano ya kuweka kipaumbele katika huduma ya afya na kutekeleza ujenzi mkubwa wa miundombinu ya afya, kama vile walijua kwamba bila ya maandalizi mazuri ya afya katika nchi yetu, tunaweza tukakumbwa na milipuko ya magonjwa ambayo yatatukuta katika hali ngumu sana. Miundombinu hii ya zahanati, vituo vya afya na hospitali imetuweka katika hali bora zaidi sasa hivi ya kuweza kuwahudumia wananchi wetu kuliko kama miundombinu hii mingi ingekuwa haikujengwa, wananchi wangehudumiwa maeneo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu atuepushe na ugonjwa huu, lakini kama tukiingiwa na milipuko maana yake sasa hivi tuna miundombinu bora zaidi ya kuweza kushughulikia wananchi wetu ambao watakuwa wamekumbwa na ugonjwa huu. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali yangu, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa maono ya mbali haya na kwa kazi kubwa ambayo imefanywa katika Awamu hii ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ujio huu wa *Corona* unaonesha kwamba kazi kubwa bado inabidi tuifanye. Kuna maeneo ambayo bado hayana zahanati na vituo vya afya. Kwa maana hiyo ni lazima sasa tuihamasishe Serikali kuongeza juhudhi na bajeti kwa ajili ya kujenga zahanati na vituo vya afya vingi zaidi ili wananchi wetu wengi zaidi waweze kupata huduma za afya katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Bagamoyo kutoa shukrani zangu nydingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutujengea vituo vya afya viwili, kimoja Kerege na kingine Matimbwa. Kituo cha Kerege kinafanya kazi nzuri sana, kinawahudumia wananchi na kinaendelea vizuri. Ni kituo cha mfano, kilikuwa namba moja katika awamu ile ya pili ya ujenzi wa vituo vya afya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Matimbwa nacho kimekamilika, kina upungufu wa vifaa tiba. Naomba Mheshimiwa Waziri Jafo kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya atuharakishie kupata mgao wa vifaa tiba kwa Kituo hiki cha Afya cha Matimbwa ili nacho kiweze kuungana na vituo vingine kutoa huduma nzuri ya afya kwa ajili ya wananchi wetu. Nina uhakika Mheshimiwa Waziri kwa juhudzi zake bila shaka siyo muda mrefu tutaweza kupata vifaa tiba. Leo hii halmashauri imeamua kukizindua Kituo cha Afya Matimbwa pamoja na uhaba wake wa vifaa tiba ili kuhakikisha wananchi wanaanza kupata huduma katika kituo hicho cha afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika barabara hii ya Bagamoyo - Msata, Kata zetu za Magomeni, Makurunge na Fukayosi ambazo zina jumla ya vitongoji 36, hazina kituo cha afya hata kimoja. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri katika mipango yake aangalie uwezekano wa kuweza kupata walau kituo kimoja cha afya kwa kata hizi na vitongoji hivi zaidi ya 36 katika Jimbo langu la Bagamoyo ili tuweze kupata huduma nzuri. Hususani kituo hiki cha afya kiwe katika Kijiji cha Fukayosi na Kata ya Fukayosi ili kiweze kutoa huduma katika vitongoji hivi pamoja na vitongoji vile ambavyo viro katika Kata ya jirani ya Kiwangwa ndani ya Jimbo la Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie katika sekta ya miundombinu ya barabara. Kwanza, naomba kutoa shukrani nyngi sana na pongezi kwa Mheshimiwa Rais na Serikali ya Awamu ya Tano kwa utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa kilometra 5 za lami katika Mji wa Bagamoyo. Mita 620 zimeshakamilika na mita 630 sasa hivi ziko katika hatua za ujenzi. Zilizobaki ni kilometra 3.75, namuomba Mheshimiwa Waziri azisimamie ili ahadi hii ya Mheshimiwa Rais iweze kutekelezwa kabla ya miaka mingi kupita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ina mtandao wa barabara za mjini na vijijini wa jumla ya kilometra 520. Barabara hizi nyngi ziko katika hali

mbaya na hasa katika vipindi kama hivi vya mvua; vuli, masika, barabara hizi zinakuwa hazipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali kuzingalia kwa umakini sana barabara hizi za mijini na vijijini na hususani barabara za vijijini ndiyo mishipa ya damu ya uchumi wa nchi yetu. Kule vijijini ndiko kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao ya...

NAIBU SPIKA: Ya biashara.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, mazao ya chakula na mazao ya biashara, ndiyo miundombinu ambayo inasimamisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iangalie namna ya kuiongezea *TARURA* bajeti yake ili iweze kufanya kazi nzuri ya ujenzi wa barabara hizi katika nchi yetu. Ikiwezekana kuiwekea tengeo kubwa zaidi la Mfuko wa Barabara ili *TARURA* iweze kujenga barabara hizi za vijijini kwetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana, nashukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga atachangia kwa dakika tano, Mheshimiwa George Malima Lubeleje dakika tano na Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel dakika tano.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu mpewda wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumzia shida hii ya *Corona* ambayo imeikumba dunia. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna alivyolichukulia jambo hili kusema kwamba tuwe makini, tufuate taratibu na masharti tunayopewa na wataalam wetu wa afya lakini watu tuendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kufanya kazi itakuwa shida sana kuweza kuwahudumia wananchi wetu. Watu watoke wafanye kazi wajipatie riziki zao lakini tufuate masharti yote tunayoambiwa na wataalam. Maji ya kunawa tunawe tunapotakiwa, *sanitizers* kama zipo tuzitumie pale inapostahili bila kukosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, niendelee kwa kuipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii ya TAMISEMI. Tumemsikia vizuri Mheshimiwa Waziri ametoa taarifa yake lakini na mimi kama Mjumbe wa TAMISEMI mmeskia pia taarifa yetu ya Kamati ya TAMISEMI. Tumeyazungumza kwa umakini lakini tumeona kazi kubwa inayofanywa na Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la hospitali lilirozungumzwa hapa; hospitali 67 na katika bajeti ijayo kuna mpango wa kujenga hospitali zingine 27 sio jambo dogo, ni jambo la kujivunia kwelikweli. Suala zima la shule, kwamba tumekuwa na ongezeko la shule za msingi 914 katika miaka hii minne siyo jambo dogo, ni jambo la kijivunia kabisa. Kuna ongezeko la wanafunzi wapatao 1,832,000, hili sio jambo dogo, ni jambo la kujivunia na kuipongeza sana Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna huduma mbalimbali za wananchi zinazofanyika huko mfano umeme upande wa *REA*. Pamoja na kwamba natambua kabisa jimboni kwangu hadi sasa bado tuna vijiji 6 ambavyo havijaguswa kabisa na umeme lakini naamini kabisa kwa ratiba ya *REA*, Awamu ya Tatu kwamba itakapofika mwaka 2021 vijiji na vitongoji vyote ndani ya nchi hii vitakuwa vimepata umeme, naamini tutalitekeleza bila wasiwasi wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la maji. Tumekuwa na shida sana ya maji kwa nchi kama nchi. Kumekuwa na shida ya maji hata jimboni kwangu vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba katika miaka hii minne katika Jimbo la Chilonwa peke yake Serikali imeweza kutuchimbia visima 28, siyo jambo dogo. Katika visima hivi 28, visima saba nimechimba mimi kama Mbunge wao kwa kupitia Mfuko wa Jimbo, nifedha ya Serikali hiyo, kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongelea suala la barabara, tumesikia taarifa kwamba wameweza kutengeneza na kukarabati kilometra 74,940. Katika hizi zipo kilometra za Wilaya ya Chamwino na zipo kilometra za Jimbo langu la Chilonwa. Kati ya hizo kuna kilometra 485 za lami na katika hizi kilometra 485 za lami kilometra sita (6) ni za kwangu zinatoka pale Wilaya ya Chamwino, naipongeza sana Serikali hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mvua kubwa tulizopata mwaka huu. Tumepata baraka ya mvua na kwa hiyo tumepata chakula cha kutosha, kwa kweli tuna chakula cha kutosha lakini njia na madaraja yameharibika sana.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joel, muda umekwisha.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa George Malima Lubeleje, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, dakika tano, Mheshimiwa William Tate Olenasha ajiandae.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli, kwa kazi nzuri anayoifanya. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunaipongeza TAMISEMI ni kwa sababu wamefanya kazi nzuri. Kwa mfano, katika Wilaya ya Mpwapwa wamejenga Vituo vyta Afya vitano (5): Vituo vyta Mima; Mtera; Pwaga; Chipogoro; na Kibakwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bado namwomba sana Mheshimiwa Waziri akamilishe ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mbori. Kituo hiki ni muhimu sana kwa sababu kitahudumia Kata za Chamkoroma, Tububwe, Mseta, Mlembulwe, Matomondo, Kimagai, Godegode na Lupeta. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri akamilishe kituo hiki kwa sababu kitahudumia Kata ya Chamkoroma ambayo anaifahamu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna zahanati sita (6) ambazo sasa ni miaka kumi hazijakamilika. Kwa uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa hawawezi wakakamilisha zahanati hizi. Zahanati hizo ni Mgoma, Mzase, Igoji II, Salaza, Mlembule, Kisokwe pamoja na Kiseyu. Kwa hiyo, naomba sana Wizara yako isaidie kukamilisha zahanati hizi ili wananchi hao waweze kupata huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni barabara Gulwe – Mima - Chitope. Wakati Waziri anajibu swalii Bungeni aliniahidhi kwamba atanitengea shilingi bilioni moja na milioni mia sita ili barabara ya Gulwe – Berege – Chitemo – Mima - Chitope iweze kufanyiwa matengenezo makubwa. Kwa hiyo, naomba katika bajeti hii utenge fedha za kutosha, pamoja na barabara ya Mtanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tuko Mima na Mheshimiwa Waziri nilimueleza kwamba siku moja atembelee Mkanana, barabara ile ni mbaya sana, kwanza ina mawe mengi halafu ni mlimani. Wananchi wa Mkanana wana matatizo mengi sana. Kwanza wako mlimani, kutoka Mkanana mpaka makao makuu ya kata ni kilometra 30. Kwa hiyo, walikuwa wanaomba angalau nao wapate kata yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni Daraja la Mpwapwa pale Miembeni ambalo liliisombwa na maji hivi karibuni. Daraja hili Mheshimiwa Waziri analifahamu vizuri sana. Naomba achukue hatua za haraka, hata kama wakati huu mvua zinanyesha hawezি akajenga madaraja lakini naomba hata *Bailey bridge* ili wananchi wa Mpwapwa Mjini waweze kupata huduma za usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa William Tate Olenasha, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji ajiandae.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa dakika zako tano ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo hapa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kidogo kuhusu Janga la *Corona*. Kama wengi walivyochangia janga hili kwa kweli ni kubwa kwenye Taifa letu na hatua nyingi zimechukuliwa. Napenda tu na mimi niongeze sauti yangu kwenye maeneo ambayo naona ni muhimu Serikali ikayaangalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba *international flights* zimesimamishwa, ni jambo jema, lakini mimi napendekeza pia kwamba mipaka yetu iruhusu tu labda mizigo na Watanzania ambao wanarudi nichini na hao wanaorudi wawekwe karantini kwa siku 14 kwa ajili ya

kuangaliwa afya zao kabla hawajaweza kuingia katika maeneo yao wanayoishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna *private sector*; shule binafsi na maeneo mengine ambapo wamepeleka wafanyakazi likizo bila malipo. Napenda kujua Serikali ina mpango gani kwa ajili ya haya makusanyo ya *NSSF* na *Pay As You Earn* kwa hawa watu ambao kwa sasa hivi wako nje ya ajira kwa sababu ya *Corona*. Je, Serikali ina mpango gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nafikiria tungehitaji kufanya *projection* kama nchi kuangalia makundi na kupima hivi katika watu 500 waliopimwa watu wangapi ambao wameonesha dalili za *Corona*. Tukafanya kwa makundimakundi na kuweza kufanya *projection* ya kutusaidia kupanga mikakati ya kutuepusha na hili janga la *Corona*. Kwa hiyo, nafikiri ni muhimu sana kuweza ku-project idadi ambayo tunaweza tukapata. Tunaomba Mungu aepushilie mbali isiwe jambo kubwa, lakini ni vizuri kujitayarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimeona *breweries* wamesema watatengeneza *sanitizers* na tunawapongeza lakini nashauri pia viwanda vingine vyote ambavyo vinatumia *ethanol* kwenye *production* waweze kutumia hiyo *ethanol* kutengeneza *sanitizers* ambazo zita- *flood market* ziwe kwa bei nafuu, kila mtu aweze kuzinunua. Nina uhakika kama *sanitizer* itakuwa Sh.500 au Sh.1,000 watu wengi wataweza kununua *sanitizers* hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile *Corona* imeonekana sasa inaambukiza hata kwa hewa, kwa hiyo, hii ina maana kwamba tunahitaji kuvala *masks* na hazipatikani. Kwa hiyo, napendekeza, nilisikia kwenye redio wanasema watu watafundishwa jinsi ya kutengeneza *mask*. Ni jambo jema, watu wafundishwe kutengeneza *mask* kwa *materials* ambazo tutashauriwa na Wizara ya Afya na iwe ni *mandatory* kwa watu kuvala *mask* hasa kwenye maeneo ya watu wengi kama maeneo ya sokoni, hospitali, maeneo ya mabasi na

maeneo yote ambayo yanakuwa na msongamano wa watu kusudi kujaribu kupunguza maambukizi ya *Corona*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda nizungumzie suala la *bar*. Kwa nini Serikali iisipige marufuku watu kwenda *bar*? Maana kwenda kwenye vinywaji kwenye vijiwe kule nayo ni sehemu moja ambayo inaleta maambukizi. Watu wakanunue *drinks* zao, wakanywe nyumbani ili wasiweze kujikusanya mahali.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. RUTH H. MOLLEL: Zimeisha dakika tano? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa dakika tano ulizonipa. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ABDALLAH H. ULEGA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu ya kuweza kuandika mchango wangu huu kwenye mjadala wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Seleman S. Jafo kwa uwasilishaji wake wa hotuba ya Wizara hii. Pia niwapongeze Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii katika maeneo mawili; moja, napenda kuiomba Wizara izikubalie Halmashauri zetu nchini

kutekeleza miradi yao ya maendeleo kwa mapato ya ndani kutegemea na vipaumbele vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwongozo wa Sheria ya *Fedha* (*The Finance Act, 2019*), Halmashauri zinatakiwa kutumia 60% ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo (*development expenditure*) na 40% iliyobaki ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (*recurrent expenditure*).

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hii ya miradi ya maendeleo (60% ya mapato ya ndani) kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti hugawanywa katika kiasi kidogo kidogo kwenye miradi mingi ambapo matokeo ya miradi hiyo inakuwa haina mashiko, Sheria hii ya Bajeti inazuia Halmashauri kutekeleza miradi yao ya kipaumbele kwa kuwa kuna kiwango cha matumizi kinachotakiwa kwa kila Idara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ina miradi ya vipaumbele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kukamilisha maboma ya zahanati katika Vijiji vya Nyanduturu, Magodani, Mihekela, Kizomla, Dondwe, Mvulen, Kifumangao, Kisiju Pwani, Kisiwa cha Kwale na Mwanzega, pili, kujenga chuo cha Ufund Stadi na tatu, kufanya ukarabati mkubwa wa majengo na kujenga jengo la kisasa katika Hospitali ya Wilaya – Mkwalia

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo ya kipaumbele niliyotaja hapo juu inaweza kutekelezwa kwa mapato yetu ya ndani. Kwa mfano kiasi cha fedha shilingi bilioni tatu zikikusanywa zinaweza kugawanywa katika miradi hiyo mitatu na kwa wastani wa shilingi bilioni moja kila mradri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu wa kutumia mapato ya ndani kukamilisha miradi ya kipaumbele itasaidia kupunguza mzigo kwa Serikali Kuu kugharamia miradi katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuomba Waziri kwa mamlaka aliyopewa kisheria, kuibadilisha sheria hii ili Halmashauri ziweze kutumia fedha ya miradi ya maendeleo katika miradi mikubwa ya kipaumbele kama vile kujenga zahanati na vituo vya afya, vyuo vya ufundisti, barabara na madaraja, masoko ya kisasa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naielekeza kwenye malipo ya ushuru wa huduma (*service levy*) kutoka kwa wazalishaji bidhaa mbalimbali katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumuomba Mheshimiwa Waziri arejee barua niliyomwandikia tarehe 07/04/2020 yenye Kumbukumbu namba Kumb. Na. MB/MK/2020/012 yenye kichwa cha habari "MALIPO YA USHURU WA HUDUMA (SERVICE LEVY) ambapo niimeeleza masikitiko yangu juu ya wazalishaji katika Halmashauri ya Mkuranga ambao wanalipa ushuru wa huduma katika Manispaa za Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa ofisi zao za mauzo zipo huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ya Ushuru wa Huduma (*service levy*) inazinyima Halmashauri zetu chanzo halali cha mapato ya ndani ambayo yanetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia kwamba kwa kiasi fulani uzalishaji kama vile viwandani huambatana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira (*pollution*) ambao una athari kwa wakazi wa maeneo hayo, hivyo basi ni busara kwa Wizara kuamua ulipaji wa ushuru wa huduma ukafanywa katika eneo (Halmashauri) husika ili kupunguza machungu ya athari hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mkuranga ina viwanda vipatavyo 86 ambavyo vingi hulipa ushuru wa huduma katika Manispaa za Jiji la Dar es Salaam hali inayopelekea Halmashauri ya Mkuranga kukosa zaidi ya shilingi bilioni 2.2 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama niliviotangulia kueleza, endapo Halmashauri husika itapata ushuru huu, itasaldia kuanzisha miradi ya maendeleo yenye tija kwa kuwa maeneo ya vijijini kama Halmashauri ya Mkuranga yana changamoto kubwa za huduma za jamii kama afya, elimu, maji, nishati ya umeme, miundombinu ya barabara na madaraja kuliko maeneo ya Majiji na Manispaa ambako ushuru huu unalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri atazipa uzito hoja zangu hizi kwa maslahi mapana ya ustawi wa Halmashauri zetu kwa kuwa Wizara hii ni muhimili wa ustawi wa jamii zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Ahsante sana.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja ya bajeti ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Jafo wa Wizara ya TAMISEMI kwa kazi nzuri aliyofanya katika vipindi vyote vya utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Serikali kwa kudhamiria kutekeleza ujenzi wa zahanati tatu kwa kila jimbo ili kuhakikisha wanasogezza huduma ya afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kudhamiria kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya elimu kwa kujenga maabara saba za sayansi katika kila jimbo Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu John Pombe Magufuli kwa kazi aliyofanya katika kipindi cha muda wa miaka mitano na kukuza uchumi, kuboresha barabara zetu, bandari, viwanja vya ndege, ununuzi wa ndege, ujenzi wa mradi mkubwa wa

Nyerere Hydro Power, ujenzi wa barabara ya reli ya kisasa, ujenzi wa vituo vya afya katika majimbo yote Tanzania.

Pia uwepo wa huduma za afya zimeboreka na usambazaji umeme vijjini. Mazuri yote yaliyofanyika yameleta tija kwa wananchi, lakini yamekuza ajira nchini, yamekuza uchumi nchini, kuongeza mapato ya Serikali. Ni jithada kubwa zimefanyika kwa kipindi kifupi. Nimtakie Rais kheri na kuungwa mkono na Watanzania wote katika kipindi hiki cha uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kusaidia yafuatayo; kituo cha afya Kata Mnazimmoja, Lindi Manipaa, wananchi wa kata tano wanatumia kituo hiki jumla yao ni wananchi 26,164 wanaopata huduma. Katika kituo hakuna vifaa vya upasuaji, vifaa vya huduma ya meno (*dental chair*) na vifaa vingine. Aldha, kituo kina madaktari wa kutosha. Ninaiomba Serikali kusimamia maombi haya ili wananchi waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

MHE. ANGELAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa pongozi zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na uongozi mzima kwa kazi nzuri mnayoifanya pamoja na hotuba nzuri inayoelezea mafanikio yaliyopatikana na mwelekeo wa mwaka 2020/2021.

Pamoja na haya, napenda kushauri yafuatayo; kwanza barabara za vijjini zijengwe na kukarabatiwa mara kwa mara. Ni muhimu pia bajeti ya kutosha kwa ajili ya TARURA kuweza kutekeleza wajibu wao. Pili, ifanyike tathmini ya kina kuhusu mikopo inayotolewa na Halmashauri ili kujiridhisha endapo waliopewa mikopo hiyo walistahili au la, na endapo umetumia ipasavyo kwa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, ni vyema wanaoshughulikia mikopo hii ni muhimu maafisa biashara wahusika ili watumie pia taaluma zao katika utoaji wa mikopo hii. Vilevile ni vyema

ukaguzi ufanyike maana ziko Halmashauri nyingine pesa wanazo na mikopo haitolewi kwa wakati, fedha zimeshikiliwa tu.

Tatu, katika llani ya Uchaguzi ya 2015 - 2020 ilielekeza zabuni za Halmashauri 30% zitolewe kwa vijana na wanawake na Sheria ya Manunuzi kwa Umma nayo imeelekeza zabuni zielekezwe kwa wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu. Ni muhimu ifanyike ukaguzi wa utendaji (*perfomance audit*) ya takwa hili la kisheria na la llani yetu ya uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni muhimu Halmashauri zetu wapate mikataba ya utendaji, inayopimika na kutekelezeka.

Baada ya mchango huu, niutakie uongozi mzima wa TAMISEMI kazi njema na endeleeni kuimarisha usimamizi wa Serikali za Mitaa na naunga mkono hoja.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Wilaya ya Ulanga hana gari baada ya gari aliyokuwa anatumia kupata ajali. Kwa sasa anaazima gari la Ofisi ya Uratibu Elimu kwa muda sasa, hii inampa ugumu kufanya kazi kulingana na ukubwa na mazingira magumu ya miundombinu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, tuliahidiwa kupewa pesa za ujenzi Hospitali ya Wilaya lakini hata kwenye bajeti hii hakuna, majengo ni chakavu na eneo ni dogo hivyo Halmashauri imeshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya hivyo tunaomba pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pesa za vijana na akina mama, Halmashauri ya Ulanga ina deni kubwa la nyuma hivyo tunaomba msukumo wa Ofisi yako ili ilipwe na vijana wanufaikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba pesa kwa ajili ujenzi wa Kituo cha Afya Ruaha, tarafa hiyo ni kubwa, ina kata nne hivyo ina watu wengi sana, lakini huduma za afya

shida, hivyo mimi nikishirikiana na wananchi tumechangisha pesa, hivyo Serikali itoe pesa ili tuendelee na ujenzi.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Jafo. Ninaipongeza Wizara kwa kazi nzuri katika kutekeleza majukumu yake, niwapongeze kwa dhati watendaji wote wa Wizara hasa kwenye Halmashauri zetu kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi yafuatayo; kwanza Wilaya ya Kwimba ilisahaulika katika ugawaji ya pesa za ukamilishaji wa ujenzi wa maboma ambapo katika mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Kwimba pekee ilisahaulika, nilileta maombi ya maboma 21.

Pili, kutokana na uamuzi wa Serikali wenyewe busara wa kuwapelekea pesa nyingi za miradi, naomba kuleta maombi ya kukuomba Bwana Waziri utupatie watalaaam wa uhandisi wa ujenzi ambapo kwa sasa Kwimba hatuna Mhandisi wa Ujenzi jambo ambalo ni hatari katika usimamizi wa miradi mikubwa ya ujenzi, kwa mafano, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, ujenzi wa Chuo cha VETA, ujenzi wa Vituo vya Afya, ujenzi wa tanki la maji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, hatuna Afisa Mipango wa Wilaya ambaye ni *competent*. Pia Mkoa wa Mwanza yapo mapengo (*gaps*) za wafanyakazi katika idara mbalimbali kwa mkoa wetu, maombi ya kuziba *gaps* za wafanyakazi katika idara mbalimbali mkoani Mwanza. Aidha, tunao upungufu mkubwa wa watendaji katika idara mbalimbali kama vile afya, elimu, maji, watendaji, *VEO's*, Maafisa Ugani, Ushirika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri sana zinazofanywa na Serikali nikuombe sana watendaji wako waje na utaratibu wa ukaguzi wa kila mradi unaotekeliza na Serikali kwa kushirikiana na wananchi tofauti na kusubiri kwenda kuwabomolea maboma ya misingi na maboma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwatakie kila lillojema katika utekelezaji wa yaliyoainishwa katika hotuba hii na niwatakie maandalizi mema ya sikukuu ya Pasaka na kwa wenzetu wa dini ya kiislamu niwatakie maandalizi ya mfungo wa Ramadhani.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanazozifanya kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania, Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa jinsi anavyoimudu vizuri Wizara hii, kwa kweli ni Waziri mchapakazi na ni mfano mzuri kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze Naibu Waziri wote Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Waitara kwa kufanya kazi vizuri sana, bila kuwasahau Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wote na watendaji wote wa TAMISEMI kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwalettea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana kwa kupewa Hospitali ya Wilaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Tulipewa shilingi bilioni 1.5 na tumeshakamilisha majengo yote saba katika Hospitali zote za Wilaya 67 mpya kwenye bajeti hii zimepewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi tatu kila moja kasoro *Njombe DC*, pengine mmechanganya na *Njombe TC* naona fedha zimeelekezwa huko, angalia kiambatanisho namba 10. Naomba kupewa ufanuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Njombe DC* tuna vituo vya afya vitano, kati ya hivyo tumepata fedha kwa ajili ya kituo cha afya kimoja jumla ya shilingi milioni 200; tunashukuru sana, bado vituo vinne navyo ni Lupembe, Sovi, Ikuna na Matembwe tunaomba navyo vipewe fedha za ukarabati na nyongeza za wodi, *theatres* na kadhalika, naomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo Ia Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe lina shule tatu zenyé kidato cha tano na sita katika shule za Lupembe, *Manyunyu Girls* na Itipingo Sekondari. Tunashukuru tumepata fedha kwa ajili ya mabweni mawili katika Shule ya Wasichana Manyunyu. Kuna changamoto ya ukosefu wa mabweni na madarasa katika shule zote tatu, naomba shule ya Lupembe na Itipingo zipewe fedha za ujenzi wa mabweni na madarasa. Wananchi wameanza ujenzi wa mabweni katika shule ya Itipingo limeshapauliwa, basi Serikali iunge mkono juhudhi za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira za watumishi wa afya na walimu wa shule za msingi; kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa afya nchini kutokana na ongezeko la zahanati, vituo vya afya na hospitali, pia kuna upungufu mkubwa wa walimu wa shule za msingi na masomo ya sayansi kwa shule za sekondari. Naomba Serikali iajiri watumishi wa kutosha wa afya na elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa pumzi na kuniwezesha kuchangia kwa maandishi. Aidha, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kazi kubwa ya kuliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa na mwisho lakini sio kwa umuhimu naomba kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa kwa umahiri mkubwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akishirikiana na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri huyu anayehusika na TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo ametutendea haki sisi Watanzania ikiwa ni pamoja na wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kwa mambo makuu yafuatayo:-

Kwanza, ujenzi wa Hospitali za Wilaya, vituo vya afya na zahanati nchi nzima. Namtumbo nayo imeguswa, imejengewa Hospitali ya Wilaya, vituo vya afya viwili na zahanati mpya 17 zilizo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Tunakushukuru sana na tunakuombea urudi tena kwa kishindo na Mheshimiwa Rais akuteue kuendelea na nafasi hiyo ili Wananaamtumbo waweze kujengewa zahanati katika vijiji 12 vilivybaki na vituo vya afya vingine vipyta vya kata za mbali za Magazini, Ligera na Mchomoro, pamoja na kupanua na kuboresha vituo vya afya vya Lusewa, Mputa na Mkongogulioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo naliomba tusaidiwe ni barabara na madaraja yanayounganisha Mji Mdogo wa Namtumbo ambapo ndio Makao Makuu ya Wilaya na maeneo ya kilimo pamoja na vijiji na kata. Barabara hizo ni pamoja na barabara ya Mageuzi - Ruvuma - Mbimbi - Libango - Minazini ambayo ina madaraja mawili makubwa ya Njiro na Libango. Wakati madaraja la Libango limefanyiwa usanifu na *BOQ* yake inaonesha itahitaji shilingi milioni 950, Daraja la Njiro bado halijasanifiwa. Barabara hii inaziunganisha Kata za Hanga hususan Vijiji vya Mageuzi, Mlilayoyo, Mawa na Ruvuma; Kata ya Luegu hususan Kijiji cha Mbimbi na Kata ya Namtumbo hususan Vijiji vya Libango na Minazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba uniruhusu nimuombe Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa TAMISEMI atusaidie kutatua changamoto hizo mbili nilizozifafanua za miundombinu ya afya na barabara za *TARURA* zinazotunganisha Wananaamtumbo na maeneo yetu ya kilimo pamoja na Makao Makuu ya Wilaya ya Namtumbo. Kazi hiyo ifanyike kabla ya Serikali ya awamu ya tano katika kipindi chake hiki cha kwanza hakijafikia tamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kutamka kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia 100 na naomba nawasilisha.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii na pongezi nyingi kwa watendaji wote wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu kubwa ni kwa nini pesa ya Kituo cha Afya Heru Juu, *Kasulu TC*, Mkoa wa Kigoma mwaka wa 2019/2020 hadi sasa haijapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuatilia hadi naonekana kichekesho, Waziri Jafo tumeongea zaidi ya mara tano, mara wanajua Hazina, mara ngoja kidogo, *what is this?* Serikali ni moja, nataka maelezo, wananchi 17,000 wakazi wa kata ya Heru Juu wanataka majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru kwa majibu wakati unahitimisha hoja hii. Ahsante.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kuniwezesha leo kuchangia hotuba hii. Ama nikushukuru wewe binafsi kwa namna unavyoliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kwa ufanisi wenye miundombinu ya kisasa, Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipekee naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John J. P. Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kutupeleka kwenye Tanzania yenye kipato cha katni na uchumi wa viwanda. Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu ili aendelee kutumikia katika kipindi kijacho.

Vilevile nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jafo na wasaidizi wake wote kwa utendaji uliotukuka katika Wizara hii. Hakika Mheshimiwa Jafo ni chaguo sahihi katika Wizara hii na ameitendea haki, yeye na wasaidizi wake Mheshimiwa Kandege na Mheshimiwa Waitara, wote kwa pamoja Mungu awabariki sana. Bila kuwasahau naomba kuwapongeza Makatibu wote wanao hudumu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kuzungumzia sekta ya *TARURA*, Serikali imefanya jambo kubwa sana la kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini ili kuimarisha miundombinu ya barabara zetu vijijini. Lakini wakala huu bado una matatizo makubwa yafuatayo:-

Kwanza, ni uhaba wa vitendea kazi kama magari pamoja na maofisi, pili, uhaba wa wataalam na watumishi kwa ujumla na tatu, rasilimali fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matatizo niliyoyaainisha hapo juu ninashauri yafuatayo; ajira ya watumishi zizingatie mahitaji halisi ya mahali au Halmashauri husika, kwa sasa uwiano katika watumishi hao hauko vizuri toka Halmashauri moja hadi nyingine. Pia Serikali ihakikishe inawapa watendaji vitendea kazi katika sekta hii na vitendea kazi hivyo pia vizingatie jiografia za Halmashauri zetu. Mfano Halmashauri ya Liwale yenye matatizo makubwa ya miundombinu ya barabara za vijijini, haina watumishi wa kutosha wa gari la idara hii.

Kwa kuwa mtandao wa barabara za *TARURA* ni mkubwa sana, ni vyema Serikali ikaona umuhimu wa kuwaongeza fedha na kupandisha toka 30% ifike walau 40%.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichangie kuhusu ujenzi wa majengo ya taasisi za umma na majengo ya Serikali. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameelekeza majengo haya yajengwe kwa *force account* na ili majengo haya yajengwe katika ubora unaotakiwa ni Serikali ni lazima iajiri wataalam wa kutosha kwenye Halmashauri zetu. Kwani tatizo kubwa linaloikabili Halmashauri nyingi nchini kwa sasa ni uhaba wa wataalam wa usimamizi wa majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa wataalam wengi walikwenda *TARURA* na nafasi zao hazijapata wa kuziba nafasi hizo. Mfano Halmashauri ya Liwale hadi leo hakuna mtaalam wa majengo, jambo linalosababisha majengo mengi kujengwa chini ya kiwango na kushindwa kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kuititia kwa Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa iliyofanywa ya kuboresha elimu nchini, kuanzia na ujenzi wa miundombinu ya majengo na vitendea kazi, kwani sasa watoto wanaokosa fursa za elimu wamepungua sana kama sio kuisha kabisa. Hii ikiwa sambamba na uboreshaji wa afya za Watanzania kwa ujenzi wa miundombinu mbalimbali za sekta ya afya ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi na bajeti kubwa za madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe mchango wangu kwa kuishukuru sana Serikali hasa kwenye bajeti hii kwa kutengewa fedha zaidi ya shilingi bilioni 1.9 ili ziende kuimarisha huduma za afya pamoja na elimu. Mimi kama mwakilishi wa Wanaliwale nachukua fursa hii kwa dhati ya moyo wangu kuishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Sambamba na hilo nikipongeze sana chama changu, Chama cha Mapinduzi kwa kuisimamia vyema Serikali yake na kuhakikisha ilani yake inatekelezwa vyema na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba kuiambia Serikali yangu kuwa Wilaya ya Liwale si mionganoni mwa Wilaya mpya, lakini Wilaya hii haijawahi kuwa na majengo yafuatayo; jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, jengo la Halmashauri ya Wilaya, jengo la Polisi la Wilaya, jengo la Mahakama ya Wilaya wala jengo la Hospitali ya Wilaya. Lakini hapa nishukuru mwaka huu tumetengewa fedha kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya. Hivyo basi naomba Serikali kuitupia jicho la ziada Wilaya hii kongwe na ya muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono kwa nguvu zote bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliyo nzuri na yenye mambo makubwa yanayonufaisha Taifa letu. Ninashukuru wananchi wa Hanang kwa ushirikiano mkubwa waliokuwa wanani pa muda wote nikiwa Mbunge wa Jimbo letu na Mungu awabariki.

Wananchi wamekuwa na mimi katika kuleta maendeleo na ujenzi wa uchumi pamoja kupokea huduma za jamii. Ahsanteni sana.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza Waziri Mheshimiwa Jafo pamoja na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini pia nimpongeze Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kazi kubwa ya kuwatumikia wanachi bila kuchoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia suala zima la afya, Serikali imejitahidi kujenga zahanati na vituo vya afya kote nchini, lakini kuna changamoto ya baadhi ya maeneo wananchi wamejenga vituo vya afya kwa nguvu zao na viro kwa hatua tofauti tofauti, hili limejitokeza katika Jimbo langu la Lushoto, wananchi wamejenga vituo vya afya viwili katika kata ya Gare na Kata ya Ngwelo na wananchi wamejenga vituo hivyo kwa adha wanayoipata kwa kufuata huduma ya afya zaidi ya kilometra 50 na ukizingatia Jimbo la Lushoto lina kituo cha afya kimoja tu, kwa hali hii wananchi wanapata mateso makubwa ya kufuata huduma za afya kwa umbali mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa adha hii wanayoendelea kuipata wananchi hawa niiombe Serikali yangu tukufu na sikuvi, itenye pesa kwa ajili ya kumalizia vituo vya afya hivi viwili ili wananchi waweze kupata huduma kwa karibu, kama wengine wanavyopata huduma hiyo. Pamoja na hayo pia wananchi wamejenga zahanati nydingi kwa nguvu zao na zimekamilika, lakini zahanati zile hazina vifaa tiba pamoja na watumishi. Kwa hiyo niiombe Serikali yangu tukufu itenye fedha za kutosha kwa ajili ya kupeleka vifaa tiba na watumishi ili wananchi wetu wapate huduma kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie suala la *TARURA*, chombo hiki kinafanya kazi nzuri mno na ukizingatia barabara za vijijini ndio zenye kutoa mazao mengi kutoka kwa wakulima, lakini leo kuna changamoto kubwa sana ya barabara zetu kutokupitika na kupelekea mazao ya

wananchi kuendelea kuharibika mashambani na wakulima hawa kuendelea kupata hasara kwa mazao ya kuoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali yangu iongeze fedha za *TARURA* iweze kufika asilimia 40 kuliko ilivyokuwa sasa na ndio maana unakuta barabara nyingi zimeharibika kwa mvua zinazoendelea kunyesha, lakini *TARURA* haina mafungu ya kutosha, wala hakuna hata mafungu ya dharura na hii imepelekea barabara ya kuanzia Mlola, Makanya, Milingano hadi Mashewa, barabara hii ni mwaka wa tano huu haijawahi kutengenezwa zaidi ya kufukia mashimo tu tena si zaidi ya kilometra sita, wakati barabara yote ina kilometra 57.7 na barabara hii ni ya kiuchumi ina wakulima wengi mno wanaolima mazao ya biashara, pamoja na barabara mbadala ya kuanzia Doch, Ngulwi hadi Mombo kilometra 16 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu sana kama unavyoju Lushoto ina barabara moja tu, kwa hiyo, barabara hii inapopata *breakdown* hakuna sehemu nyingine ya kupita, kama ilivyokuwa mwaka 2017 baada ya barabara kuzibwa na maporomoko, wananchi walikosa huduma zaidi ya wiki mbili pamoja na wananchi kupata hasara kubwa ya mazao pamoja na kukosa huduma zote muhimu. Niishauri Serikali yangu tukufu barabara hii ichukuliwe na *TANROADS* ili barabara hii itengenezwe ili iweze kupitika muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la elimu; kuna maboma mengi ya maabara yamejengwa kwa nguvu za wananchi na mpaka leo hayajakamilika pamoja na kujenga hosteli. Niishauri Serikali yangu itenye bajeti kubwa ili maabara zile ziweze kumaliziwa pamoja na kujenga hosteli hasa katika sekondari za Mlongwema, Malibwi, Gare, Kwai, Ubiri na Ngwelo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia hoja ya Waziri wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa utumishi uliotukuka kwa nchi hii. Lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa kuitendea haki nafasi hii ya Waziri kwa Wizara hii. Nawapongeza sana watumishi walio chini yake pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya awamu ya tano imefanya makubwa kwenye sekta ya afya. Serikali imejenga Hospitali za Wilaya 98, vituo vya afya 433 na zahanati 368 kwa nchi nzima. Naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Simiyu tunashukuru sana kwa kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Mkoa ambayo itatumika kama Hospitali ya Rufaa kwa Mkoa wetu. Lakini pia naishukuru sana Serikali kwa kutujengea Hospitali za Wilaya ya Busega, Itilima na *Bariadi DC* zilizogharimu jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 4.5.

Ninaishukuru Serikali pia kwa kutupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya akina mama na watoto katika Hospitali ya Mkoa kiasi cha shilingi bilioni 2.2 ambapo ujenzi unaendelea vizuri. Tunashukuru pia kwa kupewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.7 kwa ajili ya ujenzi wa maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sasa Serikali yangu iangalie suala la watumishi katika sekta hii. Kuna upungufu mkubwa wa watumishi kwa kada ya afya na hasa kwa Mkoa wetu wa Simiyu kwa ngazi zote yaani zahanati, vituo vya afya, hospitali za Wilaya na Mkoa. Naomba sana changamoto hii itatuliwe kwa nchi nzima hususani pia katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala llingine ni la umeme mbadala. Vituo vyetu vya afya na Hospitali zetu za Wilaya hazina jenereta ili kutumika wakati umeme unapokatika.

Naomba sana jambo hili lifanyiwe kazi ili kusaidia hasa umeme unapokatika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni la ubovu wa miundombinu ya barabara zinazohudumiwa na *TARURA* uliosababishwa na mvua kubwa mwaka huu. Naiomba Serikali yangu itenge fedha za dharura kupitia *TARURA* ili barabara zilizoharibika ziweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na naunga mkono hoja.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba ya Ofisi Rais, TAMISEMI kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu ujenzi wa vituo vya afya na zahanati. Nitashukuru sana Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Jemedari wetu Rais wa awamu ya tano Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutupatia vituo vya afya viwili vya Nikasage na Mchoteka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizi ninaomba kukumbushia ahadi ya Rais wa awamu ya nne ya mwaka 2014 ya kujenga kituo cha afya cha Nalasi ambapo kuna wakazi zaidi ya watu 30,000 katika kata mbili na Nalasi Mashariki na Nanalasi Magharibi. Mji huu upo umbali wa kilometra 70 kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Tunduru hivyo kituo hiki ni muhimu sana kwa manufaa ya wananchi wa Nalasi.

Vilevile ninakumbushia ahadi ya Mheshimiwa Rais wa awamu ya nne ya kutoa gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Mchoteka kilichopo umbali wa kilometra 80 kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Bahati nzuri kituo hiki kimeboreshwa na kinatoa huduma katika kata tano kutoka Tarafa ya Nalasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za ujenzi wa zahanati zilizotengwa hazikuzingatia ukubwa wa Halmashauri. Halmashauri zingine ni kubwa, zina majimbo zaidi ya moja

hivyo kutenga fedha kwa Halmashauri ni kuziumiza Halmashauri zile kubwa sana kama ilivyo Halmashauri ya Tunduru. Hivyo ninashauri mgao kuzingatia idadi ya majimbo badala ya Halmashauri na ikiwapendeza majimbo yote wapewe Halmashauri kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninaomba Kituo cha Afya Mtina iboreshwe kama cha Mchoteka na Nkasale.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa elimu napenda kutoa pongezi kwa Rais kwa kuendelea kutoa elimu bila malipo na kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya mabomba na miundombinu mingine ya shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni Serikali kuangalia ugawaji wa fedha za maabara, *EP4R*na majengo ya maboma yazingatia majimbo badala ya Halmashauri kwani Halmashauri zingine zina majimbo mawili na zina kata nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tunduru walihamasishwa kufyatua matofali 100,000 kila kijijiini, hivyo ninaiomba Serikali kutoa fedha kwa ajili ya kununua vifaa vyta viwandani kama vile mabati, saruji na misumari ili kuunga mkono nguvu hizi za wananchi zisipotee bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* iongezewe uwezo wa kifedha na rasilimali watu pamoja na magari ili kuwawezesha kufanya kazi zao vizuri. Kuna barabara ya Chemuchemu - Ligoma haijawahi kupata matengenezo ya kawaida zaidi ya miaka 10, barabara ya Mchesi - Mrusha - Njia Panda ya Semeni - Mchesi - Chikomo - Njia Panda ya Mbasa pamoja na barabara ya Marumba - Masuguru - Mchoteka na Marumba Jenga - Mchoteka zina hali mbaya sana, zinahitaji matengenezo ya haraka sana kwani barabara hizi hazijawahi kutengenezwa zaidi ya miaka 10.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kwanza naanza kuunga mkono hoja sababu ziko nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutujengea Hospitali ya Wilaya Nyang'hwale, kutoa fedha ya upanuzi wa Kituo cha Afya shilingi milioni 700 Kharumwa na shilingi milioni 400 Kituo cha Afya Nyang'hwale ambazo ziliporwa zote. Zilitolewa shilingi milioni 500 ujenzi wa mabweni na hosteli kwenye shule za sekondari Msalala na Nyang'hwale. Fedha za kukamilisha vyumba nya madarasa na vyumba za walimu na fedha za matengenezo ya barabara na maeneo mengi tu, napenda kuomba fedha ya Kituo cha Afya Nyang'hwale shilingi milioni 400 zilizoporwa zilejeshwe. Pia mipango yote ya Serikali ya mwaka 2020/2021 naiunga mkono kwa asilimia 100. Pia nakumbushia fedha shilingi milioni 287 za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya za Backaa ili tuendee na ujenzi.

Naomba kukumbushia ahadi ya Mheshimwa Rais wa awamu ya nne na Mheshimwa Rais wa awamu ya tano Mheshimwa John Pombe Magufuli, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Kahama, Nyang'horongo, Bukwimba,Kharumwa, Nyijundu, Busolwa, Ngoma, Busisi Ferry.

Mheshimwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Wabunge wenzangu wengine waliompongeza Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutuongoza vizuri wananchi wake na kuletea maendeleo makubwa ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati thabiti ya kuwezesha Taifa letu kuingia katika uchumi wa kati, uchumi wa viwanda na hivyo kupiga hatua kubwa ya kutoka kwenye umasikini. Kwa haya yote anayoyafanya Rais, ni busara kumpa tena nafasi ya kuliongoza Taifa hili kuwa ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu baadae mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Selemani Said Jafo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hotuba yake nzuri alioitoa hapa Bungeni akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa

mwaka wa fedha 2020/2021. Hotuba hiyo imegusia maeneo muhimu mengi naomba nizungumzie machache yafuatayo:-

Mheshimwa Naibu Spika, kwanza ni ujenzi wa hospitali, vituo vya afya na zahanati. Serikali imefanya kazi kubwa katika kuongeza idadi katika kipindi cha miaka minne iliyopita. Naipongeza sana Serikali yetu kwa kufanikisha hili. Jimbo langu la Morogoro Kusini tumenufaika kupatiwa Hospitali ya Wilaya Mvuha, Vituo vya Afya vya Duthumi, Kisemu na Kisaki ambacho fedha zake za ujenzi zimekuja baadae na sasa tumeelezwa Serikali itaziongezea kila Halmashauri zahanati tatu, ni jambo jema sana.

Mheshimwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuangalia pia majengo ya zahanati za vijiji ambavyo wananchi wallitikia wito wa Serikali wa kujijengea zahanati kila kijiji na sasa yamesimama kabisa ujenzi wake kutohana na Halmashauri na wananchi kushindwa kumalizia. Gharama za kumalizia ujenzi kwa zahanati hizi zinatofautiana kati ya shilingi milioni 10 hadi milioni 20. Serikali iandae mkakati wa kukamilisha majengo hayo kwa kushirikiana na Halmashauri zetu ili wananchi vijijini waweze kupata huduma hizi karibu zaidi na wanapoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Morogoro (*MDC*) ni kati ya Halmashauri chache nchini zenyе majimbo zaidi ya moja. Tuna Jimbo la Morogoro Kusini na Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki. Yapo matatizo mengi yanajitokeza kwenye mfumo huu. Kugawana mapato ya Serikali sawa kwa sasa sio rahisi. Kugawana rasilimali nyingine na fursa zinazojitekeza sawa kwa sawa ni shida. Mfano, Halmashauri umepewa nafasi ya kuchagua vijiji saba vipatiwe umeme. Wananchi wa majimbo haya mawili yaliyomo ndani ya Wilaya na Halmashauri ya Morogoro wangenufaika zaidi kama kila jimbo lingekuwa na Halmashauri yake. Tuondokane na malalamiko ya upendeleo wa kugawana rasilimali. Kugawana zahanati tatu zinazoongezwa na Serikali kwenye Halmashauri yangu yenye majimbo mawili ni mtihani wa nani apate zahanati mbili na nani apate moja na maelezo yapi tunatoka kwa wananchi wanapata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuendeleza ujenzi wa barabara na matengenezo yake katika Halmashauri zetu. Hata hivyo bado maeneo mengi muhimu ya kilimo kwenye Jimbo la Morogoro Kusini barabara zake ni mbovu sana zinahitaji matengenezo. Uwezo wa Halmashauri yetu kuhudumia ni mdogo na wananchi wameendelea kuteseka. Barabara kutoka Kilengezi kwenda Kongwa, barabara kutoka Kangazi kwenda Mtombozi, barabara kutoka Mtombozi kwenda Lugeni na Mtombozi kwenda Tandale, ni baadhi tu ya barabara zilizokuwepo lakini zimeharibiwa sana na mvua zilizonyesha na hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kuendeleza mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria. Nimesoma kwenye hotuba ya Waziri, Serikali imetoa mbao wa viuadudu vya lita 96,000 na kusambazwa katika mikoa yenye maambukizi ya malaria, Kagera, Mtwara, Dar es Salaam, Lindi, Geita na Kigoma. Nimekuwa najiuliza malaria iliyosamba jimboni kwangu Morogoro Kusini na malaria inaua, kwa vipi hatukupewa mgao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, ugonjwa wa malaria ni tishio. Nchi nzima tusambaze dawa hii ya viuadudu vya kibailoja. Tusifanye mgao wa kuziacha sehemu nyingine ambazo zitafanya kuwa mazalia ya mbu na baadae nazo zitaibuka kuwa na maambukizi makubwa. Serikali itengeneze mpango mkakati wa kusambaza dawa hii kila Mkoa, kila Wilaya, kila kijiji nchi nzima. Kiwanda chetu cha kutengeneza viuadudu vya kibailoja kilichomo Kibaha ni kiwanda cha kisasa kabisa kina uwezo mkubwa wa kutengeneza dawa hizo na kumaliza kabisa tatizo la malaria hapa nchini na nje ya nchi. Ni teknolojia kutoka nchi ya Cuba ambao wao waliitumia teknolojia hiyo kumaliza tatizo la malaria nchini mwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amezungumzia pia mipango yao katika kukabiliana na homa ya mapato inayosababishwa na virusi vya Corona yaani COVID-19. Mipango hiyo ni kutenga vituo 182 vya kuwatenga washukiwa

(isolation centers) na kutambua hoteli zitakazohifadhi wageni wanapoingia nchini. Ushauri wangu, kuna haja ya TAMISEMI kuangalia Mikoa, Wilaya na Halmashauri zitaathirika kwa kiwango gani, hatua zipi zichukuliwe kusaidia kurudisha uwezo utakaopotea, mapato yao yataathirika, biashara nydingi za watu zimeathirika, uchumi kiujumla utakuwa umeathirika hivyo hatua za kusaidia kurudisha tena shughuli za uchumi ni vema zibainishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika kuona juhudzi za Serikali katika kuwapa elimu Maafisa Ustawi wa Jamii. Imeelezwa kwenye hotuba ya Waziri kwamba Maafisa Ustawi wa Jamii 711 wamejengewa uwezo wa namna ya kushughulikia mashauri ya watoto wanaokinzana na sheria na waliofanyiwa vitendo vya kikatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshazungumzia Bungeni humu masuala ya watoto wanavyofanyiwa ukatili, watoto waliotelekezwa na wazazi wao ambao wanakwepa wajibu wao wa kuwatunza na kuwalea watoto wao, watoto wanatangatanga barabarani, wamekuwa ombaomba, wanalala mitaani, lakini wapo Maafisa Ustawi wa Jamii ambao wakitaka watamaliza matatizo haya ya watoto. Niwaombe waige utendaji kazi wa askari wetu wa usalama barabarani, wafanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri TAMISEMI yafuatayo; kuanzia baada ya Uchaguzi Mkuu ujao kwa Madiwani wapya; Halmashauri zisiruhusiwe kumdhaminii Diwani ye yeyote kukopa benki. Hivi sasa mikopo ni mingi kuititia *SACCOS* na kadhalika, haihitaji mzigo wa dhamana kwa mkopo binafsi kuwa unaratibiwa na Serikali.

Pili, punguzeni idadi ya vikao kwa mfano kwa nini Kamati za Fedha kukutana kila mwezi? Hili lina tija gani? Mabaraza yawe *semi annual*, Kamati ziwe *quarterly*. Pia Kamati ni nydingi mno zipungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI ilekeze idadi ya siku za Mabaraza kama siku mbili tu na si zaidi. Kamati iwe siku moja tu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI ifute mara moja kanuni ya kusema eti posho za Madiwani wanaweza wenyewe kujipangia. Hii ni hatari sana. TAMISEMI itoe agizo elekezi kuwa posho ziwe katika *structure* gani kwa Halmashauri kutegemeana na kipato cha Halmashauri husika.

Pia Waziri wa TAMISEMI awe na mamlaka ya kuidhinisha au kutoidhinisha posho zote za Madiwani kabla ya kuanza kutumika, iwe ni marufuku kupanga na kutekeleza bila Waziri kujua na kutoa ruhusa ili waoneshe uwezo wao wa kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *party caucus* je, nani anagharamia? Nashauri iwe kama Bungeni yaani Madiwani watacaa ndani ya siku ambazo ni za Kamati au Baraza iwe pasiwe na malipo ya ziada kupunguza gharama. Aidha posho ya mwezi ya Madiwani ni mshahara kwa kweli, itolewe na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa asilimia 10, 40 na kadhalika iwe na ufuatiliaji mkubwa. Baadhi ya Halmashauri wanaleta *data* za kupika hasa kwenye *definition* ya mapato ya ndani ni nini, wanachukua michango ya wananchi kujenga shule, zahanati na kadhalika wanaweka kama ndio hela walizorudisha wao kwenye maendeleo na kadhalika. Aidha, naomba kituo cha afya Kibaigwa na Songambele Wilayani Kongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote TAMISEMI. Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kusimamia dhidi ya mlipuko wa Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na pongezi. Awali naomba kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kazi nzuri sana. Endeleeni kusonga mbele, utekelezaji wa llani ni mzuri.

Kuhusu afya; naishukuru Serikali kwa kutujengea vituo viwili vya afya; Kerege na Matimbwa. Huu ni mchango mkubwa sana kuboresha huduma za afya katika Jimbo la Bagamoyo. Pia hii ni hazina katika maandalizi ya mapambano dhidi ya Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Kerege kinafanya kazi ila kina mapungufu ya watumishi, pia haina OPD. Kituo cha Afya Matimbwa kimekamilika sasa mwaka mzima lakini hakijaanza kutoa huduma. Tatizo ni ukosefu wa vifaa tiba, samani na watumishi. Namuomba Mheshimiwa Waziri Jafo atusaidie kupata vifaa tiba na watumishi ili Kituo cha Matimbwa kianze kufanya kazi.

Pia tunaomba Kituo cha Afya Fukayosi ili kiweze kutoa huduma katika Kata za Makurunge, Fukayosi na Kiwangwa ambazo hazina Kituo cha Afya. Kata hizi zina vijiji zaidi ya 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TARURA*, tunaishukuru Serikali kwa utekelezaji wa ahadi ya Rais ya ujenzi wa barabara za lami Bagamoyo kilometra tano. Barabara kilometra 0.62 imekamilika na kilometra 0.63 iko katika utekelezaji. Tunaomba Serikali itusaidie kukamilisha ujenzi wa barabara kilometra 3.75 zilizobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ina mtandao wa barabara takribani kilometra 440 ila hali ya barabara hizi ni mbaya sana hasa vipindi vya mvua za masika na vuli. Idadi kubwa ya barabara zetu hazipitiki

vipindi vya mvua. Wananchi wanapata shida sana wakati za mvua. Bajeti ya *TARURA* ni ndogo sana, haiwezi kukidhi mahitaji ya ujenzi mpya wa barabara na ukarabati unaohitajika. Serikali iiongezee *TARURA* bajeti hususan Serikali ifikirie kuiongezea *TARURA* mgao wa Mfuko wa Barabara walau uwe 50:50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu, tunaishukuru Serikali kwa ukarabati mkubwa wa shule ya sekondari Bagamoyo na shule kongwe nchi nzima, mamilioni ya shilingi yametumika. Tunaipongeza Serikali kwa kuongeza ufaulu wa kidato cha nne na sita kwa kiwango kikubwa. Sasa wakati umefika Serikali iongeze nafasi za elimu ya juu katika fani ya sayansi mfano udaktari, famasia, uuguzi, uhandisi na kadhalika, kwa sasa nafasi hazitoshi. Wanafunzi wanafaulu kwa madaraja ya juu lakini hawapati nafasi ya kusomea fani wanazotamani. Jambo hilli linawakatisha tamaa sana vijana wetu wenye ari ya kulitumikia Taifa letu. Nchi ya uchumi wa kati 2025 inahitaji wataalamu wengi wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi kwenye hoja ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kumpongeza Rais na watendaji wake wa Wizara hii chini ya uongozi wa Waziri Jafo na Naibu Mawaziri wake kwa kazi nzuri ya kutoa huduma bora za kiuchumi na kijamii na hivyo kuchangia katika juhudini za kuharakisha maendeleo ya wananchi na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naishukuru Serikali, Ofisi ya Rais kuititia TAMISEMI kwa miradi mikubwa na muhimu waliyotupa sisi Wanalongido kwenye sekta za afya, elimu, barabara, na kadhalika, ikiwepo ujenzi wa vituo viwili vya afya (Kata za Engarenaibor na Kimokouwa/Namanga) pamoja na Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kwa pamoja miradi hii mitatu imepatiwa jumla ya shilingi billioni 2.6 na utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 80 ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kazi zimesimama kwa sababu fedha zilizotengewa zimemalizika kabla ya miradi hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itenye fedha katika bajeti hii ya kukamilisha miradi hii mitatu muhimu inayosubiriwa kwa shauku kubwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Longido, tuna Tarafa moja kubwa ya Ketumbeine, yenye vijiji 19 vikubwa na zaidi wa wakazi 20,000 wanaoishi katika Kata sita kubwa na zilizo mbali na huduma za afya. Wananchi wa Tarafa hii wamejlongeza na kuanza ujenzi wa kituo chao cha afya hadi kukamilisha kitengo cha wagonjwa wa nje (*OPD*). Naiomba Serikali, kuitia TAMISEMI watoe pesa za kwenda kuendeleza ujenzi wa kituo hiki cha afya na kukimalizia kwa ukamilifu wake ili kiweze kuanza kuwahudumia wananchi ambao kwa sasa wanateseka sana na kuingia gharama kubwa katika kufuata huduma ya afya makao makuu ya Wilaya kwa kusafiri zaidi ya kilometra 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru kwa kupokea mchango wangu na ninaunga mkono hoja.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Waheshimiwa viongozi wa Taifa letu, Watanzania wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote. Hata hivyo tuendelee kumwombwa Mungu atuepushie janga hili la Corona katika nchi yetu na dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu mpandwa, Mheshimiwa Makamu wa rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, uongozi wa Bunge letu na waandamizi wengine

wote kwa jinsi walivyoiongoza nchi yetu mpaka leo, hakika nchi imepiga hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wachangiaji waliochangia maombi ya *TARURA* kutafutiwa vyanzo vya fedha vya uhakika, kwa sasa fedha wanazopata *TARURA* kwa mwaka kwa Halmashauri kama Mbulu Mji ni shilingi milioni 670 wakati daraja la Gunyoda linalounganisha halmashauri ya Mji wa Mbulu na Mbulu Vijijini linahitaji shilingi milioni 800. Hata hivyo Halmashauri zote mbili zinaendelea kuomba fedha za maombi maalum kwa miaka minne, lakini *TARURA* imeshindwa kwa kuwa bajeti yake imekuwa kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kutoa maombi ya miradi ya kimkakati hasa fedha za soko la Mbulu Mjini, *stand*'ya mabasi Halmaashauri ya Mbulu Mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi ya kuomba fedha za ukarabati/ujenzi wa jengo lilitokuwa la Halmashauri ya Wilaya Mbulu ili liwe jengo la utawala la Halmashauri ya Mji wa Mbulu.

Aidha, kwa kuwa Hospitali ya Mji wa Mbulu ina upungufu mkubwa sana wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendea kazi kwani kama maeneo mengine upatikanaji wa dawa ni kwa asilimia 93, hali kwa Hospitali ya Mbulu Mji ni mbaya. Naiomba sana TAMISEMI ichukue hatua ya kuongeza fedha kwani Hospitali ya Mbulu iko katikati kwa hiyo wananchi wa mipakani kutoka Karatu, Babati na Mbulu Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mbulu Mji ina upungufu mkubwa wa kada muhimu ya watumishi hususan afya, uhandisi, wanyama pori, ushirika, TEHAMA na kadhalika. Hali hii imetoka na mgao wa 40% kutoka Halmashauri mama ya Wilaya ya Mbulu ilipogawanyika, hivyo naomba katika ajira zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nampongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Selemani Said Jafo na

waandamizi wote wa Wizara kwa kazi nzuri, Mungu awajalie kudumu katika nafasi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa TAMISEMI, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, wewe binafsi Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia TAMISEMI imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa wa ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na miundombinu ya shule za msingi na sekondari na pia ukarabati wa barabara za vijijini. Jimbo la Mbeya Vijijini limenufaika kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na vituo vitatu vya afya (Ilembo, Santilya na Ikukwa). Pia kukamililika kwa shule ya sekondari ya Wasichana Galijembe na ufunguzi wa shule za sekondari za Sisyaka, lyela Inyala na Ilembo kwa kidato cha tano. Ujenzi huo umeweka historia ya kipekee katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya bado ina changamoto za kumalizia miundombinu ya zahanati na vituo vya afya vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi ikiwemo vituo vya afya kwa Kata ya Ilungu, Kata ya Isuto, Kata ya Bonde la Songwe na zahanati katika kila kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ina mtandao wa barabara wa zaidi ya kilometra 1,000 na karibu mtandao mzima hali ya barabara ni mbaya na hazipitiki krahisi hasa kipindi cha mvua. Barabara hizi ni llembو – Isono; Songwe Viwandani – Jojo; Mjele – Ikukwa; Kawetere – Ikukwa; Mbalizi – Ilota; Nyalwela – Ngole; Nyalwela, Mbonile – Itala na Irambo – Shamwengo. Kwa bajeti ndogo ambayo ni kilometra chini ya 100 kwa mwaka, ni vigumu kutatua changamoto za barabara hizi, kwa kiasi kikubwa zinabeba uchumi wa kilimo wa Mbeya na Tanzania kwa ujumla. Napendekeza bajeti ya ukarabati wa barabara iongezwe pamoja na mambo mengine itasaidia kuimarisha uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Mbeya kuna Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ambao una wakazi zaidi ya 100,000 na shughuli nyingi za kiuchumi ikiwemo viwanda, madini na hata Uwanja wa Ndege wa Songwe. Pia katika Kata ya Utengule Usongwe kuna Kijiji cha Mbalizi ambacho mipaka yake haviungani na vijiji vingine vyakata hiyo. Napendekeza Serikali ipandishe hadhi ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kuwa Halmashauri ya Mji na pia kurekebisha mipaka ya Kata ya Utengule Usongwe hasa Kijiji cha Mbalizi chenye wakazi zaidi ya 100,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa na zenye tija walizozifanya katika kipindi hiki. Hakika mmezikonga nyoyo za Watanzania na mmeturahisishia kazi Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara bado kuna haja ya kuwafanyia mafunzo watendaji hasa Wakurugenzi ili kuwakumbusha nidhamu za utumishi na mipaka ya majukumu yao. Mfano, suala la Mfuko wa Jimbo lipo kisheria lakini Mkurugenzi kwa sababu yeye ndio Afisa Maduhuli wa Halmashauri basi anamuingilia Mbunge na Kamati yake ya Mfuko wa Jimbo katika upangaji matumizi. Suala hili limenitokea mimi binafsi,

Mkurugenzi wa Temeke amekataza matumizi ya pesa za Mfuko wa Jimbo za mwaka 2019/2020 hadi leo licha ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo kufidia mgawanyo ambapo Mkurugenzi huwakilishwa na mchumi katika kikao hicho. Mambo ya aina hii yanamdhalilisha Mbunge kwa wananchi ambao aliahidi kuwasaidia kwa kuwa inaonekana muongo kwa kutekeleza ahadi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri kama kuna mapungufu katika Sheria ya Mfuko wa Jimbo basi yaainishwe kwa wote badala ya kuwaachia Wakurugenzi waambie utakavyo. Baadhi ya Wakurugenzi hawatutendei haki katika majimbo yetu kwa sababu tunazozifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchache naomba kuwasilisha.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la watumishi. Shida kubwa katika ofisi hii walimu kwa muda mrefu hawajapandishwa madaraja na wanadai malimbikizo ya madai yao kwa muda mrefu ikiwemo kutolipwa *stability* zao hasa pesa za likizo.

Kuhusu afya kada hii ina changamoto ya wafanyakazi wa afya na kupelekea ukosefu wa huduma ya afya katika zahanati zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora; kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za kiutendaji kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Mikoa kutengua Mameya wa Upinzani bila kufuata utaratibu na Wizara hii kukaa kimya.

Tunaomba sana Wizara hii pia iwe inarudisha mapato ya Halmashauri kwa wakati ili Wakurugenzi wafanye kazi.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na timu nzima ya Serikali. Pili, pongezi kwa Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji mzuri wa llani ya CCM 2015-2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Halmashauri zote zisimamiwe vema zaidi katika kubuni vyanzo nya mapato, wapelekewe wataalam pale inapobidi ili kuongeza mapato ya ndani (*own source*).

Kuhusu fedha zinazotolewa kwa ajili ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ziwekewe mfumo bora zaidi wa mipango na ufuatiliaji ili zisaidie kweli kukuza uchumi wa wanufaika na wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu mzima wa mpango wa *TASAF* upitiwe upya na mara kwa mara ili kuondoa kasoro na kuboresha kote nchini unakotekelawa. Serikali iangalie uwezekaji na tija ya kuwashirikisha mabalozi sambamba na watendaji wa Serikali katika ngazi ya chini kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano wa mgawanyo wa fedha za *RFB* kwa ajili ya ujenzi wa barabara upitiwe upya ili kuainisha urefu na aina ya barabara zinazohudumiwa au/ na kujengwa (lami, changarawe, udongo na kadhalika). Pia matengenezo ya barabara yaendane na msimu wa mvua ili kuepuka kupoteza fedha wakati wa ujenzi na/au muda mfupi baada ya barabara kukamilika kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itekeleze miradi ya ujenzi wa barabara ile tu inayoendana na uwezo wa kibajeti utakaozalisha barabara bora kuliko kuwa na mtawanyiko mkubwa wa fedha unaogusa barabara nyingi bila ufanisi.

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri na Manaibu Waziri TAMISEMI kwa kazi nzuri na kubwa zinazofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tumeshuhudia mvua nyingi na hasa mkoani Kagera. Barabara nyingi zimeharibika na hasa barabara inayotokeo Katerero kwenda Kanazi, Ibwera, Rubale hadi Ruhunga na ile inayotokea Ibwera kwenda Katoro kuzunguka hadi Ruhunga zilizo Bukoba

Vijijini. Mahali pengine barabara hazipitiki, watu wanavushwa kwa kubebwa mgongoni au kwa mitumbwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa Serikali ni kuwa *TARURA* wapewe fedha zaidi ili waweze kutengeneza barabara hizo hapo juu na kurudisha miundombinu ya barabara zote zilizoharibika nchi nzima.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi hoja ya Waziri wa TAMISEMI.

Nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Nchi, TAMISEMI kwa kazi nzuri anayofanya kwa kushirikiana na Naibu Mawaziri wake. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri ukiendelea hivi mtaifikisha mbali nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Magufuli kwa usimamizi uliotukuka katika utekelezaji wa mipango na miradi mbalimbali nchini. Nchi imebadilika hata tabia za Watanzania zimebadilika kuelekea maendeleo maana utamaduni wa kuchapa kazi unaeleweka kwa Watanzania karibu wote kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa naomba nitoe ushauri wangu kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kuhusu malipo ya walimu waliopanda madaraja. Kuna walimu ambao walipanda madaraja lakini hawakupata nyongeza za mishahara yao walipopanda madaraja. Mfano walimu waliopanda madaraja kuanzia tarehe 1 Juni, 2014 walirekebishiwa mishahara yao mwezi Novemba, 2014 na kuanza kulipwa tangu hapo kuendelea mbele bila kulipwa mapunjo yao kwa miezi ya Juni, Julai, Agosti, Septemba na Oktoba. Walimu hawa wameandika barua za kuomba kulipwa lakini mpaka sasa hawajalipwa. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri ashughulikie jambo hili ili walimu hawa wakiwamo wa Jimbo langu la Maswa Magharibi waweze kupata stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufuutiliaji na tathmini ya miradi; Serikali inapeleka fedha nyingi sana za miradi kwenye Wilaya na Mikoa. Ili kupata thamani ya fedha ya miradi na miradi hii iweze kugusa maisha ya watu wengi na kwa uendelevu zaidi, miradi hii lazima ifuatiliwe na kufanyiwa tathmini ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwanza, iwe inatenga kiasi cha fedha za kutosha kwa ajili ya ufuutiliaji na tathmini ya miradi inayotengewa fedha. Pili, Serikali iimarishe Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwenye Halmashauri kwa kukitengea fedha na rasilimali watu ili kitengo hiki kiweze kufanya kazi yake ipasavyo. Ikiwezekana kitengo hiki kiripoti kwa *Internal Auditor General* kwa masuala ya kiufundi na Halmashauri ibaki kushughulikia mambo ya utawala tu kwa kitengo hiki. Hii itatoa uhuru zaidi kwa Wakaguzi wa Ndani kufanya kazi zao kwa uhuru bila kuogopa Wakurugenzi ambao kwa upande mmoja ndio wanaowasimamia, lakini kwa upande wa pili, wakaguzi hawa wanawakagua Wakurugenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mungu kunipa afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu kwanza nashauri bajeti ya *TARURA* iongezwe.

Kuhusu maboma ya vituo vya afya na zahanati Serikali itenye fedha za kutosha kumalizia maboma hayo. Pia naishauri Serikali kwa vile vituo vya afya na zahanati ambavyo vimekamilika Serikali itenye bajeti ya kutosha ili kuweza kununua vifaa tiba vya kutosha na kuweka katika vituo hivyo.

Pia naishauri Serikali iajiri wauguzi na madaktari wa kutosha ili waweze kutoa huduma katika vituo vya afya na zahanati zote zilizokamilika.

Naishauri Serikali pindi mtumishi mfano mwalimu mara anapopandishwa daraja na mshahara wake uongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho fedha zinazoidhinishwa zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na afya; kwanza ujenzi uzingatie jiografia/mipaka ya Halmashauri. Tuangalie mtawanyo wa ukanda ndani ya Halmashauri ili kweli tupeleke huduma karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa Kondoa Mjini, tunayo Hospitali ya Mji ambayo ipo katikati ya mji ambapo kanda hiyo ina kata tatu za Kilimani, Chemchem na Kondoa Mjini yenye. Ukanda wa Kusini una kata tatu za Kingale, Suruke na Serya ambapo tumepata Kituo cha Afya kimoja kilichopo Kingale. Tunahitaji sasa Kituo cha Afya kingine kimoja kwa sasa kipelekwe ukanda wa Kaskazini wenye kata mbili za Kolo na Bolisa. Hii itawapunguzia sana umbali wa kufuata huduma kutoka ukanda huu kwenda mjini kati kwenye Hospitali ya Mji, Kondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu, kipaumbele kiwe ujenzi wa maabara. Kaulimbiu iwe "sekondari ni maabara". Huwezi kuakisi uchumi wa viwanda bila ya wanasayansi. Pia tutafute mkakati mahsus na wa msukumo kama ambavyo tumefanya kwenye ujenzi wa vituo vya afya 433 nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara mgawanyo wa bajeti ubadilishwe iwe 40% kwa 60% badala ya 30/70 ilivyo sasa. Mtando wa barabara za vijijini ndio mkubwa zaidi na unayo madaraja na makalavati mengi sana kutokana na uhalisia wa jiografia zetu. Huko ndio shughuli nyingi za kiuchumi na uzalishaji nchini zinafanyika. Sio zote zinapitika misimu yote ya mwaka. Watanzania walio wengi wanaishi vijijini. Serikali iliangularie hili vizuri zaidi.

Kuhusu uwezeshaji kiuchumi, Kamati ya mikopo (10% za mapato ya ndani ya Halmashauri - vijana, wanawake na walemauvu) imeondoa uwepo wa Mbunge. Hii sio sawa. Ukichukulia uwakilishi wa wananchi ambao ndio wanufaika mahsuswa wa mikopo hii, Mbunge ndiye mwenye maslahi mapana zaidi katika Jimbo/Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo na mchanganyiko wa Wajumbe wa Kamati ya Mikopo uzingatie uwakilishi wa wanufaika wakuu yaani vijana, wanawake na wenye ulemauvu. Uwakilishi huu unaweza kupatikana kuitia AZAKI au utaratibu mwingine utakaoonekana unafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa mikopo hii, uzingatie uwiano na mgawanyo wa kata, mitaa na vijiji katika Jimbo/Halmashauri husika. Tumeshuhudia ukosefu mkubwa sana wa uadiliifu unaofanya na wajumbe ambao ni watumishi wakishirikiana na Wenyeviti wa Halmashauri kuperendelea kata zao na za Madiwani ambao ni safu yake. Tukumbuke, Mwenyekiti wa Halmashauri yupo muda mwangi zaidi kule Jimboni/Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wenyeviti wa Mitaa; uandaliwe mpango/mkakati wapate semina kuwajengenge uwezo na uelewa wa majukumu yao. Wapewe nyaraka za miongozo ya rejea. Wengi ni wapya na uelewa ni bado mno.

NAIBU SPIKA: Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa William Tate Olenasha, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajindae.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Wizara hii nyeti. Naomba nianze kabisa kwa kusema kwamba naiunga mkono hoja iliyopo mezani kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni Wizara pacha na Wizara ya Elimu katika masuala

ya elimu kwa hiyo. Katika mambo mengi ambayo wanafanya, tunashirikiana kila siku. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jafo pamoja na Manaibu wake; Mheshimiwa Waitara na Mheshimiwa Kandege pamoja na Katibu Mkuu na Manaibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Wizara yao kwa ufanisi mkubwa katika shughuli zao za kawaida. Kwa kweli, wametusaidia sana katika Wizara ya Elimu kazi yetu iwe rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba hoja nyingi ambazo zinagusa Wizara yangu zimeibuliwa na Waheshimiwa Wabunge, hoja hizo tutazijibu kwa ufasaha zaidi wakati wa mjadala wa hotuba ya Wizara yetu. Kwa sasa naomba tu nitumie dakika hizi chache ambazo nimezipata kujibu au kutolea ufanuzi hoja mbili ambazo zimeibuka. Hoja ya kwanza kabisa ni ile iliyoibuliwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza kuhusiana na suala la udhibiti ubora ambao yeye alitoa hoja kwamba mwaka 2018/2019 udhibiti ubora haukufanyika ipasavyo kwa hiyo, iliathiri sana kiwango cha elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto zilizopo kwa rekodi tulizonazo katika Wizara ya Elimu inaonesha kwamba mwaka 2018/2019 tulipanga kufanya tathmini taasisi za elimu 11,000 na katika utekelezaji wake tumeweza kufikia taasisi 8,700 ambayo ni sawasawa na asilimia 77 ya lengo. Katika taasisi hizo tumeweza kufanya tathmini ya ubora wa elimu kwa Shule za Msingi 7,260 na shule 1,398 za sekondari ikiwa ni pamoja na vyuo 45 vya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na changamoto zilizopo, na tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja ya kuongeza zaidi kasi na kupanua wigo wa udhibiti ubora, kwa kweli, mwaka wa 2018/2019 tumejitahidi sana kwa sababu tumeweza kufiki lengo tulilojiwekea kwa asilimia 77.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, katika miaka ya hivi karibuni kati ya maeneo ambayo tumeweka nguvu kama Wizara ya Elimu,

kwa kweli ni suala la udhibiti ubora. Katika kipindi cha miaka minne tumefanikiwa kujenga ofisi mpya 100 kwenye Halmashauri mbalimbali ambazo zimegharimu zaidi ya shilingi bilioni 15. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge nyie ni mashahidi, mnaona majengo mapya mazuri ambayo yamejengwa, ni majengo ya wadhibiti ubora. Lengo ni kuwapatia mazingira mazuri ya kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kipindi hicho tumeweza kununua magari mapya 45 kwa ajili ya wadhibiti ubora na tuko mbioni kununua magari mengine 65. Hatukuishia hapo; kwa kutambua upungufu wa watendaji katika Ofisi za Wadhibiti Ubora katika Halmashauri zetu, hivi karibuni tumeajiri wadhibiti ubora wapya 400 na kuwasambaza nchi nzima. Lengo ni kuendelea kupanua wigo wa huduma hii ambayo kwa kweli ni muhimu sana kwa ajili ya kuboresha elimu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea sana kuhusu upungufu uliopo wa miundombinu ikiwa ni pamoja na miundombinu salama na rafiki kwa ajili ya watoto wa kike na hasa katika Shule za Sekondari. Hii inanikumbusha sana hoja ambayo imejengwa kwa nguvu sana na Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene kuhusiana na uhitaji wa Shule za Sekondari na hasa katika jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba hivi karibuni tumekubaliana na Benki ya Dunia kupata mkopo wa gharama nafuu wa shilingi trilioni 1.3, dola milioni 500, mkopo ambao nakuhakikisha utabadilisha sura ya elimu katika nchi yetu katika miaka mitano ijayo. Fedha hizi ambazo tunategemea kuanza kuzitumia kuanzia mwaka ujao wa fedha, inategemewa kutoa changamoto zilizopo na kufikia wanafunzi milioni 6.5 nchi nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya kazi ambayo mkopo huu utafanya ni pamoja na kujenga mazingira salama na rafiki kwa ajili ya watoto wa kike. Kwa hiyo, Shule za

Sekondari za Wasichana ni moja kati ya masuala ambayo mkopo huu utafanyia kazi. Kwa hiyo, naomba niwaondolee Waheshimiwa Wabunge wasiwasi, Serikali imechukua hatua na kwa kweli, huko tunakoenda miaka mitano tuko salama; watoto wetu wa kike watakuwa salama na miondombinu ya elimu kwa ujumla katika Shule za Sekondari itaongezwa kwa kiasi kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya machache, naomba tena niunge mkono hoja na kuwapongeza sana TAMISEMI kwa hotuba nzuri. Shukrani sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji dakika saba, atafuatiwa, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara dakika kumi na Mheshimiwa Josephat Kandege ajilandae.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Naomba nianze kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote; Manaibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo wamesema Waheshimiwa Wabunge wengi hii, ni Wizara inayoshughulika na wananchi na kiukweli kazi nzuri imefanyika, Watanzania wanaiona. Hongera sana Mheshimiwa Jafo kwa kazi njema ambayo umeifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika maeneo machache ambayo Waheshimiwa Wabunge wameeleza. La kwanza kabisa ni kutoka hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani walipotamka kwamba kuna shilingi 184,184,497,000/= ambazo hazijatolewa kwa ajili ya umalizaji wa maboma katika Sekta ya Afya na katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika bajeti ambayo tunaiheshimu sana ni bajeti ile ambayo tunakwenda kumalizia nguvu za wananchi zilizopoishia. Ndiyo maana kuanzia mwaka 2017/2018 bajeti yote tulioitenga tumekuwa tukiitoa kwa ajili ya maboma ya zahanati na kwa ajili ya maboma ya shule zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu huwa zinasema vizuri zaidi. Mwaka 2017/2018 tulipanga bajeti ya shilingi bilioni 38.9 na tulipomaliza mwaka huo tulikuwa tumezitoa shilingi bilioni 38.9 kwa ajili ya umalizaji wa maboma 96 ya Vituo vya Afya. Kwa hiyo, hii pia iwaeleze Waheshimiwa Wabunge wanaosema kwamba Serikali hajafanya jambo katika Sekta ya Afya, tumefanya makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vituo vinavyotajwa 433, hivi ni vipyta ambavyo kwanza vimekwenda kuanzishwa na Serikali yetu na vyote vimekamilika, vyote vinatoa huduma kwa wananchi. Pia pale ambapo wananchi wetu wameanzisha maboma, tumekuwa tukikamilisha mwaka hadi mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018/2019 tulitenga shilingi bilioni 29.9 kwa ajili ya kukamilisha maboma 2,392 ya madarasa ya shule zetu za sekondari. Tulipokamilisha bajeti hiyo mwaka huo, tayari tulishatoa fedha hizi zote, shilingi bilioni 29.9 kwenda kukamilisha maboma ya shule zetu za sekondari. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi, mnawatendea haki sana wananchi wetu, kusimama hapa kueleza ukweli. Mabadiliko ni makubwa na wananchi wetu wanayaona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kukiombea chama changu na viongozi wake wakuu, tutaishangaza dunia mwaka huu mwezi wa Kumi kwa ajili ya mengi mema yaliyotendwa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu wa 2019/2020 Bunge lako Tukufu lilipitisha shilingi bilioni 19.5 kwa ajili

ya kukamilisha maboma haya na tumeshatoa zote. Ninapoongea sasa hivi tulishapeleka zote shilingi bilioni 19.5 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya nyumba 364 za walimu wetu kwenye Shule za Msingi na maboma ya Zahanati zetu 52. Wote kila mmoja ambaye dhamira yake ni njema na ana hofu ya Mungu, nina uhakika analitambua hili kwenye jumbo lake alikotoka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwa mwaka ujao wa 2020/2021 Serikali yetu imetenga shilingi bilioni 228.15 na tuna uhakika tunakwenda kuzitoa zote kwa sababu, Serikali ya Magufuli ni Serikali ya wananchi. Wananchi walimwamini wananchi na sasa tunatenda kwa ajili ya wananchi wetu wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hiyo takwimu illyotajwa na Kambi Rasmi ya Upinzani, labda watusaidie ni wapi walikoitoa ili tuweze kujua ni kipi ambacho Serikali yetu ilipanga. Kwa sababu tunachokisema...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kuna taarifa. Mheshimiwa Halima Mdee.

TAARIFA

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, mbele yangu hapa nina Taarifa ya Serikali ama Maelezo ya Serikali kwenda kwenye Kamati ya Bajeti ambayo pamoja na mambo mengine kulikuwa kuna mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kutokana na maelekezo ama Maelezo ya Serikali baada ya kuihaji Serikali kutokupeleka fedha za maboma za kutosha. Sasa naomba hapa ninukuu kipengele kidogo tu cha mapendekezo ya Kamati ya Bajeti ili kumweka sawa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya Kamati ya Bajeti yanasema hivi: "Katika mwaka wa fedha 2017/2018

jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maboma zilikuwa shilingi bilioni 251. Kati ya fedha hizo Serikali ilitoa bilioni 67. Mwaka 2018/2019, (mwaka mmoja baadaye) Serikali ilitoa bilioni 19.8" (mwaka 2019/2020 ambao anazungumza). Kilichobaki ni shilingi bilioni 164." (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuna Taarifa ya Kamati ya Bajeti ambayo kikao cha Kamati ya Bajeti walikaa na Waziri wa Fedha, Waziri wa Fedha akakiri na Kamati ikamtaka hiyo shilingi bilioni 164 ahakikishe imetoka kabla ya mwaka huu wa fedha haujaisha. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Kwa kwasababu ulikuwa unatoa taarifa, kwahiyu, ameshaisikia. Ahsante sana.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nampa taarifa kwamba anachokizungumza hiyo shilingi bilioni 19, yes, ilishatoka. Shilingi bilioni 164 hamjatoa. Sasa ndito mtuambie... (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji unaipokea taarifa hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nilishawahi kusema ndani ya Bunge hili, ukiwa Mwanasheria *deal* na mambo ya kisheria. Ukiwa mchumi shughulika na mambo ya kiuchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka huu tunaotekeleza sasa, nenda kwenye vitabu vyote vya bajeti vilivypitishwa ni shilingi bilioni 19.5 na pesa tuliyotoa kama Serikali ni shilingi bilioni 19.5 kwa sababu, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni Serikali ya wananchi. Sasa hizo shilingi 164 tunaenda kuzitoa wapi? Sisi wachumi tunafahamu *what is a budget?* Maana ya bajeti ni nini? Tumepanga na uzuri tumeshatekeleza kwa asilimia 100 kwa ajili ya maboma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Watanzania wafahamu, sishangai. Ndiyo maana watu wanasimama

wanaanza kuimba kuhusu kuporomoka kwa mapato wakati tumetoka kukusanya mapato ya shilingi bilioni 800 kwa mwezi na sasa tunakusanya mapato shilingi trillioni 1.9. Hiyo ndiyo Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Miaka mitano ya kuwahudumia Watanzania, wanalifahamu hilo na sasa kilichobaki nimesema tusubiri Oktoba 25 haiko mbali, tutatambua nini maana ya Serikali inayowajali wananchi wake. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia na hoja moja maana naamini muda wangu umepungua. Imeongelewa taarifa...

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya muda, hii itakuwa taarifa ya mwisho. Mheshimiwa Catherine Ruge.

TAARIFA

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda nimpe Taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, mapato anayoyaongelea yameongezeka. Unafanya *comparison* ya mapato ya Serikali ya Awamu ya Nne na Serikali ya Awamu ya Tano, lakini unatakiwa ufanye *comparison* kati ya malengo na kiasi mlichokusanya, kiasi halisi. Pia ni lazima ufanye *trend*...

NAIBU SPIKA: Taarifa ni moja Mheshimiwa. Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji unaipokea Taarifa hiyo?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha inaongozwa na wachumi wawili makini. Wasuburi siku ya bajeti ya Wizara ya Fedha ili watambue nini wanasema na porojo zilizopigwa huko nje zote tutazijibu moja baada ya nyingine. *You can't compare two things that are not comparable. You can't do that.* Wasuburi siku inakuja, tutayasema yote ndani ya Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, tunafahamu barabara zetu zimeharibika kwa kiwango kikubwa na yametolewa mapendekezo mbalimbali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu, ipo Kamati ya Kitaifa ya kupanga hadhi za barabara ambayo inakamilisha kazi yake. tunapokamilisha tutajua nini kifanyike kati ya *TARURA* na *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutaona tunaisaidiaje *TANROADS* ili Watanzania tuweze kuwafikia na malengo mema ya Chama cha Mapinduzi na Serikali yake yaweze kufikiwa ya kuweza kuhakikisha kwamba mfumuko wa bei unaendelea kubaki katika *digit* moja nayo ni chini ya asilimia tano kama ambavyo tumeweza kufanya kazi katika kipindi chote cha miaka minne.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimia Mtoa Hoja utakuwa unajiandaa kwa ajili ya kuhitimisha.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. Yako mambo mengi sana ambayo yametolewa kama maoni na ushauri kwa Waheshimiwa Wabunge, hayo mengine tumeyapokea. Kwa hiyo, nitajaribu kupita kwenye baadhi ya maeneo ambayo naona ni muhimu niseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ilikuwepo hoja ya namna ambavyo fedha zinakusanya katika Halmashauri zetu na tumenunua *POS* mpya za kisasa 7,227 ambazo pamoja na mambo mengine zinatibu pia namna ambavyo ilikuwa fedha zinapotea. Zilikuwa zinaweza kutumiwa hata kupiga simu; sasa hivi tena haiwezekani. Kwa hiyo, hiyo *POS* kazi yake ni kukusanya fedha, hata ikizimwa unaweza ukafuatilia fedha zilipo na ukajua zinavyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelekeza kwamba mamlaka ya Serikali za Mitaa zote fedha za umma lazima zikusanywe kwa mfumo na fedha isitumike ikiwa mbichi, iingizwe kwenye mfumo na iweze kufanya kazi yake vizuri. Haya mambo natumaini kwamba yatazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo lilzungumzwa na Mheshimiwa Jafary Michael ambaye pia aliwahi kuwa Meya wa Moshi, nakumbuka vizuri, alitaka itolewe tathmini ya namna ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi imejipanga na namna ambavyo tunawezesha halmashauri zetu kufanya kazi ya kupeleka huduma kwa wananchi. Nitapitia baadhi ya maeneo machache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, miradi yote ambayo imeletwa kwenye Bunge tukufu ni miradi ambayo inapitishwa kwenye mchakato kuanzia ngazi ya Kitongoji mpaka halmashauri na kwenye Kamati ya Bunge TAMISEMI na Utawala inafika kwenye Bunge lako. Ni sehemu ya kwanza ya ushirikishwaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ni namna ambavyo uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulifanyika. Uchaguzi huu ulikuwa huru na haki na utaratibu wa uchaguzi huu sisi tumeshamaliza, jamvi lilitfungwa Mheshimiwa Jaffo. Kazi inayofanyika ni kubwa na utaona watu ambaao wanaleta hoja ya kulalamika hapa ni Wabunge, sasa sijui kama walitaka wawe Wenyelevi wa Mitaa, *at the same time* wawe Wabunge, sielewi! Huko mtaani, *site* hali ni shwari na wote wanafanya kazi yao kama kawaida ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kule *site* wale ambaao walikuwa wanagombea, wenye nafasi zao, wanatoa ushirikiano wa kutosha katika shughuli mbalimbali, hakuna malalamiko. Kwa hiyo niwaombe tu kwamba tusipoteze muda, huu ni mwaka wa 2020 tunaenda kwenye Bunge na Madiwani, Serikali za Mitaa tumeshafunga mjadala wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini miradi iko ili kuoneshakwamba kazi inachapwa na kumekuwa na ubadilishaji mkubwa , kwa mfano, elimu msingi bila malipo ambayo wenzangu wamesimama hapa kuanza kubeza sana nawashangaa. Ukienda kwenye *site* kule, kwenye Halmashauri, Vijiji na vitongoji ukajaribu kuponda elimu msingi bila malipo, utapigwa mawe! Yaani wanafunzi wanaosoma kwa fursa hiyo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli, ni muhimu sana kwao. Wako watoto ambao walikuwa wanafanya kazi za ndani, siku hizi ma-bar maid hawapatikani, wanasoma. Watoto walioenda sekondari wakashindwa kulipiwa ada, Serikali ya Awamu ya Tano inalipa ada watoto wanasoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, msibeze vitu ambavyo wananchi kule wanavipokea. Zimetumika shilingi trillioni 1.01 kwa ajili ya msingi bila malipo lakini madarasa yamejengwa 19,808 ya sekondari na msingi, matundu ya vyoo 7,922, madawati zaidi ya milioni tano, hayo mambo machache nипитиshe tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunapozungumza hapa alisema kwamba kuna viongozi wa Serikali wamechaguliwa na wakajaribu kuondolewa bila kufuata utaratibu. Tunao viongozi wa halmashauri wanne, mmoja alikuwa wa hapa Dodoma Manispaa, alikuwa ni wa Chama Cha Mapinduzi, alikiuka taratibu akaondolewa, CCM hawalalamiki, Upinzani wanalamika! Wa pili ni Kondoaa, na ye ye pia ni wa Chama Cha Mapinduzi, aliondolewa baada ya ukiuka taratibu zile.

Wa tatu ni Iringa Mjini, Msigwa anasimama anatoa povu hapa. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kule aliyekuwa Meya wa Iringa amesimama amekabidhi ofisi kwa heshima kubwa. Yaani aliyeondolewa madarakani anakabidhi anashukuru na anaomba kutoa ushirikiano kwa Meya atakayeku ja kuongoza

Iringa, wewe unalalamika ambaye hukuwa na cheo kile.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es Salaam, Meya wa Jiji alishaondolewa kwa mujibu wa taratibu, amejificha huko anafanya mambo yake. Haya mambo ni mambo ambayo hakuna aliyeonewa. Hata leo, ukikiuka taratibu ukaondolewa, tunashughulika na wewe na kazi inaendelea. Tunataka watu wafuate taratibu za namna ya kuongoza halmashauri zetu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka niseme tu kwamba ni kweli mambo yanaweza yakazungumzwa sana, inafanyika siasa lakini kwa kweli hivi kwa mfano katika Mkoa wa Dodoma, tunatarajia kupata Mbunge wa Upinzani hapa? Watu wa Dodoma wanamshukuru Mheshimiwa Dkt. Magufulli, hizi barabara kwa mamia na maelfu zilizotajwa, stendi, barabara za lami na miradi mbalimbali hapa ina maana Makao Makuu ya nchi yapo Dodoma. Natarajia mwezi wa kumi mwaka huu watu wa Dodoma watampa shukurani Mheshimiwa Dkt. Magufuli na wagombea wa Chama chake, *ofcourse* zitarajii kuweka hapa. *(Makofi)*

Vilevile ukienda Tanga, nenda Tanga pale Mjini, barabara za lami, taa, watu wanakaa pembezoni mwa barabara wanasoma usiku. Tutarajie kuona Tanga lazima Mbunge atakuwa ni wa Chama Cha Mapinduzi, hakuna miujiza. Nenda Babati Mjini, nenda Mbeya Mji, nenda kila mahali, uchaguzi wa mwaka huu ndiyo tutapata mbivu mbichi, wananchi wanaenda kumpa shukurani Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kazi nzuri ambayo amefanya. Umeme wa REA, hivi kushusha bei kutoka shilingi 300,000 mpaka sijui elfu 67,000 kuku wawili na *change* inabaki, pia makofi kwa Dkt. Magufuli tafadhali, hakuna namna! *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Amen!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa

Naibu Spika, lakini unajua waswahili wanaasema ukitaka kujua mtu tabia yake mpe cheo na fedha. Hawa wapinzani hawa wameunda Baraza Kivuli hapa miliona hamkuliona? Wangepewa nchi Baraza lingekuwa lile, ile ndio sura yao halisi! Hawa wanazungumza kwamba wamechangia fedha kwenye miradi ya maendeleo waulize Wabunge wa Upinzani nani ametoa shilingi 100 akapeleka kwenye darasa, fedha Mfuko wa Jimbo mnaotambia hapa! Tukiziba huo mwanya pale hawana shilingi 100...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): ..Mbunge asijisifu ametoa fedha kwenye miradi ya maendeleo.

MBUNGE FULANI: Taarifa!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Hii ni fedha ya Serikali, kodi ya Watanzania, ni Serikali CCM wana roho nzuri sana na Magufuli ana roho nzuri. Ukiwaminya hawa, ukiwa-switch kidogo biashara imeisha! Hakuna mtu amechangia bati kwa fedha yake. Fedha ya Serikali, kodi ya Watanzania. Lakini jamaa hawa waulize leo, waulize upinzani...

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwita Waitara, subiri kidogo. Mheshimiwa Bungara naomba ukae. Taarifa ya mwisho nadhani ulikuwepo wakati nikisema. Muda umekwisha. Hatuna muda mrefu. Mheshimiwa Bungara naomba ukae. Naomba ukae Mheshimiwa Bungara. Mheshimiwa Waitara malizia. (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ulinde muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichosema ni kwamba hawa wangepewa nchi, Baraza la Mawaziri ambalo wameunda mashoga, marafiki, mashangazi, wajomba nchi ingekuwa hivi! Hii ndiyo hali halisi ya nchi ingefanana. (Vingelegele)

MHE. ESTER BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiwauliza hawa jamaa, ukiwauliza kama kweli unakusanya ruzuku na miaka mitano umeshindwa kujenga hata ofisi moja huwezi kuzungumza habari ya Magufuli...

MHE. ESTER BULAYA: Naomba aseme Wabunge sio hawa anavyo-*address* aseme Wabunge asiseme hawa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): ...ambaye amejenga lami kila mahali, amepela maji, amepeleka barabara, vituo vya afya, zahanati, nidhamu ya utumishi wa umma, maskini Watanzania wanasema nani kama Dkt. Magufuli? (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Hakuna!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, watu kama Dkt. Magufuli hawazaliwi kila siku, hawa wanaopinga watakuja kusoma vitabu vya historia kwamba aliwahi kuwepo Dkt. Magufuli kutoka Chato na yeye alifanya mambo makubwa katika Taifa hili tumuombee Mungu. Tarehe 25 mwezi wa Kumi Mheshimiwa Esther Bulaya kule Bunda mmepewa hospitali. Serikali ya CCM ina huruma sana, huyu kapewa hospitali ya Wilaya bilioni 1.5 asingepata

chini ya CCM! Ipongeze CCM na hiyo ndiyo habari ya Dkt. Magufuli, CCM hoyeee!

WABUNGE FULANI: Hoyeee!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):2020 hoyee!

WABUNGE FULANI: Hoyeee!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Nani kama Dkt. Magufuli?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu 2020 tunakutana Tarime Vijijini, piga kelele, ndiyo urudi hapa kutoka hapa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): ...Tarime Vijijini, iwe inanyesha mvua, liwe linapiga jua, iwe ni kiangazi, hapa tunarudi kutoka Tarime Vijijini, mtafute kazi ya kufanya! (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane kwanza. Mheshimiwa Mwita Waitara wakati unachangia, Waheshimiwa Wabunge tusikilizane! Mheshimiwa Esther Bulaya, wewe ni *Chief Whip* hapo mbele! *Chief Whip* mwenzio yule pale, hawa wenzio wana afadhali, wewe ni *Chief Whip* kwa hiyo, tulia maana wewe ndiyo unatakiwa utilize wenzio huko. Waheshimiwa Wabunge tusikilizane.

Wakati Mheshimiwa Mwita Waitara, nitaeleza mambo mawili. Wakati akichangia kuhusu mchango wa Mheshimiwa Peter Msigwa alisema ametoa povu, nadhani neno sahihi ni wakati akichangia sio wakati akitoa povu, kwa hiyo hayo maneno yataondoka kwenye Taarifa Rasmi ya Bunge. Sawa.

Sasa jambo la pili nataka kufafanua. Waheshimiwa Wabunge, tusiwe tuna, nilishawahi kusema tena huko nyuma, usichague maneno ya kusikiliza, sikiliza yote, Sikiliza yote, ukisikiliza moja itakupa wakati mgumu. Mheshimiwa Mwita Waitara, ametumia neno shoga akataja marafiki n.k kwa hiyo, katika tafsiri huwezi kuchukua neno moja ukaliokota halafu marafiki ukaliachach. Kwa hiyo, yanaongozana yote na hicho ni Kiswahili cha kawaida kabisa. (*Makof!*)

Kwa hiyo, maneno ametoa povu yameondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa hiyo, tunaendelea, Mheshimiwa Josephat Kandege, halafu mtoa hoja ajiandae.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa. Naomba kipekee nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya niweze kusimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shuhuda, Wizara yetu imepokea pongezi nyingi kutoka katika michango ya Waheshimiwa Wabunge karibu wote. Kipekee naomba nishukuru Kamati yetu ya Utawala na TAMISEMI, imekuwa ikitoa michango ya kujenga na sisi tunapokea lakini kama haitoshi pia tumekuwa tukipata michango mizuri kutoka LAAC, wamekuwa wakitoa michango ya kujenga na ndiyo maana TAMISEMI ya jana na kesho ina tofauti kwasababu ya michango mizuri ambayo imekuwa ikitolewa na waheshimiwa Wabunge. Lakini kama haitoshi, tumekuwa tukipata michango mizuri sana kutoka kwenye Kamati ndogo ya sheria, Kamati ya Sheria Ndogo. TAMISEMI ilivyokuwa wakati ule na leo ukilinganisha kuna utofauti mkubwa sana. Kwa ujumla, nawashukuru sana wote na Mungu azidi kuwabariki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naomba nimshukuru Dkt. Jasson Rweikiza Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI pamoja na Wajumbe wote. Wametoa ushauri, kwa sababu ya muda nitapitia baadhi ya michango ambayo imetolewa ambayo inahitaji ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hii hoja ambayo imeibuka na imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana kuhusiana na suala zima la *TARURA* juu ya uwezo wake wa kifedha na jinsi ambayo inaweza kuhudumia kilometa 108,000 na wengi wameomba kama ikiwezekana *formula* ibadilike, pia Mheshimiwa Jafary naYe amechangia akitaka ikiwezekana kuwe na maboresho ambayo yatatambua uwepo wa Waheshimiwa madiwani na mabaraza yao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia yuko Mheshimiwa Magdalena Sakaya amesema bajeti iongezwe. Mheshimiwa Haonga anataka *formula* ibadilike, ikiwezekana iwe 50 kwa 50. Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia anataka *TARURA* iongezewe uwezo wa kifedha, lakini kwa kutafuta vyanzo vingine nya fedha, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, bajeti iongezwe. Maftaha, Abdallah Nachuma bajeti iongezwe 50 kwa 50. Bupe Nelson Mwakang'ata anataka 50 wa 50, Mheshimiwa Maulid Said Abdallah Mtulia anataka 50 kwa 50, Ally Mohamed Keissy anataka *TARURA* iongezewe fedha lakini kwa kutafuta chanzo kingine. Mheshimiwa Justin Joseph Monko anataka barabara ambazo zinahudumiwa na *TARURA* ziongezewe fedha illi iweze kuhudumu vizuri zaidi. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, *TARURA* iongezewe kwa kutazama vyanzo vingine. Mheshimiwa Grace Victor Tendega anataka *TARURA* ongezewe bajeti, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava bajeti iongezwe, Mheshimiwa Cosato David Chumi anataka bajeti iongezewe, Mheshimiwa Hamid Hassan Bobali, bajeti iongezewe. Husna Sudi Mwilima, bajeti iongezewe na Mheshimiwa Kakoso na wengine hawa ambao wamemalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote tunakubaliana na kazi nzuri ambayo inafanywa na *TARURA* lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba Serikali inatambua kazi nzuri ambayo inafanywa lakini ni vizuri pia tutazame namna gani ya kuweza kuongea fedha bila kupunguza upande wa kutoka 30 kwa 70 kwa sababu kazi ambayo inafanywa na *TANROADS*ni kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuendelee kuvuta subira, Serikali inafanyia utaratibu wa *formula* ipi ambayo itakuwa *sustainable* kulikoni habari ya kwamba tunakwenda kupunguza kile kiasi ambacho kiko upande wa *TANROADS*. Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatoe wasiwasi, *TANROADS* Silipofikia hapo ni baada ya kujengwa kwa kupewa fedha ya kutosha, Serikali inahangaika kutafuta fedha tofauti na hiki ambacho kinaongelea na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba pia niwatoe wasiwasi na mtambue kwamba kuna vyano vingine ambavyo vinatumika ili kuhakikisha kwamba *TARURA* inakuwa na uwezo mkubwa zaidi ndiyo maana ukienda kama Dar es Salaam tuna ule mradi wa *DMDP*, una kiasi kingi sana cha fedha lakini pia tunakwenda kipeleka fedha nyingine katika mikoa ile ambayo inalima mazao kama maua ili tuwe na fedha nyingi. Kwa hiyo, ushauri ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge, sisi hatupuuzi ushauri hata mmoja, tunaenda kufanya kazi ili tuboreshe chombo chetu hiki *TARURA* na wengine, nchi nyingine waje kujifunza namna ya utendaji bora...

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Mheshimiwa Naibu Spika, unamsikia Waziri huyo? Sio mnatuletea lilevi hapa, chokochokochoko, Waziri mnamsikia anavyosema huyo? (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bungara, huruhusiwi kuzungumza kabla hujapewa fursa. Mheshimiwa Naibu Waziri...

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kuna hoja ambayo imetolewa na Kamati yetu ya Utawala na TAMISEMI kuhusiana na asilimia 10 ambayo inatakiwa ikusanywe na iende kuhudumia katika vikundi vya akinamama, watu wenye ulemavu na vijana. Katika mapendekezo ambayo ametoa na Waheshimiwa Wabunge wengi nao wamechangia, wengine wakitaka

tuhakikishe hicho kiasi cha fedha ambacho kinatolewa kinaenda kutolewa kwa vikundi vilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia itafutwe *formula* ambayo itaweza kukidhi haja kwa sababu ni ukweli usiopingika, ukienda kutafuta watu wenyewe uhitaji maalum kwa maana ya walemaru, ukitaka waende kuunda makundi ya kumi kwa kumi huwapati. Kwa hiyo, naomba niseme sisi tumepokea ushauri huu, tutazidi kuufanyia kazi ili tuje na *formula* itakayokuwa nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Bunge lako litakumbukwa ni namna ambavyo wamekuja na utaratibu katika fedha hizi ambazo ni makusanyo ya ndni, ni Bunge lako hili ndilo ambalo limepitisha sheria ikaanzishwa na imekuwa ikifanya kazi vizuri sana. Ukienda kule Mafinga mpaka kuna vikundi vinapewa millioni 70 na kazi ambazo zinafanyika ni nzuri. Ukienda Temeke kuna kikundi cha akinamama ambao wamewea kununua malori ya kusomba takataka kinafanya kaiz vizuri sana, ukienda Magu kule kuna kikundi kizuri sana cha akinamama ambacho kinafanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, waheshimiwa Wabunge ni wajibu wetu sisi kutoa hamasa na kuwaelimisha. Tumekuwa tukipata taabu kidogo kwenye kundi la vijana maana wengine wanakuwa wanadhani pesa hii inatolewa kwa ajili ya matumizi kwamba ukatumie hatarudi. Lakini, fedha hii ni *revolving fund* ambayo inatakiwa itumike na ndio maana katika michango ambayo waheshimiwa Wabunge wanasema kwamba fedha hii ni vizuri tukaifuatilia. Katika michango ambayo tumpata kwa maandishi ni pamoja na mchango wa Mheshimiwa Spika wetu nae amesema fedha hizi ni vizuri zikawekewa utaratibu mzuri na sisi tunaendelea kuboresha na miongozo inatoewa ili fedha hii wakatengeneze *millionaires* wengi wa Kitanzania ambao chimbuko lake kubwa ni Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la fedha kwa ajili ya kwenda kumalizia maboma. Imesemwa vizuri na

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na katika kuja kuhitimisha namba tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Serikali hii tukiahidi tunatekeleza na ninyi nyote ni mashuhuda. Ingekuwa ni sehemu ambayo tunapiga kelele tu hakuna vitendo waswahili wanasema vitendo vinaongea zaidi kuliko maneno. Serikali Awamu ya Tano inaongea kidogo, utendaji ni mwingi zaidi ninyi nyote ni mashuhuda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la ajira kwa ajili ya vituo vyetu nya afya ambavyo vimejengwa ili vikafanye kazi iliyokusudiwa. Sio vizuri mkawahisha kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa utwala atakuwa na bajeti ya kwake. Atakuja kusema lakini ninyi nyote ni mashuhuda, sisi ofisi ya Rais TAMISEMI tumeweza kutangaza nafasi 610 kwa ajili ya madaktari wetu lakini hali kadhalika ofisi ya afya nao wametangaza 290 katika zile nafasi 1,000 ambazo Mheshimiwa Rais baada ya kuwasikiliza madaktari juu ya uhitaji wa kuwa na madaktari akatoa nafasi 1,000. Hakuna ubaya kama sisi wote kwa pamoja tukampongeza Mheshimiwa Rais kwa kumpigia makofi kwa uamuzi wa kizalendo wa kuhakikisha kwamba haya maboma ambayo yanajengwa yanaenda kufanya kazi na kazi nyingine ni kuhudumia Watanzania, kupunguza umbali wa wananchi kwenda kufuata huduma ya afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la asilimia 20 ambazo zinatakiwa zirudi kwenye vijiji. Imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na hili ni takwa la kisheria. Katika mambo ambayo Bunge lako tukufu limepitisha ni kuhakikisha kwamba asilimia 20 inaenda kwenye vijiji ili ikaweze kusaidia maana Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiongelea juu ya suala zima la Waheshimiwa Wenyeviti wetu ambao tumewachagua wanasimamia miradi. Ni vizuri tuwahakikishie na ninaomba kutumia fursa hii kutoa maelekezo kwa wakurugenzi wote kuhakikisha kwamba asilimia 20 kwa mujibu wa sheria inatakiwa irudi ikafanye kazi kule kwenye Serikali za Mitaa na kwenye vijiji vyetu. Hakuna *excuse* yoyote ambayo inatakiwa itolewe na mkurugenzi awaye ye yeyote miongozo na maelekezo

yamekuwa yakitolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhakikisha kwamba pesa hizi zinakwenda na mkurugenzi awaye yeote miongozo na maelekezo yamekuwa yikitolewa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhakikisha kwamba pesa hizi zinakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa naamini Wabunge watapitisha bajeti hii tukafanye kazi, nakushukuru sana na Mungu awabariki. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nimuite sasa Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, mtoha hoja ahitimishe hoja yake. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema, lakini nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa fadhila zake nyingi sana. Mimi nikawa kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa sababu kipindi hiki tunaenda mwaka wa tano ameniamini kuendelea kudumu katika ofisi hii, binafsi naona amenipa imani kubwa sana kwa kuhakikisha namsaidia katika ofisi yake nikawa Waziri wa Nchi. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mapenzi yake makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Makamu wa Rais mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa malezi yake kama mama na kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Naomba nimshukuru kwa dhati kabisa kaka yangu, mkubwa wangu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa; hakika yeche amekuwa kiongozi wa aina yake nadhani kwa sababu ni Mwalimu. Naomba niwaambie inawezekana wenzetu hampati *flavor*, sisi Mawaziri tunaonja *flavorya* kuwa na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Amekuwa ni mtu ambaye kwa kweli kwa sisi Mawaziri ametusaidia sana na kwa kweli sisi wengine amekuwa ni *role model* wetu wa kujifunza kwake, Mungu amlipe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayofanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi mimi naomba kuishukuru sana Kamati yangu ya Utawala Bora na TAMISEMI ikiongozwa na mkubwa wetu Dkt. Rwekiza na mama yetu mama Mwanne Mcemba, mtu kutoka kwa Wanyamwezi kule. Kwa kweli Kamati hii niseme imefanya kazi kubwa sana kwa kipindi chote cha miaka hii, miaka minne tumemaliza sasa tunaenda mwaka wa tano huu, kwa kweli Kamati hii imefanya kazi ya mfano, binafsi najivunia kuhudumu katika Kamati hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati ya *LAAC* kwa kweli wajumbe hawa wote tukikutana katika Kamati na wanavyofanya kazi unaona kabisa kwamba Kamati hizi watu wamejipanga kwa ajili ya kuisaidia nchi. Kweli kazi yao huwa wakiwa katika Kamati hawajali mipaka yao ya vyama vyasiasa, kazi yao kubwa imekuwa ni kuelekeza na kuishauri Serikali na sisi tumekuwa watifulu sana kwa kadiri iwezekanavyo na tunawaomba radhi kama tuliwakwaza kwa jambo lolote, inawezekana haikuwa nia yetu lakini kwa kweli sisi; mimi na timu yangu hapa tunajivunia kuwa katika hizi mbili kwa kipindi chote. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuisahau Kamati ya Sheria Ndogo ambayo sheria zetu katika Halmashauri wao amefanya kazi kubwa za uchakataji wa Sheria Ndogo, kwa kweli tunajivunia kwa kiwango kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Manaibu wangu wapambanaji, Mheshimiwa Mwita Waitara na Mheshimiwa Kandege, hawa mabwana wenzangu wana miili mikubwa kuliko mimi lakini kwa kweli wamekuwa wakikimbizana muda wote, niwashukuru sana. Wakati mwingine mpaka usiku unampa mtu *assignment* anasema Mheshimiwa Waziri nimekuelewa na nimekusikia naenda *site*; kwa kweli Manaibu wangu nawashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Katibu Mkuu wangu pamoja na Manaibu Katibu Wakuu pamoja na viongozi wote Wakurugenzi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI na maafisa mbalimbali, kwa kweli kazi yao ni kubwa.

Niwashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri na mamlaka zote na watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sababu eneo hili lina jumla ya watumishi takribani asilimia 72.6 ya watumishi wa umma, kwa kweli nawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa leo kwa kweli naomba niseme, Spika wetu Mheshimiwa Job Ndugai ametusaidia sana katika mchakato huu wa miaka minne na wewe ukiwa unamsaidia na Wenyeviti. Kwa kweli sisi TAMISEMI tunajivunia sana lakini hali kadhalika niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili, maneno haya yote yanayopigwa humu, lakini niseme Wabunge wa Bunge hili wameiwezesha TAMISEMI kufanya kazi yake vizuri sana, nawashukuru Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuwasahau Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wetu wa Vijiji, Vitongoji pamoja na Mitaa, miaka hii mine kuna kazi kubwa imefanyika na nishukuru sana hata ukiangalia hapa katika hoja zilizochangiwa takribani Wabunge 85 wamechangia, kati yao 68 wamechangia kwa mujibu wa kuongea lakini 17 kwa mujibu wa maandishi. Hii inaonekana licha ya muda umekuwa mchache lakini hamu ya Wabunge kuchangia imekuwa kubwa na niwashukuru sana karibuni asilimia 99.999 wote wamekuwa *positive* katika Bajeti ya TAMISEMI, niwashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie yote sisi tumeyachukua, tunajua kwamba yaliyochukuliwa yote kila mtu alikuwa anatoa hisia zake za ndani. Lengo letu ni kuhakikisha mmekuwa na nia kwa ajili ya kuboresha kazi ya ofisi hii ya wananchi iweze kufanyika vizuri katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia ni wengi kwa kweli sitoweza kuwataja Wabunge wote waliochangia lakini maeneo ambayo yamechangiwa kwa kiwango kikubwa ni bajeti ya *TARURA* na bahati nzuri sana niwashukuru sana Manaibu wangu wametolea ufanuzi, ukarabati wa

miundombinu, suala zima la Sekta ya Elimu, utendaji wa kazi katika Mikoa na Wilaya, mikopo ya asilimia 10, upelekaji wa fedha za maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, usimamizi wa fedha za maendeleo, suala zima la ajira na mambo mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu watu wengi wamechangia hasa Kamati yetu ya Bunge imetoa mchango wa kutosha lakini nikiri wazi Spika wetu wa Bunge amechangia sana katika bajeti yetu hii. Kwa hakika naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Spika lakini na Wabunge kwa upana wote tumechangia kwa kiwango kikubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze tu hoja hizi kwa ujumla wake. Jambo la kwanza, kulikuwa na hoja hapa illizuka sana suala zima la mgao kwamba mgao unaonekana haupo rafiki, maeneo mengine yana Kata nyingi, lakini maeneo mengine Halmashauri moja ina Majimbo matatu na hasa tuliposema suala zima la zahanati kila Halmashauri, ina maana wengine wenye Majimbo matatu ukisema zahanati tatu kila Halmashauri tayari mgongano ulikuwa unajitokeza hapa jinsi gani Majimbo matatu katika Halmashauri moja mgao utafanyika vipi. Ndio maana naomba niseme kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni wasikivu, tumesikia kilio chenu, tumeenda kukifanyia *analysis* kuweka mgawanyo vizuri. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie hilo jambo tumelifanyia kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tuliangalia hata suala zima la Majimbo haya jinsi gani tufanye kila mtu apate huu mkate kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma. Tulifanya hivyo hivyo hali kadhalika katika suala zima la ujenzi wa maabara na maboma. Ajenda hiyo tumeifanyia kazi kwa nguvu nzuri na wewe ulichangia sana siku ile upo katika Kiti hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala ambalo Manaibu wangu wameshatoa ufanuzi ni suala zima la fedha za *TARURA*. Ni kweli mtandao wa barabara katika

TARURA ambazo zile zimeshakuwa registered tayari kilometra 108,000.9, changamoto ni kubwa, lakini niwashukuru sana Wabunge wote mmesema jinsi gani TARURA inafanya kazi. Tutaendelea kuwa watifiu kuhakikisha tunafanya kazi kwa weledi huu. Mgao ni mdogo lakini Serikali kwa umoja wetu tutaendelea kufanya kazi kwa kina na kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana hapa ofisi yangu inaendelea kufanya *resource mobilization* kutafuta vyanzo vingine mbalimbali, ndio maana ukiacha ule mpango na mpango mwengine ambao unaona kwamba kuititia Mfuko wa Barabara wanafanya tathmini ya suala zima la *formula* kuangalia nini kifanyike kwa ajili ya uboreshaji, lakini tumezidi kupanua *goal*, ndio maana mnaona kwamba hata katika maeneo ya miji hii tumeamua kutafuta fedha katika vyanzo vingine kwa ajili ya kuboresha miundombinu. Ndio maana katika Jiji la Dar es Salaam tumepata dola milioni 300 ambazo *it's equivalent to* bilioni 660 na kuongezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana leo Jiji la Dar es Salaam tumeamua kulibadilisha katika suala zima kuititia fedha zingine kutoka mifuko mingine. Pia ile Miji 18 ambayo unaona kwamba tumeifanyia kazi kubwa sana, tulipata dola takribani 255 na ile Miji mingine saba leo hii ndio maana ukizunguka Tanzania nzima katika Halmashauri za Miji, Majiji na Manispaa zetu zote ninyi ndio mashahidi mnatoka huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa ndugu yangu Mheshimiwa Jaffary pale tulienda kuzindua barabara pale za lami na Mama Samia Suluhu, haikubagua kila mahali unapokwenda. Ndio maana Mbunge wa Mpanda hapa amesema ukifika Mpanda unashangaa, ni kweli, kama kuna mtu wa Mpanda alitoka Mpanda mwaka 2012, kama alienda Ulaya amerudi leo hii ukimfikisha Mpanda pale hatoweza kuamini kama yupo Mpanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii imefanyika nchi nzima; hata kwa ndugu yangu Mheshimiwa Zitto Kabwe ukienda pale Ujiji, nenda kaangalie Serikali ya Awamu ya Tano

ilivyofanya Mapinduzi makubwa kutengeneza barabara za lami na taa za kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili halikuacha, maeneo yote ya Halmashauri na Manispaa hata kwa ndugu yangu Mheshimiwa Sugu ukienda pale Mbeya tumefanya vurugu za kufa mtu pale. Jiji la Mbeya tumejenga barabara nzuri kabisa za kisasa, hii ni kazi kubwa tumefanya *resource mobilization; package* hii tumetumia karibuni shilingi bilioni 884.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana ukiangalia katika mpango huu sasa miji hii kwa ujumla wake, katika mpango tunaoendelea nao sasa tumeamua kupanua goli, tunaenda katika Halmashauri zipatazo 45. Kuna watu wa Kasulu walikuwa hawajafikwa, Nzega na Handeni wote tunawaingiza katika kapu moja. Maana yake huko tunapokwenda tunaenda kufanya Mapinduzi makubwa ambayo watu watashangaa, nchi yetu inavyofanya kazi na kuibadilisha nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunajua fedha ndogo katika TARURA na Serikali imeliona jambo na tunaenda kufanya kazi kubwa, lakini niwaombe ndugu zangu Wabunge wakati mwengine tushukuru. Mungu anasema kwamba ukipewa shukuru na Mungu anasema kwamba mkishukuru nawaongezea, ni kanuni ya Mwenyezi Mungu; tumshukuru Mungu jamani. Sisi Wabunge humu tuna kila sababu ya kila mtu kujivunia Bunge hili Watanzania waliondoka Marekani na Asia mwaka 2014, leo wakifika Tanzania hii kila wanapopita wanashangaa. Ni kazi kubwa mmefanya ninyi Wabunge kwa hiyo tusiibeze hii kazi ambayo tumeifanya kwa mikono yetu ndani ya miaka minne na sasa hivi tunaenda mwaka wa tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Afya ninyi ndio mashahidi, siku zote mnazungumza. Tulipofika mwaka 2015 tulikuwa na vituo vya afya lakini vituo vilivyokuwa na uwezo wa kufanya huduma ya upasuaji vilikuwa vituo 115, leo hii ndani ya kipindi hiki, vituo takribani 430 na zaidi hivyo

vinaweza kufanya huduma ya upasuaji. Maana yake ukizungumza kituo cha afya sio ovyo ovyo, ni kituo chenye uwezo wa kufanya huduma ya upasuaji. Ndiyo maana hata kwa Mzee Lubeleje pale Mboli naomba nimwondoe shaka. Hata ndugu yangu Mchengerwa pale eneo la Rufiji ambapo kituo kimezama na maji, Serikali itakuja kufanya kazi pale. Serikali imefanya kazi kubwa, hii ni *transformation* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali za Wilaya tulikuwa na 77 za Serikali, leo ndani ya kipindi hiki zimeongezeka hospitali 98, *investment* kubwa hii, lazima Wabunge tushukuru kwanza kwa hii kazi iliyofanyika, ni *outstanding performance*. Sasa dada yangu Mheshimiwa Salome pale alivyozungumza nilikuwa namsikiliza lakini ukiangalia katika Manispaa ya Shinyanga pale tunajenga Hospitali ya Mkoa ya Rufaa na tumeanza jengo la *OPD*. Tumechukua ushauri, lengo letu ni kwamba tutaenda kuongeza huduma ya vituo vya afya katika maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo hata ndugu yangu wa Tunduma pale anafahamu, Mheshimiwa Mwakajoka. Hali ilikuwa mbaya pale, sasa hivi katika sehemu ambayo watu wana hospitali ya mfano pale Tunduma na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ameweka jiwe la msingi. Kituo chake cha afya pale Tunduma watu mpaka kutoka Zambia wanakuja pale kwa ndugu yangu kuja kupata huduma, hii ni kazi inaendelea kufanyika. Kwa hiyo ndugu zangu, kwanza kwa hatua tunayopiga, tuendelee kushukuru kwamba sisi tunaenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ajenda ya suala zima la madai ya Madiwani, tumeshatoa maelekezo katika Halmashauri zote mpaka tarehe 30 Mei na jambo hili naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge tunaenda kulisimamia. Madai yote tuhakikishe kwamba yanasmamiwa vizuri na sehemu hii Mheshimiwa Spika ametoa michango mingi sana na niseme kwamba ushauri wake wote tunauchukua kwa ajili ya kwenda kuufanya kazi kama Spika wa Bunge anayelijua Bunge vizuri na ile michango yake yote na

mchango wake wa maandishi tunaenda kuuchukua kwa ajili ya kuufanya kazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo mbalimbali kulikuwa ni hoja bahati nzuri Mheshimiwa Waitara amezungumza, hili suala la kwamba Mameya wameondoka na walitolewa na kwa sababu lazima sisi kama viongozi tuheshimu mabaraaza yanapokaa kule na kama kuna jambo la rufaa, basi iweze kutolewa. Hata Halmashauri ya Nyangh'wale ambayo inaongozwa na CCM iko kule Geita Mwenyekiti wake wakamwona kama hatoshi wakamuazimia, wakamtoa. Kwa hiyo, CCM tu Wenyevitii wa Halmashauri watatu, wametolewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuseme kwamba inawezekana huko kuna hapa na pale zinazoendelea lakini kubwa kwamba Baraza la Madlwani linapofanya maamuzi tunayapima kwanza. Bahati nzuri hata wa Iringa alivyotoka yule, nia yangu ni kusubirufaa, kama kuna mtu anataka kukata rufaa, baso akate, tunasikiliza kwa ajili ya kufanya kazi na watu wengine wajipime kuangalia nini kifanyike. Lengo letu tuweze kufanya kazi kwa ushirikiano, tulinde rasilimali zetu tulizokuwa nazo kwa ajili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ambayo ukizungumza suala la kibajeti, ukiangalia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, bajeti tuliyonayo katika bajeti ya maendeleo shilingi triliioni 1.6, leo tumefika triliioni mbili *point something*, hiyo inaonesha Serikali inavyoendelea kufanya kazi kwa kiwango kikubwa kuhakikisha kwamba inatatua matatizo mbalimbali ya wananchi. Naomba muamini kwamba ofisi hii lengo lake kubwa, ndio maana nimesema hii ni Wizara ya wananchi, lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba inaenda ku-*address* matatizo yote ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana leo hii Sekta ya Elimu Mheshimiwa Ole Nasha alizungumza hapa kidogo, lakini tuzungumze ukweli, leo hii tukiangalia elimu uwekezaji wake ukoje? Hii triliioni 1.101 ambayo imewekezwa hiyo ni *package* moja ya elimu bila malipo peke yake, ukiachia suala

la miundombinu, shule kongwe ambazo zilikuwa taabani kabisa, leo katembelee shule kongwe nyingine zipo kama *university*, ni kazi kubwa lazima tu-*appreciate*, hali imebadilika ndugu zangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla ni kwamba kazi kubwa imeendelea kufanyika, lakini naomba niseme kwamba michango tumeichukua kwa ajili ya kwenda kuifanya kazi. Kuna ajenda ya suala zima la ajira, tumeongea na ndugu yangu Mheshimiwa Mkuchika tusiwalishe shughuli, yeeye atakuja kutoa watu walioajiriwa na mipango ya ajira na taarifa yake inakuja kesho. Kwa hiyo, jambo hili kaka yangu Mheshimiwa Mkuchika, mkubwa na mzee wangu atakuja kulifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiujumla hoja ni nyingi, lakini zote naomba niwahakikishie kwamba tutatoa majibu yake na kuziwasilisha vizuri kwa maandishi na kila Mheshimiwa Mbunge ataweba kuititia majibu ya maeneo mbalimbali. Niwashukuru Wabunge wote tuliochangia hoja hizi kwa ujumla wake. Nimewasikia akina Mheshimiwa Mchengerwa, Mheshimiwa Mkuchika mpaka baadhi ya Mawaziri; pia namshukuru sana Mheshimiwa Kairuki naye ukapenyeza na ndugu yangu Mheshimiwa Ulega akapenyeza kwa ajili ya watu wa Mkuranga. Kwa ujumla naomba niseme kwamba tunaheshimu michango ya Wabunge wote na bahati nzuri yote itabakia katika *Hansard* zetu za Bunge kwa ajili ya kuhakikisha kwamba bajeti ya Ofisi ya TAMISEMI ambayo inalenga wananchi iweze kutatua matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haya sasa, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yenye jumla ya Sh.7,019,800,353,000 kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI; Fungu 56 - Tume ya Utumishi wa Walimu; Fungu 2, Mafungu 26 ya Mikoa yakijumuisha Halmashauri 185. Kati ya fedha zinazoombwa Sh.4,729,880,457,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yanayojoumuisha na mishahara ya Sh.3,878,738,058,000 na Sh.851,142,339,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, jumla ya Sh.2,289,919,896,000

zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, Sh.1,296,949,390,000 ni fedha za ndani na Sh.992,970,506,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha maelezo haya, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa hoja zote za Waheshimiwa Wabunge zitajibiwa kwa maandishi kama ilivyo ada yetu kwa siku zote za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza haya sasa, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, tukae tutaendelea na utaratibu wetu. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya mabadiliko ambayo tumeyafanya kwa ajili ya uendeshaji wa Bunge kipindi hiki, kwa sababu hatuhoji vifungu lakini nimeletewa hapa majina kwa uwakilishi wa vyama vilivyopo hapa kwa Waheshimiwa Wabunge wanaotaka au wanaohitaji ufanuzi kwenye mshahara wa Waziri. Kwa hivyo, nitawapa fursa hawa ili Mheshimiwa Waziri apate fursa ya kutoa ufanuzi halafu baadaye ndio tutahitimisha ili hii hoja ya bajeti na Waheshimiwa Wabunge mnaendelea kupiga kura zenu kwenye hii bajeti, kwa hiyo nitawaambia hapo baadaye.

Waheshimiwa wanaotaka ufanuzi kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutaanza na Mhesimiwa Mary Pius Chatanda.

HOJA ZA KISERA

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba tu nipate ufanuzi kwenye maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri juu ya ujenzi na ukarabati wa zahanati, vituo vyta afya pamoja na hospitali. Kwa bahati mbaya sijasikia vizuri suala la ukarabati wa hospitali zile kuu kuu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi,

je, zile hospitali za muda mrefu zitapewa fedha kwa ajili ya ukarabati?

Mheshimiwa Naibu Spika, lilikuwa ni hilo tu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA

NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukarabati kama nilivyosema lengo letu kubwa ni kwamba hospitali zote ziwe katika hali nzuri ya kutoa huduma ya afya. Ndiyo maana ukija kuangalia utaona licha ya ujenzi wa zile hospitali 98 lakini tuna ukarabati wa takriban hospitali 21. Lengo letu ni kwamba hospitali zote za halmashauri ikiwepo na Hospitali ya Magoma kwa mama yangu Mheshimiwa Mary Chatanda, hospitali ya Mwanga, hospitali ya Mheshimiwa Mwakyembe kule Kyela, zote tumezibainisha ofisini kwetu. Kwa hiyo, lengo kubwa ni kwamba hospitali zote tutaziweka katika mpango wa ukarabati ili wananchi waweze kupata huduma vizuri.

NAIBU SPIKA: Kabla sijamuita wa pili anayetaka ufanuzi, niwakumbushe katika dakika moja ijayo zoezi la kupiga kura litafungwa. Kwa hiyo, Mbunge ye yeyote ambaye bado hajapiga kura ana fursa hiyo katika dakika moja ijayo zoezi hilo litafungwa.

Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, ulikuwa unahitaji ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri?

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na pongezi nzuri kwa Serikali nataka tu kupata *commitment* ya Serikali juu ya 2% ya watu wenye ulemavu kwa sababu katika baadhi ya maeneo kwa kweli kumekuwa na changamoto ambapo sheria inataku kwamba wajunge vikundi kuanzia vya watu 5 – 10 lakini baadhi ya kwenye kata utakuta kwamba idadi hiyo ya watu wenye ulemavu inakosekana. Kwa maana kwamba kama vigezo vingelegezwa au kungekuwa na mabadiliko ya sheria hiyo

hata mtu mwenye ulemavu mmoja mwenye sifa anaweza akachukua mkopo huo na akaweza kuutumia kwa mahitaji yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tu katika Jiji la Dar es Salaam ambalo limefanya vizuri sana katika hii 2%, wamefikia mpaka kukopesha bajaj. Kwa hiyo, kama ni mmoja akipata bajaj na anaendesha yeche na halmashauri nyingine zikafanya hivyo kwa kuangalia ni kwa jinsi gani tunawawezesha hawa watu wenye ulemavu, naamini kabisa kwamba lile lengo la kuwakomboa na kuwaondoa katika ile hali ya kuwa tegemezi itasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata ufanuzi wa Serikali katika hili. Kama ni sheria basi katika Bunge hili waweze kuleta kwenye ile *Finance Bill* tufanye hayo mabadiliko au kama ni sheria ndogo basi hizo kanuni pia ziweze kubadilika. Ahsante

NAIBU SPIKA: Ufanuzi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana lakini nimshukuru Mheshimiwa Amina Mollel kuhusu jambo hilo. Vilevile jambo hili lilikuja katika Kamati ya Bunge na hata Kamati ya *LAAC* na hata mikoa mingi wakati wanawasilisha bajeti zao lakini kwa bahati mbaya liko ndani ya sheria siyo kanuni, kwa hiyo, lazima tufanye mabadiliko ya sheria. Tumelichukua jambo hili na sasa hivi tunalifanyia mchakato kuona nini kifanyike kwa mujibu wa sheria na lengo kubwa siyo walemvu peke yake hata yale makundi ya vijana wakati mwingine ushauri umetolewa kwamba kwa nini isiwe hata watu watano, kwa nini iwe watu 10, inawezekana watu hamkubaliani. Kwa sababu sheria ndiyo tulikuwa tumeanza kuitekeleza baadhi ya changamoto tumeziona lengo letu ni kuboresha zaidi. Kwa hiyo, jambo hili tunalifanyia kazi ofisini kuona jinsi gani tutafanya hata kama baadaye tuirekebishe sheria kuhakikisha kwamba kila mtu anapata haki vizuri kuhusu mikopo hii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Raphael Jafary Michael, ufanuzi.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu kama Msemaji wa Kambi nilizungumzia suala la mapato ya halmashauri na bahati mbaya Mheshimiwa Waziri hajazungumzia sana hapo. Hoja yangu ni kwamba ili Wizara ya TAMISEMI iwepo maana yake lazima halmashauri zifanye kazi vizuri kwa sababu TAMISEMI ni halmashauri. Kwa hiyo, sifa zote hizi ukizitafuta lazima halmashauri zifanye kazi vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kubadilisha sheria na kuruhusu Kamishna wa Kodi akishirikiana na Waziri wa Fedha kuchukua baadhi ya vyanzo, halmashauri nydingi zimeanza kuyumba au kupata mkwamo katika utendaji wake. Imefika mahali ambapo sasa halmashauri zinaanza kubuni vyanzo *very petty*, vile vidogo vidogo hata vya kuumiza wananchi. Kwa mfano, halmashauri zinaweza zikafika mahali zinataka kwenda kwenye kumbi za starehe au kwenye sherehe mbalimbali kuanza kuchukua kodi ndogo ili ziweze kuijendesha jambo ambalo halizisaidii halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kazi kubwa ya Serikali Kuu ni kuzi-*regulate* halmashauri kwa maana ya kuzisimamia na kuhakikisha kwamba zinatoa usimamizi mzuri kule kwenye halmashauri. Kwenye michango mingi Wabunge wengi wanashukuru kwa sababu wamepelekewa fedha kule kwenye halmashauri maana yake mtazamo uliopo kwa Serikali Kuu ni kuhakikisha zile halmashauri zinapotea kabisa kwa sababu Serikali Kuu ndio itakuwa kila kitu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kengele imeshagonga.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja.

NAIBU SPIKA: Sasa na yeye inabidi nimpe fursa atoe ufanuzi.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja tu namaliza.

NAIBU SPIKA: Haya malizia.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilichokuwa naomba ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri, baada ya kuangalia hii *performance* ya miaka miwili tangu baadhi ya vyanzo vya mapato vya halmashauri kuchukuliwa Serikali Kuu na utendaji wa halmashauri ulivyo kwa sasa, haoni ni wakati sasa wa ku-revise ile sheria ili vyanzo vya mapato virudishwe halmashauri ili zisiendelee kukwama kama ambavyo zinakwama sasa? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Japhary Michael kwa uungwana wake. Amekuwa muungwana sana, mara nyingi ametoa ushauri mzuri na siyo hapa hata nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili niseme kwamba lengo kubwa la Serikali ni kuhakikisha mambo ndani ya nchi yanakwenda. Suala zima la kodi ya majengo ambalo sasa linasimamiwa na *TRA*, kwa ujumla wake Serikali ilifanya vile kuangalia jinsi gani tunaweza kwenda mbele zaidi kuhakikisha kwamba lile kundi kubwa likikusanywa liweze kutawanywa katika maeneo mbalimbali mradi halmashauri mbalimbali ziweze kupata fursa nzuri. Ndiyo maana hapa katikati tukaweza kubuni hata utaratibu wa miradi mikakati kwa ajili ya kuziwezesha halmashauri mbalimbali kupitia fungu

linalokusanywa kwa kiwango kikubwa kugawanywa katika halmashauri mbalimbali hata zile zisizokuwa na uwezo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni jinsi gani tunaweza kuhakikisha tunaongeza misuli ili fedha hizi zinakusanywe vizuri, jambo hili kuptitia Wizara ya Fedha kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango anaendelea kulifanya kazi. Kwa hiyo, nadhani tuwe na subira tu, lengo kubwa la Serikali ni kila jambo liende vizuri. Kaka yangu wala usiwe na hofu Serikali inafanya tathmini kwa kina hata kuangalia makusanyo ya sasa hivi, je, tunakusanya inavyotakiwa? Je, nini kifanyike zaidi kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu zinafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo hili linafanyiwa kazi vizuri na Serikali ili kusaidia nchi iweze kwenda mbele.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi nahitaji kupata ufanuzi kwenye suala zima la maabara. Sijaona na napata shaka sana kama hakuna mpango mkakati mahsus na wa msukumo mkubwa sana kwenye kumaliza maabara zetu. Nilitarajia kama ambavyo tunasema 'Nyumba ni Choo', basi kwenye upande wa sekondari tungekuwa na hata kauli mbiu inayosema 'Sekondari ni Maabara'.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuakisi uchumi wa viwanda bila kuwa na wanasyansi. Nchi nzima tuko chini ya 20%, sisi kwetu Dodoma hapa tuko asilimia 15, Kondoa kule tuko kwenye asilimia 10. Kama ambavyo tuliweka mkakati kwenye vituo vya afya mpaka leo tumejenga vituo 433, kwenye upande wa maabara tuna mkakati gani mahsus huenda tukasema ni wa dharura ambao utatutoa kwenye tatizo hili ili wanafunzi wetu wa sekondari wafanye mazoezi kwa vitendo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima leo ni kama umefungulia, hamna kitabu hapo cha kusoma? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- TAMISEMI, ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA

NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumshukuru kaka yangu Mheshimiwa Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini kwa hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeliona hilo na ndiyo maana ukiangalia katika mpango wetu wa mwaka huu kwa mara ya kwanza tumekuja na bajeti ya shilingi bilioni 64.32 kwa ajili ya ujenzi wa maabara. Hii ni *package* ya maabara peke yake katika bajeti ya mwaka huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Kwa mara ya kwanza tutaona kila halmashauri ukiachia mipango ya halmashauri yenyewe lakini Serikali Kuu huku kwa ujumla wake, tunawezesha ujengaji wa maabara hizo zenye thamani ya shilingi bilioni 64.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kumuarifu Mheshimiwa Sannda kwamba hivi sasa jambo hilo tumeshalifanyia kazi aondoe hofu tu. Kitu kikubwa tukienda katika ujenzi wa maabara niwaombe Waheshimiwa Wabunge twende tukasimamie *value for money* ipatikane kwa ajili ya kuhakikisha maabara hizi zinajengwa katika maeneo yetu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa, kwenye mchango wangu nilimpa mpaka na mfano wa utofauti mkubwa wa ukubwa wa maeneo yetu lakini pia na idadi ya watu ambao ndiyo unatupelekea kuangalia namna gani ya kugawa hizi rasilimali chache

tunazokuwa nazo. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba TAMISEMI ni wasikivu na wanalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukubaliane kwamba jambo hili kwa namna moja au nyingine limeleta tofauti kubwa sana ya kimaendeleo kati ya eneo moja na lingine. Hili ni eneo muhimu na nchi hii ni ya kwetu sote na wananchi wetu wanahitaji maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu Mheshimiwa Waziri atuambie wanalifanyia kazi kwa namna ipi? Au kama Wizara kwa maana ya Serikali wana-*commitment* gani kwenye jambo hili la mgawanyo hasa kwa hizi zahanati na maabara kwa kuzingatia ukubwa wa maeneo yetu, idadi ya watu na changamoto za kimaendeleo tulizokuwa nazo kwenye maeneo yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ufanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mnzava, Mbunge wa Korogwe, kwa hoja yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwamba hoja hii ilitolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi siku ile akina Mheshimiwa Keissy, Mbunge wa Serengeti naye alileta mpaka kimemo hapa, kila mtu alileta hoja yake hiyo. Nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango tulikuwa tunalifanyia kazi jambo hili ili kuona ni jinsi gani tuna-*address* jambo hili kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili kwa ujumla wake tumelifanyia kazi kwa kuangalia maslahi mapana ya nchi na maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, wala asihofu katika eneo hili limefanyiwa kazi.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante tena. Naomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, wilaya yetu imekuwa wilaya toka mwaka 1985, kuna wilaya nyingi sana zimekuja baadaye hata muda mfupi uliopita. Napenda kujua ni lini Mji Mkuu wa Wilaya ya Hanang utakuwa na barabara ya lami kama miji mingine ya wilaya. Pia nilimuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu nitashukuru sana watu wa Hanang wakisikia tumesubiri lakini sasa itakuwaje kusudi na sisi tupate hiyo *privilege* kama zilivyopata wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, kabla hujajibu labda kama unazijibbia wilaya zote za nchi hii kwa sababu swali hilo liko mahsusni na mimi sitaki kukuweka mazingira ambayo unaweza usiwe umeishika taarifa hiyo ya Hanang peke yake. Labda kama unajibu kwa ujumla una mpango gani kwa barabara za wilaya.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali, lengo letu kubwa kwanza ni katika makao ya wilaya zetu; tumeanza manispaa, miji pamoja na majiji kwa kuimarissha miundombinu kwa barabara za lami. Hapa katikati tulikwenda na halmashauri nadhani takribani 64 tumegusa makao makuu yake kuanza kuweka tabaka la lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba mpango wetu kama nchi kwa sababu tuko katika kutafuta fursa za mbalimbali za kifedha ili kuboresha miundombinu ya maeneo mbalimbali kwa sababu tunajua yakiboreka hata uchumi wa eneo hili utaweza kukua. Huo ndiyo mpango wetu, ndiyo maana unaona mwaka huu tumeongeza imefika halmashauri 45 lakini kuna *package* za halmashauri za wilaya hazipo katika *component* hii. Ni imani yetu siku zijazo tutagusa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

halmashauri zote kwa kadri iwezekanavyo kutokana na juhudii kubwa inayofanywa na ofisi yetu ya kutafuta fedha katika vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu Wabunge wengine wapo kwenye vyumba vingine vya mikutano na kwa utaratibu ambao Mheshimiwa Spika alikuwa ameshatuelekeza, kwa hivyo, sitawahoji kwa sababu kura zimeshapigwa na ninazo hapa. Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI ni kuomba kiasi cha shilingi 7,019,800,353,000 na kwa kura hizi nazoziona hapa, kwa sababu utaratibu wetu kwa hatua hii hatupigi kura moja moja, ningeweza kuwaambia kwa halisi nani amepiga kura gani, lakini kura jumla ya kura zote ni 316 na Wabunge walio wengi katika kura hizo wameikubali hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ya mapato na matumizi ya yake kwa mwaka wa fedha 2020/2021. (*Makofi*)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021 – Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yaliridhiwa na Bunge kama ifuatavyo:

MATUMIZI YA KAWAIDA

| | |
|--|----------------------|
| Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa..... | Sh.125,400,121,000/= |
| Fungu 02 - Tume ya Utumishi wa Walimu...Sh.14,273,473,000/= | |
| Fungu 036 - Katavi.....Sh.59,076,582,000/= | |
| Fungu 047 - Simiyu.....Sh.134,649,785,000/= | |
| Fungu 054 -Njombe.....Sh.126,967,531,000/= | |
| Fungu 063 - Geita.....Sh.158,994,551,001/= | |
| Fungu 070 – Arusha | Sh.215,030,234,000/= |
| Fungu 071 - Pwani.....Sh.198,415,266,000/= | |
| Fungu 072 - Dodoma.....Sh.204,501,008,000/= | |
| Fungu 073 - Iringa.....Sh.147,453,866,000/= | |
| Fungu 074 – Kigoma.....Sh.143,114,307,000/= | |

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

| | |
|--------------------------------|----------------------|
| Fungu 075 - Kilimanjaro..... | Sh.213,331,298,000/= |
| Fungu 076 – Lindi..... | Sh.111,825,922,000/= |
| Fungu 077 – Mara..... | Sh.187,352,312,000/= |
| Fungu 078 – Mbeya..... | Sh.222,160,522,000/= |
| Fungu 079 - Morogoro..... | Sh.249,646,714,000/= |
| Fungu 080 - Mtwara..... | Sh.146,917,941,000/= |
| Fungu 081 - Mwanza..... | Sh.287,001,600,000/= |
| Fungu 082 - Ruvuma..... | Sh.162,167,842,000/= |
| Fungu 083 - Shinyanga..... | Sh.137,473,046,000/= |
| Fungu 084 - Singida..... | Sh.127,671,534,000/= |
| Fungu 085 – Tabora..... | Sh.174,661,215,000/= |
| Fungu 086 - Tanga..... | Sh.249,000,377,000/= |
| Fungu 087 - Kagera..... | Sh.198,528,304,999/= |
| Fungu 088 - Dar es Salaam..... | Sh.390,883,502,000/= |
| Fungu 089 - Rukwa..... | Sh.92,347,995,000/= |
| Fungu 090 - Songwe..... | Sh.100,783,593,000/= |
| Fungu 095 - Manyara..... | Sh.150,250,015,000/= |

MIPANGO YA MAENDELEO

| | |
|--|----------------------|
| Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa..... | Sh.578,047,184,000/= |
| Fungu 02 - Tume ya Utumishi wa Walimu..... | Sh.500,000,000/= |
| Fungu 036 – Katavi..... | Sh.30,151,930,500/= |
| Fungu 047 - Simiyu..... | Sh.55,832,815,000/= |
| Fungu 054 - Njombe..... | Sh.48,267,082,500/= |
| Fungu 063 - Geita..... | Sh.59,099,297,000/= |
| Fungu 070 – Arusha..... | Sh.88,297,300,500/= |
| Fungu 071 - Pwani..... | Sh.74,538,002,000/= |
| Fungu 072 - Dodoma..... | Sh.109,746,176,000/= |
| Fungu 073 - Iringa..... | Sh.42,579,896,000/= |
| Fungu 074 – Kigoma..... | Sh.80,797,638,000/= |
| Fungu 075 - Kilimanjaro..... | Sh.49,945,646,500/= |
| Fungu 076 – Lindi..... | Sh.50,200,781,500/= |
| Fungu 077 – Mara..... | Sh.64,299,129,000/= |
| Fungu 078 – Mbeya..... | Sh.64,421,521,500/= |
| Fungu 079 - Morogoro..... | Sh.67,411,617,000/= |
| Fungu 080 - Mtwara..... | Sh.66,275,367,000/= |
| Fungu 081 - Mwanza..... | Sh.95,145,842,000/= |
| Fungu 082 - Ruvuma..... | Sh.57,647,491,000/= |

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

| | |
|--------------------------------|----------------------|
| Fungu 083 - Shinyanga..... | Sh.56,760,291,500/= |
| Fungu 084 - Singida..... | Sh.52,515,526,500/= |
| Fungu 085 - Tabora..... | Sh.67,077,260,500/= |
| Fungu 086 - Tanga..... | Sh.75,382,161,000/= |
| Fungu 087 - Kagera..... | Sh.77,566,071,500/= |
| Fungu 088 - Dar es Salaam..... | Sh.159,398,557,500/= |
| Fungu 089 - Rukwa..... | Sh.33,041,074,000/= |
| Fungu 090 - Songwe..... | Sh.37,396,326,500/= |
| Fungu 095 - Manyara..... | Sh.47,577,910,000/= |

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi wa hoja mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge walizitoa kupitia Kamati lakini pia kupitia michango mbalimbali ambayo imetolewa hapa ndani. Pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri miliyofanya kwenye ngazi ya Kamati kwa niaba ya Bunge zima. Tumepata fursa ya kusikia Wabunge waliokuwa sehemu ya Kamati na ambao hawakuwa sehemu ya kamati wakieleza yale ambayo Wizara hii imeyafanya. Kwa hiyo, tunawashukuru kwa kazi nzuri Waheshimiwa Wabunge wote, mmetoa michango mingi sana ambayo naamini itaboresha utendaji kazi wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Kwa namna hiyo hiyo, kwa niaba yenu niwapongeze sana TAMISEMI kwa kupitishiwa mafungu yenu na hii bajeti mliyoiomba. Tunaamini kwa utendaji kazi mlisosifiwa kwa asilimia zaidi ya 90 kwa tathmini iliyotolewa hapa bajeti hii itasaidia kusogeza maendeleo zaidi kwa wananchi na nyie itawaongezea ufanisi mkubwa zaidi kuliko kule tulikotoka kwa sababu mmeefanya kazi nzuri tunaamini mtaendelea kufanya kazi nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya Jumatano, saa Nane Kamili Mchana.

*(Saa 11.58 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 15 Aprili, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*